AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int

**BARAZA KUU**
**Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Nane**
**11-12 Februari 2026**
**Addis Ababa (ETHIOPIA)**

**EX.CL/Dec.1323- 1351(XLVIII)**
Lugha Chanzi: Kiingereza

# MAAMUZI

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI ZA KAMATI NDOGO ZA KAMATI YA WAWAKILISHI WA KUDUMU (PRC)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** mapendekezo ya PRC kuhusu ripoti za Kamati zake Ndogo, likizingatia maoni yaliyotolewa na Nchi Wanachama.

## I. KUHUSU KAMATI NDOGO JUU YA MAGEUZI YA MUUNDO - EX.CL/1635(XLVIII)

2. **LINAKUMBUKA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.920(XXXVIII) na Uamuzi EX.CL/Dec.1310(XLVII), uliopitishwa katika Mkutano wa Kawaida wa 47 wa Baraza Kuu uliofanyika tarehe 10–11 Julai 2025 huko Malabo, Equatorial Guinea, hasa vifungu vyake vinavyoiomba PRC, kwa usaidizi wa Kamisheni, kukamilisha mapitio ya vyombo vilivyobaki na kuwasilisha ripoti kwa Baraza Kuu;

3. **LINAZINGATIA** ripoti Iliyounganishwa ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Mageuzi ya Miundo kuhusu uchunguzi wa mapendekezo ya mageuzi ya kitaasisi kwa kipindi cha kuanzia tarehe 23 Septemba hadi 19 Novemba 2025, na LINAIPONGEZA Kamati Ndogo ya PRC kwa maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa kazi yake;

4. **LINAIOMBA** PRC, kupitia Kamati Ndogo yake ya Mageuzi ya Miundo, kuendelea na kazi yake, kwa kutumia mbinu ya kesi kwa kesi kwa kuzingatia upekee wa kila chombo, na kuwasilisha ripoti kamili kuhusu vipengele vilivyobakia vya mchakato wa mageuzi ya kitaasisi kwenye Mkutano ujao wa Kawaida wa Baraza Kuu ifikapo Januari 2027.

5. **LINAIOMBA ZAIDI** PRC, kwa kushirikiana na Kamisheni na Kamati ya Mawaziri ya F15 kuwasilisha ripoti kamili inayoelezea athari za kifedha, kimuundo na kisheria kwenye mazingira ya mageuzi yanayopendekezwa ya miundo yote inayofanyiwa mapitio, ikiwa ni pamoja na urekebishaji wa miundo iliyopo yenye mamlaka yanayoingiliana na yanayorudiwa pamoja na kwenye vituo vya huduma za usaidizi vya kikanda vilivyopendekezwa kwenye mkutano ujao wa Wakuu wa Nchi na Serikali kupitia Baraza Kuu;

6. **KWA KUTAMBUA** haja ya kuhakikisha uwakilishi sawia wa Nchi Wanachama ndani ya miundo iliyorekebishwa ya AU, **LINAIAGIZA** Kamisheni kwa kushirikiana na PRC kuwasilisha taarifa mpya za mara kwa mara kwa Baraza Kuu, kwa kuzingatia maamuzi ya awali kuhusu SACA, kwa mujibu wa uamuzi EX.CL/Dec.1031(XXXIV) wa Mkutano wake wa Kawaida wa 34 kuhusu, i)

kuendeleza idadi ya ukomo husika ndani ya mfumo wa AU kwa Nchi Wanachama ambazo hazina uwakilishi wa kutosha na ii) orodha kamili ya wafanyakazi wanaofadhiliwa kupitia rasilimali za fedha za nje na zisizo za Kiafrika na hatua za mabadiliko zilizochukuliwa kushughulikia hali hii;

7. **LINATAMBUA** jukumu la usaidizi ambalo Ofisi za Uhusiano za Umoja wa Afrika(AULOs) zinafanya katika kukuza amani na usalama pamoja na ujenzi mpya na maendeleo baada ya migogoro na kuhusu haja ya kuhakikisha usimamizi mzuri na sahihi wa ofisi hizi, **LINAAGIZA** PRC kwa kushirikiana na Kamisheni na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs), kukamilisha mfumo wa kitaasisi uliooanishwa kwa ajili ya usimamizi wa ofisi za uhusiano, ikiwa ni pamoja na miongozo iliyo wazi kuhusu vigezo vya kuanzisha biashara mpya, ufadhili unaotabirika na endelevu, muundo sanifu na rasilimali watu na za kiufundi zinazofaa pamoja na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini na kuwasilisha haya kwenye mkutano wa kawaida wa 50 wa Baraza Kuu mwezi Januari 2027. **LINAAGIZA ZAIDI** kwamba kufungwa na kuanzishwa upya kwa AULOs zilizotambuliwa kulingana na maamuzi yaliyopita ya Wakuu wa Nchi na Serikali, kufanyike kwa mujibu wa sheria na taratibu za kifedha na kiutawala.

8. **LINAAGIZA** Kamisheni kuharakisha uwasilishaji wa mapendekezo yote ya mageuzi ya kitaasisi yaliyosalia kwa wakati, ikiwa ni pamoja na yale ambayo hayajakushughulikiwa chini ya tathmini ya mshauri, na kuhakikisha ushirikiano kamili na Kamati Ndogo ya PRC katika uendeshaji wa kazi yake.

9. **LINAISIHI** Kamisheni kushughulikia, kama jambo la kipaumbele, changamoto za kitaasisi zinazojirudia zilizoainishwa na Kamati Ndogo, kwa kufuata kikamilifu maamuzi ya Wakuu wa Nchi na Serikali na Baraza Kuu na kulingana na vipaumbele vitakavyoainishwa na Kamati Ndogo kwa uratibu na Kamisheni.

10. **LINASISITIZA** umuhimu wa kukamilisha bila kuchelewa kuandaliwa kwa pendekezo la kuoanisha uainishaji wa nafasi zote za AU, ikiwa ni pamoja na zile za Wakuu wa vyombo vya AU, na kuliwasilisha kwa ajili ya kupitishwa, kulingana na utaratibu uliowekwa, kwa vyombo vya kufanya maamuzi vya AU ifikapo Juni 2026, kwa mujibu wa uamuzi EX.CL/Dec.1265(XLV), aya ya (39); **LINAIOMBA** Kamisheni kuunda utaratibu wa kisheria unaoainisha sifa na hadhi za kisheria za vyombo vya AU, na kuuwasilisha kwa ajili ya kupitishwa, kulingana na utaratibu uliowekwa, kwa vyombo vya kufanya maamuzi vya AU ifikapo Juni 2026.

## II. KUHUSU KIKAO CHA PAMOJA CHA KAMATI NDOGO YA USIMAMIZI NA URATIBU WA JUMLA WA MASUALA YA BAJETI, FEDHA NA UTAWALA NA WATAALAMU WA KIUFUNDI WA KAMATI YA MAWAZIRI KUMI NA WATANO WA FEDHA (F15) - EX.CL/1636(XLVIII)

11. **LINAZINGATIA** ripoti za Kikao cha Pamoja cha Kamati Ndogo za PRC za Usimamizi na Uratibu wa Jumla wa Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala na Wataalamu wa Kiufundi wa F-15.

## A. Ripoti ya Utendaji ya Nusu Mwaka kuhusu Bajeti ya AU ya 2025

**12.** **LINAZINGATIA** Ripoti ya Utendaji ya Nusu Mwaka ya 2025 na **LINAELEZA** wasiwasi kuhusu viwango vya chini vya utekelezaji vya baadhi ya Vyombo na Ofisi na **LINAKUMBUKA** aya ya 88 ya uamuzi EX.CL/Dec.1189(XLII) kuhusu utekelezaji wa bajeti, na **LINAAGIZA** Vyombo na Ofisi zenye viwango vya utekelezaji vilivyo chini ya asilimia hamsini (50%) kuwasilisha mipango ya hatua za marekebisho kwa PRC kupitia GSCBFAM kwa ajili ya kujadiliwa kabla ya mkutano ujao wa kawaida wa Baraza Kuu mnamo mwezi Juni 2026.

**13.** **LINAAGIZA** kufuata ipasavyo utekelezaji wa aya ya 88 (xiv) ya uamuzi EX.CL/Dec.1189(XLII) kuhusu kuidhinishwa kwa Bajeti za Ziada, na **LINAIAGIZA ZAIDI** PRC, kupitia Kamati Ndogo yake husika, kujadili utekelezaji wa bajeti ya nusu mwaka kabla ya kujadiliwa kwa mapendekezo yoyote ya bajeti ya ziada.

**14.** **LINAAGIZA** Vyombo na Ofisi zote za AU kuwasilisha ripoti zao za utendaji wa bajeti ya nusu mwaka na ya mwaka ndani ya muda uliowekwa.

**15.** **LINASISITIZA** haja ya kuendelea kuimarisha vitendo vya Usimamizi unaozingatia Matokeo na utamaduni wa utendaji ikiwa ni pamoja na ujumuishaji wa lazima wa utoaji ripoti wa kiufundi wa AMERT na utekelezaji wa kifedha kote katika Umoja wa Afrika.

**16.** **LINASISITIZA** kwamba ripoti zijazo za utendaji zinapaswa kujumuisha uhusiano wazi kati ya matokeo ya programu na matumizi ya bajeti ili kuimarisha uwajibikaji.

**17.** **LINAAGIZA** Kamisheni na Vyombo vingine kuharakisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kuhusu vifaa vya wafanyakazi, ununuzi, na ufuatiliaji ili kushughulikia changamoto zilizoainishwa ndani ya bajeti iliyoidhinishwa na kutoa ripoti kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika kutekeleza hatua hizi katika Mkutano ujao wa Kawaida wa Baraza Kuu.

**18.** Likikumbuka maamuzi EX.CL/Dec.1265(XLV) ya Julai 2024, EX.CL/Dec.1279(XLVI) ya Februari 2025, na EX.CL/Dec.1310(XLVII) ya Julai 2025 kuhusu uendeshaji wa utafiti wa upembuzi yakinifu kuhusu pendekezo la kulipa sehemu ya michango iliyotathminiwa katika sarafu za kitaifa; **LINAELEZA WASIWASI** kwamba, licha ya maamuzi matatu ya Baraza Kuu tangu Julai 2024, hakuna utafiti wa upembuzi yakinifu au ripoti ya maendeleo imewasilishwa hadi sasa; **LINAIAGIZA** Kamisheni, kwa kushirikiana na Wataalamu wa F15, kufanya na kukamilisha kwa haraka utafiti wa upembuzi yakinifu kwa mujibu wa Sheria za Fedha za AU; na **LINAOMBA** kwamba ripoti ya utafiti iwasilishwe kwenye mkutano ujao wa Baraza Kuu kwa ajili ya kujadiliwa.

19. **LINAAGIZA** Vyombo na Ofisi za AU kuwasilisha ripoti za utendaji wa bajeti za robo mwaka na kupitia na kushughulikia utendaji mdogo ndani ya siku 30 za uwasilishaji wa ripoti.

### B. Marekebisho ya Bajeti ya AU ya 2025 (Ziada)

20. **LINAIDHINISHA** bajeti kuu ya AU ya 2025 ya ziada ya **dola za Marekani 8,137,217,** kama ifuatavyo:

i) Bajeti ya Uendeshaji ya AU ya **dola za Marekani 5,889,169,** itakayofadhiliwa na Fedha za Akiba za AU.

ii) Bajeti ya Programu ya AU ya **dola za Marekani 2,248,048,** itakayofadhiliwa kama ifuatavyo:

- Dola za Marekani 1,392,700 kutoka Fedha za Akiba za AU
- Dola za Marekani 236,707 kutoka Mfuko wa Matengenezo wa AU
- Dola za Marekani 618,641 kutoka kwenye Michango ya Hiari ya Nchi Wanachama

21. **PIA LINAIDHINISHA** Bajeti ya fedha ya ufadhili yenye kiasi cha **dola za Marekani 6,067,000**, inayofadhiliwa na Wabia kwa ajili ya Kamisheni.

Marekebisho ya Bajeti ya Au ya 2025

| Chombo | Uendeshaji | Programu | | | | | Ziada 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Fedha ya Akiba | Mfuko wa Matengenezo | Fedha ya Akiba | Michango ya Hiari ya Nchi Wanachama | Wabia | Jumla | Uendeshaji | Programu | Jumla |
| AUC | **3,078,272** | 236,707 | 1,117,080 | 21,711 | | **1,375,498** | 3,078,272 | 1,375,498 | **4,453,770** |
| PAP | **358,000** | | | | | **-** | 358,000 | - | **358,000** |
| AfCHPR (Mahakama) | **-** | | 200,620 | | | **200,620** | - | 200,620 | **200,620** |
| AUDA-NEPAD | **861,774** | | 75,000 | 538,980 | | **613,980** | 861,774 | 613,980 | **1,475,754** |
| Bodi ya Ushauri kuhusu Rushwa | **149,736** | | | | | **-** | 149,736 | - | **149,736** |
| APRM | **453,733** | | | | | **-** | 453,733 | - | **453,733** |
| AFREC | **337,631** | | | | | **-** | 337,631 | - | **337,631** |
| PAU | | | - | 57,950 | | **57,950** | - | 57,950 | **57,950** |
| AfCDC | **650,023** | | | | | **-** | 650,023 | - | **650,023** |
| **Bajeti ya Kawaida ya Jumla** | **5,889,169** | **236,707** | **1,392,700** | **618,641** | **-** | **2,248,048** | **5,889,169** | **2,248,048** | **8,137,217** |
| AUC (*Pass-through*) | | | | | 6,067,000 | **6,067,000** | | 6,067,000 | **6,067,000** |
| **Jumla Kubwa** | **5,889,169** | **236,707** | **1,392,700** | **618,641** | **6,067,000** | **8,315,048** | **5,889,169** | **8,315,048** | **14,204,217** |

**Jedwali la 1:** Marekebisho ya Bajeti ya 2025 (Ziada)

22. **LINAIDHINISHA ZAIDI** mgao mpya wa jumla wa bajeti ya 2025 inayofikia **dola za Marekani 28,977,787**.

| Vyombo | Uendeshaji | | Programu | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Akiba | Mgao mpya | Akiba | Mgao mpya | Akiba | Mgao mpya | Mgao Halisi |
| AUC | | 60,000 | 3,009,884 | 1,323,635 | 3,009,884 | 1,383,635 | **(1,626,249)** |
| PAP | 405,000 | 405,000 | 462,649 | 50,000 | 867,649 | 455,000 | **(412,649)** |
| AfCHPR-Mahakama | | | - | 24,386 | - | 24,386 | **24,386** |
| ACHPR-Kamisheni | | 239,130 | - | - | - | 239,130 | **239,130** |
| ECOSOCC | 83,906 | 83,906 | - | - | 83,906 | 83,906 | **-** |
| AUDA-NEPAD | | | 13,414,500 | 14,525,116 | 13,414,500 | 14,525,116 | **1,110,616** |
| AUABC | 107,566 | 107,566 | 38,694 | 38,694 | 146,260 | 146,260 | **-** |
| ACERWC | 180,000 | 180,000 | - | - | 180,000 | 180,000 | **-** |
| AFREC | | 2,000 | - | 169,270 | - | 171,270 | **171,270** |
| PAU | 557,760 | | - | 575,760 | 557,760 | 575,760 | **18,000** |
| Africa CDC | | 80,000 | 10,187,816 | 10,187,816 | 10,187,816 | 10,267,816 | **80,000** |
| AOSTI | 87,032 | | - | - | 87,032 | - | **(87,032)** |
| Baraza la Michezo la AU | 16,250 | 16,250 | - | - | 16,250 | 16,250 | **-** |
| AfCFTA | | 132,632 | - | - | - | 132,632 | **132,632** |
| STATAFRIC | 299,130 | | - | 628,516 | 299,130 | 628,516 | **329,386** |
| ACSRM-Mali | 127,600 | | - | - | 127,600 | - | **(127,600)** |
| AUCTC (ACSRT) | | | - | 148,110 | - | 148,110 | **148,110** |
| **Jumla Kubwa** | **1,864,244** | **1,306,484** | **27,113,543** | **27,671,303** | **28,977,787** | **28,977,787** | **0** |

**Jedwali la 2:** Mgao wa AU wa 2025

23. **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1310(XLVII), ambapo kiasi cha dola za Marekani milioni 2.1 kiliidhinishwa kwa ajili ya ukarabati wa Jumba la Afrika (*Africa House*). **LINAKARIBISHA** juhudi za Kamisheni za kukusanya dola milioni 1.3 za Marekani kutoka Afreximbank ili kusaidia ukarabati ndani ya bajeti ya Mradi Maalum wa Miundombinu iliyoidhinishwa na **LINAHIMIZA** Kamisheni kukamilisha mchakato wa ukarabati na kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu maendeleo kwa PRC, kupitia Kamati yake Ndogo ya GSCBFAM Wataalamu wa Kiufundi wa F15.

24. **LINAPONGEZA** juhudi za Mwenyekiti wa AUC, kwa usaidizi wa Makamu Mwenyekiti, kuhakikisha usimamizi mzuri wa rasilimali, hasa kuhusiana na ukubwa wa jumbe zilizoidhinishwa kwa ajili ya kusafiri kwenda kwenye mikutano rasmi ya AU na **LINAIHIMIZA** Kamisheni kuendeleza na kuimarisha juhudi hizi.

## III. KUHUSU KAMATI NDOGO YA MASUALA YA UKAGUZI, USIMAMIZI WA HATARI, NA UZINGATIAJI WA SHERIA - DOC. EX.CL/1637(XLVIII)

**25.** **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamati Ndogo ya PRC ya Masuala ya Ukaguzi, Usimamizi wa Hatari na Uzingatiaji wa Sheria na, **LINAIDHINISHA** mapendekezo yaliyomo ndani yake.

**26.** **LINAAMUA** kwamba utekelezaji wa maamuzi yenye athari za kifedha, hasa yale yanayohusiana na ajira, kujaza nafasi zilizo wazi ndani ya miundo iliyoidhinishwa, mapitio ya mishahara na marupurupu ya wafanyakazi, au vipengee vyovyote vya ziada vya matumizi, vitaanzishwa hatua kwa hatua na kutegemea upatikanaji wa rasilimali fedha zilizoidhinishwa na za kutosha.

## A. KUHUSU RIPOTI KAMILI ZA OIO KUHUSU RIPOTI ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA VYOMBO VYA AU ZA MWAKA 2024

**27.** **LINAELEZEA** wasiwasi wake kuhusu masuala ya ukaguzi yaliyobainika na L**INAWASIHI** mameneja wote wa Umoja wa Afrika kutekeleza mapendekezo yote ya ukaguzi yaliyomo katika ripoti za ukaguzi za utendaji wa bajeti na **LINASISITIZA** umuhimu wa kuimarisha utu wa kifedha, uwazi, na uwajibikaji kote katika Vyombo vya AU, huku kukiwa na msisitizo maalum kwenye kusuluhisa utofauti kati ya SAP, AMERT, na rekodi halisi za benki.

**28.** Kuhusu masuala ya pamoja miongoni mwa Vyombo vyote vya AU **LINAAGIZA** kama ifuatavyo:

i) **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1218 (XLIII) aya ya 64 na **LINASISITIZA** haja ya mafunzo kuhusu matumizi ya SAP na AMERT, pamoja na mchakato wa ufuatiliaji na tathmini kwa Maafisa na Wasimamizi wote wa Ufundi wa Vyombo ili kuboresha matumizi ya mifumo na kuwezesha utoaji wa ripoti kwa ufanisi. **LINAELEKEZA ZAIDI** kuwa uwasilishaji wa kuchelewa wa ripoti za AMERT na utekelezaji mbovu wa mapendekezo ya ukaguzi vinapaswa kuingizwa kwenye tathmini za utendaji za maafisa wanaowajibika.

ii) Vyombo vya Umoja wa Afrika vinapaswa kuimarisha Mikataba ya Makubaliano (MoU) na Wabia na kujumuisha vifungu vya uwajibikaji vinavyovifanya viwe na nguvu zaidi kisheria kwa pande zote mbili ili kuepuka kubadilisha vipaumbele wakati wa utekelezaji wa programu zilizoidhinishwa.

iii) Kamisheni ya AU inapaswa kuboresha mchakato wa bajeti ya nyongeza kwa kuwasilisha mapendekezo ya bajeti ya nyongeza kwa ajili ya kuzingatiwa na Vyombo vya Sera ifikapo mwisho wa Agosti kila mwaka badala ya Oktoba ili kutoa muda wa kutosha kwa Vyombo vya AU

kutekeleza programu na shughuli zingine.

iv) Kamisheni kwa kushauriana na Wataalamu wa F15, wachambue kwa makini viwango vya utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita kwa kila idara, Ofisi, taasisi, na Shirika kabla ya kuidhinisha bajeti za ziada.

29. **LINAELEKEZA** zaidi chombo kimoja kimoja kuhusu masuala maalum kama ifuatavyo:

**a) Africa CDC**

i) Uongozi wa Kamishnei unapaswa kuzungumza na wafadhili na washirika wa utekelezaji ili kuiwezesha OIO kupata fedha za ukaguzi wa nje, kwa mujibu wa sharti la uamuzi wa Baraza Kuu EX.CL/Dec.1265(XLV), aya ya 55 (iii).

ii) Kamisheni inapaswa kuanzisha uchunguzi rasmi kuhusu matumizi ya Mifuko ya Washirika na baadhi ya fedha ambazo hazijatangazwa katika SAP na ambazo hazina nyaraka za uhasibu zinazounga mkono.

iii) Africa CDC inapaswa kuoanisha mipango ya shughuli zake na ratiba za utoaji wa wafadhili ili kuepuka ucheleweshaji wa utekelezaji, na kwa uwazi pamoja na madhumuni ya uwajibikaji, na kunapaswa kuwe na utofautishaji dhahiri kati ya shughuli zilizowekwa chini ya bajeti ya uendeshaji na zile zilizo chini ya bajeti ya programu, haswa kwa ununuzi na rasilimali watu.

iv) Africa CDC kushughulikia kasoro katika ripoti za SAP, kama vile mizani hasi, fomula zisizo sahihi, ili kuhakikisha ulinganifu kati ya AMERT na SAP, pamoja na rekodi halisi za benki.

v) Africa CDC inapaswa kufuata sera za ununuzi na safari za AU, pamoja na Sheria na Kanuni za Fedha za AU na vipengele vya Kanuni na Sheria zilizorekebishwa za Wafanyakazi wa AU.

**b) Kamati ya Afrika ya Wataalamu wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACERWC)**

i) ACERWC inapaswa kupunguza hatua kwa hatua utegemezi wa ufadhili wa washirika, ikihakikisha angalau 50% ya ufadhili unatoka kwa Nchi Wanachama.

ii) ACERWC inapaswa kufanya programu za kubadishana utaalamu kwa njia ya mtandao kila baada ya miaka miwili na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (AfCHPR) na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu

(ACHPR) ili kuhakikisha uendelevu wa ushirikiano kati ya vyombo, ushiriki wa maarifa, na ujenzi wa uwezo katika muktadha wa bajeti ndogo.

**c) Eneo Huria la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA)**

i) Sekretarieti ya AfCFTA inapaswa kuhakikisha kwamba gharama za ushirikiano unaoanzishwa na Nchi Wanachama zinazoalika zinalipwa na Nchi husika zinazoalika na inapaswa kuanzisha bajeti maalum kwa shughuli zinazohusiana na shughuli za uenezaji, ambazo zinaweza kufanywa katika hali ya dharula kwa sababu zinazofaa.

ii) **LINAIAGIZA** AfCFTA kuainisha programu za wazi ambazo zinaweza kukuza utekelezaji wa malengo makuu ya AfCFTA na kuendelea kuwasiliana na wabia kutoa fedha kwa ajili ya programu za AfCFTA.

iii) **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuongeza michango yao kwavajili ya program za AfCFTA.

**d) Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (AfCHPR)**

i) AfCHPR inapaswa kuunda mfumo wa kawaida wa ziara za uhamasishaji ili kuunda ipasavyo muundo wa timu, haswa kwa Wafanyakazi wa Usajili wanaoambatana na Majaji wakati wa ziara za uchechemuzi na uhamasishaji uwandani.

ii) AfCHPR inapaswa kushirikiana na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs) ili kutoa usaidizi kwa ajili ya uidhinishaji na maazimio yaliyosalia.

iii) Kwa mujibu wa Sera ya Usafiri ya AU, maafisa wa Mahakama wanaonufaika na tiketi za usafiri zilizonunuliwa kwa gharama kubwa wanapaswa kufidia gharama za ziada zilizotumika, ikilinganishwa na nauli za kawaida zinazotumika kwenye njia zile zile.

iv) AfCHPR inapaswa kushirikiana na Idara za Fedha za Kamisheni ili kuboresha usawazishaji katika matumizi ya mifumo ya SAP na AMERT, kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa usimamizi wa fedha na kuripoti shughuli za Mahakama.

**e) Mfumo wa Kujifanyia Tathmini wa Afrika (APRM)**

i) APRM inapaswa kuhimiza vikali wabia kutimiza wajibu wao kama ilivyoainishwa katika Hati za Makubaliano na hawabadilishi vipaumbele wakati wa utekelezaji wa bajeti.

ii) **LINAIELEKEZA** APRM kuzingatia nidhamu ya bajeti kwa kutumia, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Fedha za AU, fedha zilizotengwa kwa ajili yake katika kipindi husika.

iii) **LINAIELEKEZA** APRM kuimarisha mpango wake wa utekelezaji kulingana na rasilimali zilizopo.

**f) Bunge la Afrika (PAP)**

i) **LINAIOMBA** Kamisheni kufanya kazi na PAP na kuwasilisha kwa Kamati Ndogo husika ya PRC pendekezo la kurejesha bajeti 13 muhimu kwa ajili ya utendaji kazi wa PAP ambazo ziliondolewa tangu mwaka 2019.

ii) **LINATOA WITO** kwa Kamisheni kuiidhinisha PAP kujaza nafasi 25 muhimu zilizo wazi kutokana na kustaafu kwa wafanyakazi waandamizi, ili kuleta utulivu katika shughuli za Shirika. Katika suala hili, Kamisheni itaunda kwa pamoja na PAP mpango wa uajiri ili kujaza nafasi 25 zilizo wazi za muundo wa PAP ulioidhinishwa kwa miaka ya 2026, 2027, na 2028.

iii) **LINAIOMBA** Kamisheni kusaidia Bunge la Afrika (PAP) katika kutekeleza majukumu yanayohusiana na ujumuishaji wa Mpango Kazi wa Mwaka wa PAP, utayarishaji wa ripoti za utendaji za robo mwaka, matumizi bora ya mifumo ya SAP na AMERT, uboreshaji wa shughuli za kuripoti, na uimarishaji endelevu wa majukumu ya Idara ya Fedha ya PAP.

iv) **LINAIHIMIZA** Kamisheni na Kamati Ndogo husika za Jamhuri ya Watu wa China (PRC) kuratibu bajeti ya Bunge la Afrika (PAP) ili Baraza lipewe bajeti yake kamili kama ilivyokuwa kabla ya 2019.

**g) Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika Dhidi ya Rushwa (AUABC)**

i) Kwa kutambua bajeti ndogo ya AUABC, Kamisheni ya Umoja wa Afrika inapaswa kuwasilisha kwa Kamati Ndogo husika za PRC pendekezo la kuongeza kikomo cha bajeti ya AUABC ili kuiwezesha kufanya ziara na mipango mingine ya kupinga ufisadi, pamoja na programu za kujenga uwezo katika Nchi Wanachama.

ii) Kuajiri nafasi zilizo wazi za AUABC zilizobaki chini ya muundo ulioidhinishwa wa Maputo kunapaswa kuharakishwa na AUC na kuzingatia nafasi saba zilizopunguzwa chini ya muundo wa sasa, na mapitio ya muundo wa AUABC, ambao unazingatiwa, yanapaswa kufuatiliwa kwa ajili ya kuzingatiwa na kuidhinishwa na Kamati

Ndogo husika ya PRC.

iii) AUC inapaswa kupitia uainishaji wa mikutano na ziara za kisheria za AUABC na kuziainisha kwa usahihi, kuhakikisha kwamba zile zilizo chini ya programu hazionyeshwi kama zinazofanya kazi.

iv) AUABC inapaswa kuwa na ushirikiano wa karibu zaidi na RECs na STC ya Nane (STC 8) ili kutumia utaalamu na rasilimali kwa ajili ya kazi ya kupambana na rushwa na ufungamanifu wa sera.

**h) Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD)**

i) AUDA-NEPAD inapaswa kutoa uthibitisho wa kina kwa Kamisheni ifikapo Aprili 2026 wa matukio yaliyosimamishwa ya kuajiri wafanyakazi.

ii) AUDA-NEPAD inapaswa kuimarisha ushirikiano wa kikanda na ujumuishaji wa shughuli katika mipango ya kila mwaka ili kuboresha rasilimali na kuepuka urudifishaji wa juhudi.

**i) Baraza la Kiuchumi, Kijamii, na Kiutamaduni (ECOSOCC)**

iii) Kamisheni ya AU inapaswa kuipa ECOSOCC mfumo wake wa SAP wenye moduli zote chini ya kanuni tofauti ya kampuni ili kuhakikisha uhuru kamili wa uhasibu na utoaji wa taarifa kama Chombo cha AU kinachojitegemea.

iv) Kamisheni inapaswa kubadilisha jina la "kifungu cha bajeti cha PRC" kuwa "kifungu cha bajeti cha Mikutano ya Kisheria" ili kuakisi matumizi yake halisi sambamba na kanuni zingine za bajeti za kisheria.

**j) Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC/Kamisheni)**

i) **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1218 (XLIII) aya ya 41 na **LINASISITIZA** kwamba mkutano maalum wa Mwenyekiti wa AUC na PRC unapaswa kufanyika ili kujadili changamoto za utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi na athari zake kwenye utendaji wa Kamisheni.

ii) **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Des.1218 (XLIII) aya ya 40 na **LINATOA WITO** kwa Kamati Ndogo husika ya PRC kuendesha Kikosi Kazi cha Pamoja na kuanza kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na kutoa ripoti mara kwa mara kwa Kikao cha Pamoja cha Kamati Ndogo za PRC za Masuala ya Ukaguzi, Usimamizi wa Hatari na Uzingatiaji wa sheria; na Usimamizi na Uratibu wa Jumla kuhusu

Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala; na Wataalamu wa Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha (F15).

iii) Kamisheni ya AU inapaswa kuwashirikisha Wabia wa Kimataifa katika kuunganisha michakato ya ukaguzi ili kuwa na kazi ya ukaguzi wa pamoja na kuwa na ripoti za ukaguzi zilizounganishwa ili kuepuka michakato ya kuripoti inayorudiwa na kuwezesha utoaji wa fedha kwa wakati kwa Ofisi husika za AU.

iv) Kamisheni inapaswa kuwasilisha kwa Kamati Ndogo ya Masuala ya Ukaguzi, Usimamizi wa Hatari na Uzingatiaji wa Sheria, orodha kamili ya nafasi zenye madaraja husika, miundo ya mishahara, na ofisi zinazofadhiliwa na Wabia wa Kimataifa kupitia Msaada wa Kiufundi.

v) Kamisheni ya AU kuwasilisha kwa Kamati Ndogo ya Masuala ya Ukaguzi, Usimamizi wa Hatari na Uzingatiaji wa Sheria, mwongozo wenye ratiba zilizo wazi (tarehe za kuanza na tarehe za mwisho), mchakato utakaofanywa katika utekelezaji wa miundombinu mikubwa ya kidijitali ya AU, masuluhisho ya biashara na maboresho ya usalama wa mtandao na pia katika usawazishaji na upatanishi wa majukwaa ya AMERT na SAP.

vi) **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1143(XL) aya ya 18 (i) na **LINAUSIHI** Uongozi wa Kamisheni kujumuisha kipengele cha utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na kufuata utoaji ripoti wa AMERT katika kuwatathmini Wakurugenzi na Wakuu wa idara na ofisi mbalimbali huru, na pia kutoa adhabu kwa Viongozi ambao wanashindwa kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na/au kuwasilisha ripoti kwa kuchelewa katika mfumo wa AMERT.

vii) **LINAIHIMIZA** Kamisheni kuimarisha uzingatiaji wa idara kwa Sheria na Kanuni za Fedha na viwango vya kimataifa vya IPSAS katika utekelezaji wa matumizi, kwa lengo la kuhakikisha kwamba matokeo yanazingatiwa katika kubaini viwango vya utekelezaji wa kiufundi wa shughuli.

viii) **LINAIHIMIZA ZAIDI** Kamisheni, kuweka mifumo ya kuimarisha uratibu wa shughuli miongoni mwa idara, kuboresha utoaji wa ripoti, kuhakikisha matumizi sambamba ya mifumo ya AMERT na SAP, kuhakikisha kuzingatia makataa ya uwasilishaji wa ripoti, na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ili kuboresha usimamizi unaotegemea matokeo.

ix) Kamisheni itawawajibisha Makamishna na Wakurugenzi wa idara kwa ajili ya uratibu wa shughuli za Kamisheni na kusaidia kutumika kwa mfumo wa adhabu iwapo sheria hazitafuatwa.

## B. KUHUSU RIPOTI FUPI YA OIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI WA NUSU MWAKA WA 2025 WA VYOMBO VYA AU (AUC, AFRICA-CDC, ACERWC, ACHPR, AFCFTA, AFCHPR (MAHAKAMA YA AU), AUDANEPAD, APRM, AUABC, ECOSOCC, PAP).

30. **LINAZINGATIA** ripoti na **KUIAGIZA** Kamisheni kuhakikisha kwamba ripoti ya utendaji wa bajeti ya katikati ya mwaka inaboreshwa na inajumuisha taarifa kuhusu fedha zilizotolewa, ikiwa ni pamoja na tarehe ambazo fedha hizo zinapokelewa kutoka kwa washirika, tarehe zilizotengwa na kutolewa SAP kwa matumizi ya kila idara, na tarehe ambazo fedha zilihamishiwa kwa Mashirika, taasisi, na mashirika nje ya Makao Makuu ya AU. Ripoti hizo zinapaswa pia kujumuisha taarifa ya udhibiti wa ndani pamoja na mapendekezo na majibu ya menejimenti, na maoni ya wakaguzi.

31. **ZAIDI LINAELEKEZA** kwamba majadiliano ya ripoti za utendaji wa bajeti ya katikati ya mwaka yanapaswa kujadiliwa kabla ya kuzingatiwa kwa bajeti ya ziada mwezi Agosti ya kila mwaka.

## C. KUHUSU RIPOTI YA OIO KUHUSU FEDHA ZA AKIBA KWA KIPINDI CHA 01 JANUARI HADI 31 JULAI 2025

32. **LINAZINGATIA** ripoti na **KUAGIZA** kwamba takwimu katika ripoti za ukaguzi wa ndani zinapaswa kuambatishwa na michanganuo na maelezo muhimu, pamoja na taarifa kamili kuhusu maamuzi yaliyotajwa katika ripoti ili kufanya maudhui ya ripoti yaeleweke zaidi.

33. **PIA LINAELEKEZA** kwamba bajeti zilizoidhinishwa chini ya fedha za akiba zinapaswa kutekelezwa, na pale ambapo utekelezaji haujakamilika, panapaswa kuwa na ushahidi uliotolewa kwa Nchi Wanachama kwamba fedha hizo zilirudishwa kwenye mfuko wa akiba ipasavyo.

## D. KUHUSU RIPOTI YA OIO JUU YA JEDWALI LA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA NDANI KUFIKIA TAREHE 31 AGOSTI 2025

**34.** **LINAZINGATIA** Ripoti na likikumbuka uamuzi wake EX.CL/Dec.1189 (XLII), aya ya 58 **LINASISITIZA** kwamba kuna haja ya jedwali moja la utekelezaji lililounganishwa linalojumuisha mapendekezo ya ukaguzi wa ndani na nje, ili kutoa mtazamo kamili na wa taasisi mzima wa maendeleo yaliyofanywa na hatari zilizohusika.

35. **LINAAGIZA** kwamba ripoti za siku zijazo zinapaswa kuwa zimeimarisha sehemu ya uchambuzi kwa kubainisha wazi Vyombo vyenye maendeleo makubwa, maendeleo madogo, au visivyo na maendeleo, pamoja na takwimu za jumla kwenye Kamisheni na kwamba uchambuzi huu unapaswa kupelekwa kwa uongozi mkuu wa Kamisheni kwa ajili ya hatua za mara kwa mara.

36. **LINAAGIZA ZAIDI** kwamba mapendekezo ya ukaguzi ambayo hayajashughulikiwa ambayo yanahitaji umakini wa kisheria kuhusu masuala ya sera yanapaswa kuwekwa kwenye karatasi tofauti ili kuwezesha Nchi Wanachama kuyajadili kama inavyofaa.

## IV. RASIMU YA UAMUZI KUHUSU KIKAO CHA PAMOJA CHA KAMATI NDOGO YA MASUALA YA UKAGUZI, UDHIBITI WA HATARI NA UZINGATIAJI, KAMATI NDOGO KUHUSU USIMAMIZI NA URATIBU WA JUMLA WA MASUALA YA BAJETI, FEDHA NA UTAWALA (GSCBFAM); NA WATAALAMU WA KAMATI YA MAWAZIRI KUMI NA WATANO WA FEDHA (F15) - EX.CL/1638(XLVIII)

37. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kikao cha Pamoja cha Kamati Ndogo za PRC kuhusu Masuala ya Ukaguzi, Udhibiti wa Athari na Uzingatiaji; na Uratibu Jumla wa Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala; na Wataalamu wa Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha (F15) na, **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo.

38. **LINAAMUA** kwamba utekelezaji wa maamuzi yenye athari za kifedha, hasa yale yanayohusiana na ajira, kujaza nafasi zilizo wazi ndani ya miundo iliyoidhinishwa, mapitio ya mishahara na marupurupu ya wafanyakazi, au vipengee vyovyote vya matumizi ya ziada, utafanywa hatua kwa hatua na kutegemea upatikanaji wa rasilimali fedha zilizoidhinishwa na za kutosha.

### A. KUHUSU BARUA ZA UONGOZI KUHUSU TAARIFA ZA FEDHA ZA MWAKA 2024 ZA VYOMBO VYA AU ZILIZOKAGULIWA NA BODI YA WAKAGUZI WA NJE WA AU (BOEA)

39. **LINAZINGATIA** ripoti ya Bodi ya Wakaguzi wa Nje na kueleza wasiwasi wake kuhusu matokeo yanayojirudia na **KUVISIHI** Vyombo vyote vya AU kutekeleza mara moja mapendekezo yote yaliyomo katika ripoti za BOEA. Kuhusu masuala ya kawaida yaliyobainishwa miongoni mwa vyombo vyote vya AU, Baraza Kuu **LINAAGIZA** kama ifuatavyo: -

i) **LINAKUMBUSHA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1218 (XLIII) aya ya 64 na **LINASISITIZA** kuharakisha uendeshaji wa mifumo ya usimamizi wa fedha ya AU (SAP & AMERT) kiotomatiki katika vyombo vyote vya AU, ili kuhakikisha

uthabiti, uwazi, wakati na uhalali wa ripoti za fedha. **PIA LINATOA WITO** kwa Kamisheni kuhakikisha mafunzo katika matumizi ya SAP na AMERT ili kuboresha matumizi ya mifumo na kuwezesha kuripoti kwa ufanisi.

ii) **LINAIAGIZA** Kamati Ndogo ya Masuala ya Ukaguzi, Udhibiti wa Athari na Uzingatiaji Sheria pamoja na Kamisheni kutoa ripoti kila baada ya robo mwaka, kufanya kazi moja kwa moja na Vyombo vinavyoonyesha viwango vya chini vya utekelezaji, katika muktadha wa michakato ya ufuatiliaji na tathmini inayofanywa na Kamati ya Uwajibikaji wa Ndani, kujadili changamoto na maendeleo.

iii) **LINAIAGIZA ZAIDI** Kamisheni kuoanisha mzunguko wa bajeti ya ziada na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kabla ya mgao wowote wa bajeti. Aidha, **LINATOA WITO** kwa Kamisheni kufanya kikao cha bajeti ya ziada mwezi Agosti kila mwaka. Kama sehemu ya uoanishaji huu wa bajeti, Kamati Ndogo ya Ukaguzi inapaswa kuwasilisha mapendekezo yake yote kwa Kamati Ndogo ya Usimamizi wa Jumla ili kurahisisha maamuzi ya kikao cha bajeti.

iv) **LINAKUMBUSHA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1126(XXXIX) kifungu cha 41 (ii) na **LINASISITIZA** kwamba, Vyombo vyote vya AU vinapaswa kuzingatia kikamilifu Sheria na Kanuni za Wafanyakazi wa AU na Sheria za Fedha katika usimamizi wa Rasilimali za Umoja na kuhakikisha kwamba vikwazo vinatekelezwa kwa kukiuka Kanuni na Sheria hizi.

v) **LINAELEKEZA** Uongozi wa Kamisheni kuwasilisha ripoti kuhusu ucheleweshaji katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni mpya za Wafanyakazi (SRR) pamoja na athari zozote za kifedha zilizosababishwa kufikia tarehe 31 mwezi Machi, 2026 kwa lengo la kuzingatia hatua zinazofaa kuchukuliwa.

vi) **LINAELEKEZA PIA** kwamba mikataba ya washauri katika Vyombo vyote vya AU vinapaswa kuboreshwa kwa vifungu vinavyowafunga washauri kuandaa ripoti za makabidhiano baada ya kukamilika kwa kila mradi.

vii) **PIA LINAELEKEZA** Vyombo vyote vya AU kuhakikisha kwamba kubeba pesa taslimu kunaepukwa kila wakati ili kupunguza hatari ya hasara kwa Shirika hilo na kuboresha usimamizi mzuri wa fedha.

viii) **LINAELEKEZA ZAIDI** Vyombo kimojakimoja kuhusu masuala maalum kama ifuatavyo: -

**a) Kamisheni ya Umoja wa Afrika**

i) **LINAKUMBUKA** Uamuzi EX.CL/Dec.1168(XLI) aya ya 53 na **KUREJEA** haja ya ufuatiliaji wa kina na kujitolea kwa pamoja kwa ajili

ya uwajibikaji na **LINAUSIHI** Uongozi mpya wa Kamisheni kuingiza utamaduni mpya wa uwajibikaji katika usimamizi wa fedha, huku wafanyakazi wote wakifuata kwa makini Sheria za Fedha za Umoja wa Afrika, viwango vya IPSAS, na taratibu zingine zilizowekwa.

ii) **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1218 (XLIII) aya ya 40 na **LINATOA WITO** kwa Kamati Ndogo ya PRC husika kuendesha Kikosi Kazi cha Pamoja na kuanza kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na kutoa ripoti mara kwa mara kwa Kikao cha Pamoja cha Kamati Ndogo za PRC kuhusu Masuala ya Ukaguzi, Usimamizi wa Hatari na Uzingatiaji; na Usimamizi na Uratibu Mkuu kuhusu Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala; na Wataalamu wa Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha (F15).

iii) **LINAAGIZA** kwamba Mwenyekiti wa Bodi ya Wakaguzi wa Nje akutane na Naibu Mwenyekiti wa Kamisheni kujadili changamoto katika kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na kuimarisha ushirikiano na uongozi mpya. **LINAAGIZA ZAIDI** kwamba Naibu Mwenyekiti wa Kamisheni akutane na Kamati Ndogo husika za PRC kuhusu changamoto zinazohusiana na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kulingana na Uamuzi wa Baraza Kuu EX.CL/ Dec.1218 (XLIII) kifungu cha 41 ikijumuisha zile zinazohusiana na utekelezaji wa MBRS.

iv) **LINAIELEKEZA PIA** AUC kuboresha matumizi ya dashibodi ya ufuatiliaji ambayo tayari imeundwa ili kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kimfumo na kuruhusu usimamizi wa wakati halisi katika suala hili na Nchi Wanachama.

v) **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1143(XL) aya ya 18 na **KUSISITIZA** kwamba mgao wa fedha wakati wa vikao vya bajeti unapaswa kuhusishwa na viwango vya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na idara na Ofisi za Kamisheni na vyombo vingine vya AU.

vi) **LINATOA WITO** kwa Kamisheni kuharakisha mapitio ya Sera kamili ya Mali, Mitambo na Vifaa na mifumo inayohusiana ili kuhakikisha usimamizi wa uwazi na ufanisi wa mali na rasilimali za Umoja wa Afrika, unaojumuisha mali zisizohamishika na zinazohamishika.

vii) **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1168(XLI) aya ya 19 na **KUTOA WITO** kwa Kamisheni kuharakisha kusainiwa kwa Sera ya Uwekezaji na Hazina.

viii) **LINATOA WITO PIA** kwa Kamisheni ya AU kuharakisha kukamilishwa na kuidhinishwa kwa Mpango Mkakati wa Umoja Wote wa Afrika.

**b) Africa CDC**

**40. LINAELEKEZA** kama ifuatavyo:

i) uongozi wa Kamisheni kwa kushirikiana na Africa CDC na Wabia huandaa MOU, pamoja na kifungu cha uwajibikaji, kuhusu matumizi ya fedha za wabia zilizotolewa kwa Africa CDC kulingana na uamuzi wake EX.CL/Dec.1265(XLV) aya ya 55.

ii) kwamba Kamisheni na Africa CDC ziweke mifumo ya kuhakikisha ufuatiliaji sahihi wa fedha za nje ya muhuri na kuhakikisha kwamba wakaguzi wa AU wanapata matumizi ya nje ya muhuri na CDC ya Afrika, na mashauriano yafanyike kuhusu mipango mipya ya kurekebisha Mikataba ya Ushirikiano kuhusu suala hili.

iii) Africa CDC kuwasilisha kwa Kamati Ndogo husika za PRC, sharti kamili la utekelezaji mzuri wa awamu ya II(b) ya mpango wake wa kuajiri, ikiwa ni pamoja na athari zinazohusiana na bajeti, ili kuwezesha utendakazi mzuri wa Chombo hicho.

iv) Africa CDC kuhakikisha kwamba fedha zote zilizotolewa kwa mashirika chini ya Nchi Wanachama zinarejeshwa kikamilifu.

v) Africa CDC kufungamanisha usimamizi wa safari na Sheria za AU na Sera ya Safari kuhusu mahitaji ya kuweka nafasi ya tiketi ya siku kumi (10) na kikomo cha siku 21 kwa robo na pale ambapo kuna dharura inayohitaji safari za haraka, uhalali unaofaa unapaswa kujumuishwa katika idhini.

vi) menejimenti ya Africa CDC kuzingatia Sheria za Fedha za AU katika usimamizi wa rasilimali za AU kwani ni mojawapo ya Vyombo vya AU vinavyofungwa na Sheria za Umoja huo.

vii) Africa CDC na Kamisheni kufanyia kazi MOU kuhusu eneo linalotumiwa na CDC ya Afrika kama ilivyopendekezwa na BOEA.

**c) Kamati ya Wataalamu ya Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto (ACERWC**

i) **LINAIAGIZA** Kamisheni ya AU kuharakisha kutenga ACERWC kama chombo tofauti cha AU chini ya SAP kwa ajili ya uwajibikaji na utoaji wa ripoti huru.

ii) **LINAIAGIZA** AUC kuwa na mikutano ya ufuatiliaji wa moja kwa moja kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na ACERWC na vyombo vingine vya AU vyenye viwango vya chini vya utekelezaji.

**d) Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR)**

**41.** **LINAAGIZA** kama ifuatavyo:

i) kufanya kazi na Kamati Ndogo ya Utawala wa Kiraia kuhusu Mageuzi ya Miundo ili kuharakisha mapitio ya muundo uliopendekezwa ili kuweka muundo unaofaa kusaidia majukumu ya Chombo hicho.

ii) kuhakikisha mgawanyo sahihi wa majukumu katika kuanzisha, kuidhinisha na kufanya miamala ya benki katika mfumo wa kielektroniki wa benki, pamoja na malipo na upatanisho wa benki.

iii) kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa mali ikiwa ni pamoja na rejista ya mali zisizohamishika na pia kuhakikisha kwamba uchakavu wote wa thamani unarekodiwa katika vitabu vya hesabu.

iv) kupatanisha tofauti kati ya salio la akaunti zinazolipwa katika SAP GL na salio lililothibitishwa na watoa huduma.

v) **LINATOA WITO** kwa PRC na Kamisheni kuipatia ACHPR rasilimali za kutosha za bajeti kutoka kwenye michango ya Nchi Wanachama kwa ajili ya programu za kupunguza ufadhili kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa sababu Shirika likishughulikia masuala ya haki za binadamu yanayoathiri Nchi Wanachama.

**e) Sekretarieti ya Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika (AfCFTA**

**42.** **LINAELEKEZA** kama ifuatavyo:

i) Kuzingatia mashauriano yanayoendelea kati ya Sekretarieti ya AfCFTA na Serikali ya Ghana kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Nchi Mwenyeji na kuiomba Sekretarieti ya AfCFTA kutoa ripoti ya maendeleo kwa Kamati Ndogo husika ya PRC ya Mikataba ya Nchi Mwenyeji.

ii) Sekretarieti ya AfCFTA kutoa ripoti ya maendeleo inayoonyesha orodha ya kipaumbele ya wafanyakazi watakaoajiriwa katika awamu ya sasa ya ajira, kwa Kamati Ndogo husika ya PRC mnamo Juni 2026.

iii) Sekretarieti ya AfCFTA kuzingatia Sheria za AU katika usimamizi wa fedha na mali za Umoja huo na kuboresha udhibiti wa ndani katika usimamizi wa masurufu kwa kustaafu ndani ya siku 7 zinazohitajika baada ya misheni; kuboresha usimamizi na uhasibu wa mali zisizohamishika na kujumuisha mali zilizotolewa kutoka Serikali Mwenyeji ya Ghana.

iv) Kuhimiza Nchi Wanachama kutoa taarifa kwa wakati ya kuahirisha tiketi zilizokatwa kwa lengo la kuepusha hali ya hela kutorudishwa kwa tiketi zilizonunuliwa.

v) Kuagiza OIO, kufuatia uamuzi wa Malabo, kuwasilisha ripoti ya uchunguzi kuhusu utendaji wa Sekretarieti ya AfCFTA wa marekebisho ya posho kuhusu wafanyakazi walioajiriwa kimataifa kwa ajili ya kujadiliwa baadae na Baraza Kuu.

vi) Sekretarieti ya AfCFTA kuzingatia kikamilifu sheria za fedha na utawala za AU, ikiwa ni pamoja na kupata idhini ya awali kwa matumizi yote nje ya bajeti iliyoidhinishwa.

vii) Sekretarieti ya AfCFTA kuanzisha Kamati ya Ndani ili kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa awali.

viii) Michango ya Nchi Wanachama kwa Programu za AfCFTA inapaswa kuongezwa ili kupunguza utegemezi kupita kiasi kwa washirika wa nje ambao wanaweza kupanua Umiliki wa kifedha wa AfCFTA, na AU.

ix) Sekretarieti ya AfCFTA kuboresha ulinganifu na uhusiano wa kiufundi kati ya mifumo ya SAP na AMERT ili kutatua tofauti za data, na kuendesha mafunzo kwa wafanyakazi na upatanisho wa data mara kwa mara ili kuhakikisha usahihi na uaminifu wa utoaji ripoti za fedha za baadaye.

x) Sekretarieti ya AfCFTA lazima iboreshe upangaji na ufuatiliaji wa usafiri ili kupunguza athari za kifedha za tiketi za ndege zisizotumika na kutekeleza mifumo ya kuhakikisha Nchi Wanachama zinawasiliana kuhusu kutohudhuria kwa wakati unaofaa na kuchunguza hatua za uwajibikaji zisizoonekana.

**f) Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD)**

**43.** **LINAIAGIZA** kama ifuatavyo:

i) kuweka vigezo vilivyo wazi na kupunguza matumizi ya ushauri elekezi na kuwasilisha uchambuzi wa gharama na faida kwa ajili ya washauri walioshirikishwa wa Mpango wa Ujuzi kwa ajili ya Afrika (SIFA) ifikapo tarehe 31 Machi 2026.

ii) kuharakisha masuala ya wafanyakazi na ufadhili kwa Kamati Ndogo husika za PRC kwa ajili ya kupata msaada wa Nchi Wanachama kwa ajili ya mgao wa bajeti ili kujaza nafasi 166 zilizoidhinishwa ifikapo tarehe 31 Julai 2026.

iii) kutoa ripoti ya kina kuhusu kufutwa kwa tiketi za usafiri kwa Kamati Ndogo husika ya PRC. Aidha, **LINASISITIZA** Wakala kuweka hatua za kupunguza kufutwa kwa tiketi.

iv) kuweka hatua za kurekebisha usimamizi wa usafiri, udhibiti wa fedha, na tiketi zisizotumika kulingana na Sera ya Usafiri ya AU. Vilevile, **LINASIHI** AUDA-NEPAD kutoa ripoti ya kina kuhusu tiketi zisizotumika.

v) kuwa wazi katika kutumia washauri elekezi na kuacha kutumia uhaba wa wafanyakazi kama kisingizio lakini kuweka udhibiti imara wa kifedha katika suala hili. Aidha **LINAIELEKEZA** AUDA-NEPAD kuweka mipaka katika mapatano ya ushauri elekezi, na kutoa maelezo kuhusu matumizi, ikiwa ni pamoja na idadi ya washauri elekezi na sekta ifikapo Aprili 2026.

vi) kuzingatia michakato ya manunuzi katika manunuzi ya kompyuta kama inavyohitajika katika Sera ya Ununuzi ya AU.

**g) Sekretarieti ya Mfumo wa Kutathmini Utawala Bora Afrika (APRM)**

**44.** **LINAAGIZA** kama ifuatavyo: -

i) Kamisheni kushirikiana na APRM na kupitia viwango vya mishahara na posho ili kuoanisha mishahara na gharama za maisha na Kanuni na Sheria za Wafanyakazi wa AU Pamoja na maamuzi husika ya Baraza Kuu kuhusu viwango vya mshahara na posho.

ii) **LINAIOMBA** Kamisheni kutoa maoni kuhusu athari za kisheria zinazohusiana na kukomeshwa kwa malipo yasiyoidhinishwa ya posho kwa wafanyakazi wa GSA na GSB ifikapo Juni 2026 na kupendekeza mapendekezo ya jinsi ya kusonga mbele.

iii) APRM kufanya kazi na Kamisheni na kuwasilisha ombi la kufuta uwajibikaji wa muda mrefu wa Nigeria kwa Kamati Ndogo husika ya PRC baada ya mchakato unaostahili.

iv) APRM kuimarisha kazi yake ya Ukaguzi wa Ndani, na kutekeleza udhibiti wa ndani katika usimamizi wa fedha ikiwa ni pamoja na mgawanyo wa majukumu kwa kuajiri wafanyakazi wa ziada wa uhasibu ili kukidhi viwango vya kimataifa.

v) Kamati Ndogo husika ya PRC kutenga rasilimali muhimu za kifedha kwa ajili ya APRM kujaza nafasi zote 114 zilizoidhinishwa katika mpango wa kuajiri wa awamu ambao unazingatia vikwazo vya bajeti ya kubana

matumizi kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa Chombo hicho.

vi) APRM kuimarisha Ukaguzi wa Ndani wa Idara yake, kutekeleza mgawanyo wa majukumu, na kuajiri wafanyakazi wa ziada wa uhasibu wanaohitajika ili kukidhi viwango vya kimataifa.

**h) Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika Dhidi ya Rushwa (AUABC)**

**45.** **LINAELEKEZA** kama ifuatavyo:

i) Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUABC) na uongozi wa AUABC kuratibu na kufuatilia kwa karibu na ofisi husika katika Serikali ya Tanzania ili kushughulikia masuala yanayosubiriwa kuhusu Mkataba wa Nchi Mwenyeji, na pia kuwasilisha masuala yoyote ambayo hayajatatuliwa kuhusu Mkataba wa Nchi Mwenyeji kwa Kamati Ndogo husika kwa ajili ya kujadiliwa.

ii) Kamisheni na uongozi wa AUABC kufuatilia na kuratibu kwa karibu mikataba ya wafanyakazi.

iii) Kamisheni na AUABC kuwasilisha ombi la ufadhili wa ziada kwa Kamati Ndogo husika kwa ajili ya utendaji kazi mzuri wa Shirika hilo na masuala yoyote ambayo hayajatatuliwa kuhusu Mkataba wa Uhifadhi kwa Kamati Ndogo husika kwa ajili ya kujadiliwa.

iv) AUABC kuhakikisha inafuata sera za utawala, kanuni za fedha, na miongozo ya uendeshaji, na kuendelea na mashauriano ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa misheni na shughuli za Bodi.

v) Kamisheni kwa kushirikiana na AUABC kuharakisha utekelezaji wa uamuzi Ex.Cl /Dec.1287 (XLVI) wa Februari 2025 kuhusiana na makazi ya Mwenyekiti wa AUABC katika kiti cha Bodi jijini Arusha na **LINASISITIZA** kwamba Katibu Mtendaji anawajibika kwa usimamizi wa kila siku wa masuala ya utawala na fedha chini ya mamlaka na wajibu wa moja kwa moja wa Ofisi ya AUABC kama mamlaka kuu zinazohusika na jukumu la Chombo hicho kuhakikisha usimamizi bora na uwajibikaji wa kitaasisi hadi utekelezaji kamili wa uamuzi Ex.CL /Dec.1287 (XLVI).

vi) Kamisheni, kwa kushirikiana na AUABC na Kamati Ndogo husika za PRC, kufanya mapitio ya muundo ulioidhinishwa wa AUABC, ifikapo Juni 2026, ili kuwezesha Chombo hicho, ambacho kwa sasa kina nafasi saba (7) zilizojazwa, kujaza nafasi zote arobaini na mbili (42) zilizoidhinishwa, na hivyo kuimarisha utekelezaji wa shughuli zote za Bodi hiyo.

vii) Kamisheni, kwa kushirikiana na Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika Dhidi ya Rushwa (AUABC) na Kamati Ndogo husika za PRC kwamba mwezi

Aprili 2026, kufanyike mapitio ya Kanuni za Utaratibu za AUABC ili zipitishwe na Baraza Kuu mnamo Juni 2026, ili kushughulikia na kutatua uwili wa kitaasisi katika uongozi wa Chombo hicho, ambao unadhoofisha na kuvuruga utendaji kazi mzuri wa AUABC. Kwa maana hii, marekebisho ya Kanuni za Utaratibu za AUABC yatafafanua majukumu na wajibu wa Katibu Mtendaji, ambaye atatekeleza majukumu yake chini ya uongozi wa Ofisi ya Bodi, mamlaka ya kisiasa na kiutawala inayohusika na Chombo hicho.

**i) Baraza la Kiuchumi, Kijamii, na Kiutamaduni (ECOSOCC)**

i) **LINAIPONGEZA** Serikali ya Zambia kwa kuipa ardhi ECOSOCC na **LINAAGIZA** kama ifuatavyo:

ii) Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU) kufanya kazi kwa karibu na uongozi wa ECOSOCC ili kupata hati miliki ya awali ya ardhi na kuharakisha kupata ardhi hiyo ili kuzuia matumizi yoyote haramu ya ardhi hiyo.

iii) Vyombo vyote vya AU, kuhakikisha kwamba washauri wanatoa ripoti za makabidhiano baada ya kukamilika kwa kila mradi.

iv) ECOSOCC kuacha kutumia mikataba ya ushauri elekezi kufanya huduma zisizo za ushauri ili kufidia uhaba wa wafanyakazi unaohitajika kufanya kazi za kawaida, na kuhakikisha kwamba huduma za ushauri zinatumika tu kwenye kazi za kiufundi ambazo hazina ujuzi maalum kwenye programu zinazotolewa kwa muda maalum kulingana na Sera ya Manunuzi ya AU.

v) ECOSOCC kuzingatia vipengele vya matumizi ya bajeti vilivyoidhinishwa na kuacha kutumia fedha nje ya bajeti iliyoidhinishwa.

vi) ECOSOCC kuepuka makosa katika viwango vya ubadilishaji fedha katika Mfumo wa SAP, na kuweka utaratibu mzuri wa Uthibitishaji wa Ana kwa Ana na Kutoa ripoti ya mali.

**j) Bunge la Afrika (PAP)**

i) **LINAUELEKEZA** Uongozi wa PAP kutekeleza mapendekezo ya ripoti hiyo na kuendelea kufuata Kanuni za fedha za AU.

ii) **LINAIELEKEZA PIA** Kamisheni kutoa usaidizi wa kiufundi na kuijengea uwezo PAP ili kuiwezesha kuboresha mifumo yake ya usajili, uwezo wa usimamizi wa hati na kuimarisha udhibiti wa ndani.

iii) **LINAELEKEZA ZAIDI** kwamba:

a) PAP lazima ihakikishe inawasilisha taarifa zake za fedha kwa wakati ifikapo tarehe 31 Machi kila mwaka.
b) Mahudhurio ya Wabunge na wafanyakazi lazima yafuatiliwe.
c) Mahudhurio ya wafanyakazi yanapaswa kutekelezwa kupitia mfumo wa biometriki na PAP inapaswa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanafanya kazi ndani ya kituo cha kazi kulingana na SRR za AU.
d) PAP inapaswa kukamilisha kuondosha magari yaliyoharibika na kusitisha malipo ya bima yasiyo ya lazima.
e) Madai ya marejesho ya VAT ambayo hayajalipwa kuanzia 2020 na kuendelea yanapaswa kuwasilishwa bila kuchelewa zaidi.
f) Michakato ya kuajiri lazima izingatie viwango vya ushindani, huku rekodi kamili za wafanyakazi zikitunzwa.
g) PAP inapaswa kuhakikisha kwamba usimamizi wa fedha za matumizi madogo madogo unazingatia Sheria za Fedha za AU, haipaswi kulipia bima magari ambayo hayatembei, na magari yanayohitaji kuondoshwa yanapaswa kuwasilishwa kwa Bodi ya Utafiti ya AU.

## B. KUHUSU RIPOTI YA BOEA YA UKAGUZI WA KINA WA AJIRA ZOTE ZILIZOFANYIKA TANGU KUZINDULIWA KWA MFUMO WA AJIRA UNAOZINGATIA SIFA (MBRS)

46. **LINAZINGATIA** ripoti hiyo na **KUELEZEA WASIWASI** wake kuhusu matokeo mazito yaliyopo hasa kuhusu ajira na kuibua wasiwasi kuhusu masuala muhimu yaliyotolewa kuhusu ajira ya Maafisa Wakuu wa Kamisheni, ambayo yanahitaji hatua za marekebisho ikiwa ni pamoja na nafasi ambazo kuajiri kwake hakukuzingatia vipengele muhimu vya kanuni na sheria za wafanyakazi zitekelezwe haraka. **LINAISIHI** AUC kutekeleza mapendekezo yote yaliyomo katika ripoti za BOEA na kuripoti kwa Baraza Kuu mnamo Juni 2026 kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yote yaliyotolewa kwenye ripoti hiyo.

47. **LINAIOMBA ZAIDI** Kamisheni kutoa ripoti mara kwa mara kwa PRC kuhusu changamoto katika utekelezaji wa MBRS haraka iwezekanavyo

48. **LINAKUMBUKA** Uamuzi wake EX.CL/Dec. 1218 (XLIII) aya ya 38 na 39 na **LINAELEZEA WASIWASI** kuhusu kuchelewa kujadiliwa kwa ripoti hiyo na Nchi Wanachama, na **LINASISITIZA** kwamba ripoti hizo zinapaswa kuzingatiwa kwa wakati ili kuziba mapengo yaliyobainishwa na kuboresha udhibiti wa ndani.

49. **LINAIOMBA** BOEA kufanya ukaguzi wa kina wa ziada wa MBRS yenyewe, kufikia 30 Juni 2026, ikiangalia jukwaa zima la kuajiri ili kuhakikisha udhibiti na michakato ya jukwaa hilo linatosha na linafanya kazi kwa ufanisi. Ukaguzi huu wa ziada unapaswa kuzingatia kukagua MBRS yenyewe kwa lengo la kurekebisha muundo wa jukwaa la kuajiri na kuliunganisha na kadi ya alama ya kidijitali ili kuhakikisha ulinganifu na mbinu bora na malengo ya taasisi hiyo. Wigo wa ukaguzi huu unapaswa kujumuisha, pamoja na mambo mengine: -

a) Mapitio ya muundo wa sasa wa mfumo na mtiririko wa kazi
b) Tathmini ya ujumuishaji na kadi ya alama ya kidijitali
c) Tathmini ya vidhibiti na ruhusa za ufikiaji wa mtumiaji
d) Upimaji wa uwezo wa kuripoti na kufuatilia wa jukwaa hilo

**50.** **LINAIOMBA** BOEA kufanya ukaguzi wa kila mwaka kuhusu ajira ndani ya mfumo wa MBRS wakati wa ukaguzi wa kila mwaka wa AU.

**51.** **LINAELEKEZA ZAIDI** Uongozi wa Kamisheni kama ifuatavyo: -

i. kuimarisha mifumo yake ya udhibiti wa ndani kwa kuchukua hatua kali na za kimfumo za ufuatiliaji ili kuhakikisha matumizi ya sheria na taratibu zilizowekwa ni ya wazi, thabiti, na yanayozingatia sheria.

ii. kufanya tathmini ya utendaji wa mameneja wote waliotajwa katika ripoti ili kutathmini utendaji wao kwa kuzingatia maelezo ya kazi na shabaha zilizowekwa katika tathmini ya utendaji.

iii. kuhakikisha kwamba MBRS inatumika kulingana na SRR mpya kwa uwazi bila kuingilia kati na kuondoa kabisa uingiliaji kati wowote katika ngazi na hatua zote.

iv. kuhakikisha kwamba TORs mpya zinatengenezwa chini ya SRR mpya na zinapaswa kuwasilishwa kwa Kikao cha Pamoja kwa ajili ya mapitio kabla ya kuidhinishwa na Mwenyekiti wa Kamisheni kama Afisa Uhasibu wa AU kabla ya Aprili 2026.

**52.** **LINAELEKEZA PIA** Kamisheni kuhakikisha:

i. kwamba wagombea 3 bora wa mwisho waliowasilishwa kwa Mwenyekiti wanazingatia sifa za mchakato mzima kuanzia orodha fupi na vipengele vingine vyote vinavyohitajika ikiwa ni pamoja na mgawo, uwakilishi mdogo, vijana, jinsia vinatimizwa wakati wa mchakato mzima wa kuajiri na sio katika hatua ya mwisho ya mchakato wa kuajiri. Orodha hiyo inapaswa pia kuwa na taarifa kamili kuhusu jinsi orodha ya mwisho inavyowasilishwa kwa Mwenyekiti kwa ajili ya mwongozo unaofaa.

ii. wagombea wote kwenye orodha fupi ya mwisho wanastahili kuteuliwa kwa usawa na uwazi zaidi.

iii. fursa sawa kwa wanawake na kukuza utofauti katika mchakato wa kuajiri na hatua zifuatazo zinapaswa kuwekwa: -

a) Kueleza waziwazi dhamira ya AU kwa usawa wa kijinsia na utofauti katika nafasi zote za kazi na mawasiliano kama inavyofanywa na

Umoja wa Mataifa.

b) Kuhakikisha majopo yote ya tathmini yanapata mafunzo kuhusu upendeleo usiodhamiriwa na mbinu za kuajiri zinazozingatia jinsia.

c) Kutekeleza mchakato wa kuajiri bila kujua, ukiondoa taarifa zinazoweza kutambulika kutoka kwa programu ili kupunguza upendeleo usiodhamiriwa.

d) Kufuatilia na kudhibiti taarifa binafsi za wombaji katika mchakato mzima wa kuajiri.

e) Kujumuisha uwakilishi mbalimbali kwenye paneli za tathmini, hasa kwa nafasi zenye idadi kubwa ya waombaji wanawake.

f) Kuhakikisha matumizi thabiti ya bonasi ya pointi 5 kwa waombaji wanawake na vijana, kulingana na ToR.

g) Kutoa ripoti ya mara kwa mara kuhusu vipimo na matokeo ya utofauti kwa PRC na Baraza Kuu.

iv. kwamba vikwazo dhidi ya maafisa wa kiufundi waliokiuka sheria na kanuni za maadili vinatumika ili kurekebisha matokeo ya udanganyifu wa kimakusudi wa kuajiri tangu kuanzishwa kwa mfumo wa kuajiri unaozingatia sifa katika visa ambapo wafanyakazi wa kiufundi wanaowajibika wanatambuliwa.

## C. KUHUSU RIPOTI YA BOEA KUHUSU RIPOTI YA UKAGUZI NA UCHUNGUZI KUHUSU UTAWALA, USIMAMIZI, FEDHA, NA UENDESHAJI WA BUNGE LA UMOJA WA AFRIKA (PAP)

**53.** **LINAZINGATIA** ripoti na **KUELEZEA WASIWASI** kuhusu Utawala, Usimamizi wa Fedha na Rasilimali Watu, na masuala ya Utendaji na Ununuzi yaliyotolewa na Bodi ya Wakaguzi wa Nje na **KUISIHI** PAP kutekeleza mapendekezo yote yaliyomo katika ripoti za BOEA.

**54.** **LINAUELEKEZA** Uongozi na Utawala wa PAP kama ifuatavyo: -

i) Kufungamanisha Sheria na Taratibu zilizorekebishwa na Sheria na Kanuni za AU kuhusu Usimamizi wa Fedha na Rasilimali Watu na zipitishwe Juni 2026.

ii) Kuhakikisha kwamba mfumo wa udhibiti wa ndani unaboreshwa ili kuondoa makosa yaliyobainika katika usimamizi wa fedha, michakato ya kuajiri na uendeshaji wa PAP.

iii) Kuchunguza madai ya muda mrefu yasiyolipwa tangu mwaka 2014 na kuomba idhini andiko hilo kupitia mchakato unaohitajika na Umoja wa Afrika kwa ajili ya andiko hilo.

iv) Kusimamisha malipo maalum yasiyofaa ya posho maalum kulingana na

uamuzi wa awali wa Baraza Kuu.

v) Kuwasilisha matukio yasiyothibitishwa ya ulaghai na ubadhirifu kwa mahakama kama utaratibu wa usimamizi wa matokeo.

vi) Kuhakikisha kwamba michakato isiyo ya kawaida ya kuajiri, uteuzi wa muda mrefu wa kaimu bila idhini inayofaa, upendeleo, kutofuata taratibu zilizowekwa za kupandishwa cheo, likizo isiyoidhinishwa, ukiukwaji wa sheria za mishahara, na usimamizi duni wa rekodi za wafanyakazi zinashughulikiwa kikamilifu.

vii) Kuanzisha mifumo imara ya upangaji, ufuatiliaji na tathmini, kuimarisha upangaji wa ununuzi na kufuata sheria za ununuzi za AU, kuboresha usimamizi wa mali na usafiri, na kurasimisha mbinu za usimamizi wa athari kulingana na viwango na mbinu bora za AU, kulingana na Uamuzi EX.CL/Dec.1126 (XXXIX).

**55.** **LINAKUMBUSHA** uamuzi wake Na. EX.CL/Dec.1242 (XLIV) unaoitaka OLC kuisadia PAP katika kufanya mapitio ya Kanuni zake za Utaratibu na **INAPENDEKEZA** kwamba PRC, kwa kushauriana na wadau husika, ikamilishe Kanuni za Utaratibu zilizorekebishwa za PAP na kuripoti kwenye Kikao cha Kawaida cha arobaini na tisa cha Baraza Kuu mwezi Juni 2026.

**56.** Katika kutekeleza hayo, **LINAIAGIZA** zaidi Kamisheni, kwa kushirikiana na Bunge la Afrika (PAP) na Kamati Ndogo husika za PRC, mwezi Aprili 2026, kufanya ufungamanifu, mnamo Aprili 2026, kwa ajili ya kupitishwa na Baraza Kuu, wa vyombo hati zote zinazosimamia utendaji kazi wa kiutawala na kifedha wa Chombo hicho, hasa Kanuni za Utaratibu za PAP na maamuzi ya hivi karibuni ya Baraza Kuu kuhusu PAP, pamoja na masharti ya Ibara ya 12.5 ya Itifaki inayounda PAP, ambayo inasema kwamba chombo kikuu cha utawala cha PAP ni Ofisi ya PAP, ambayo chini ya mamlaka yake wafanyakazi wote wa PAP hufanya kazi zao.

**57.** **LINAIOMBA** Kamisheni kwa kushauriana na PRC, kuoanisha mamlaka, kazi na majukumu ya Wakuu wa mifumo ya utawala na usimamizi ikiwa ni pamoja na ile ya Bodi za AU, Marais na Makamu wa Rais wa vyombo vya AU na yale ya Wakuu wa utawala na usimamizi wa vyombo na vyombo vyote vya AU. **LINAIOMBA ZAIDI** Sekretarieti, kwa kushauriana na PRC, kuhakikisha kwamba kuoana huku kunatoa uwazi wa mamlaka na majukumu, ufafanuzi wa mamlaka na uwajibikaji, kuepuka miundo ya usimamizi inayofanana na kuendeleza ukamilishaji na ufanisi.

**58.** **LINAELEZEA WASIWASI** kuhusu ukiukwaji unaojirudia wa mahitaji ya akidi na mahudhurio, udhaifu katika zamu ya uongozi wa kikanda wa PAP na uwakilishi wa kikanda, na kutotekelezwa kwa utaratibu au kuchelewa kwa utekelezaji wa maazimio ya vikao na kuhimiza Ofisi ya PAP kuhakikisha kwamba udhaifu huu unashughulikiwa ipasavyo.

59. **LINAELEZA ZAIDI WASIWASI** kuhusu ukosefu wa wafanyakazi na **KUAMUA** kwamba PAP ifanye kazi na Kamisheni ili kuweka kipaumbele katika kuajiri nafasi muhimu ikiwemo Naibu Karani (Fedha, Utawala na Rasilimali Watu), Mkuu wa Fedha na Bajeti, Mkuu wa Rasilimali Watu na Utawala, Afisa Mwandamizi wa Ufuatiliaji na Tathmini, Mkaguzi Mwandamizi wa Ndani, Mkuu wa Kamati, Mkuu wa Kikao, Afisa Mwandamizi wa Itifaki, Afisa Mwandamizi wa Mahusiano ya Kimataifa, Afisa Rasilimali Watu, Mkalimani - Mfaransa na Mpambe (Sergeant-at-Arms).

60. **LINAKUMBUKA** uamuzi Ex.CL/Dec.1104(XXXIV) aya ya 29 ya Februari 2019 na **LINAISIHI** Kamisheni kuandaa mpango wa utekelezaji wa kurejesha fedha zilizopotea kwa kipindi cha 2012-2023, na matokeo ya mchakato huu yanapaswa kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Kawaida wa 49 wa Baraza Kuu mwezi Juni 2026.

61. **LINAZINGATIA** utata uliopo wa kisheria kati ya Ibara ya 12(5) cha Itifaki inayoanzisha PAP, Sheria na Kanuni za Fedha zilizorekebishwa, na uamuzi EX.CL/Dec.1031 (XXXIV) wa Februari 2019.

62. **LINAAMUA** kupitia uamuzi huo ili kuhakikisha unaendana kikamilifu na Itifaki ya PAP na **KUIELEKEZA** Kamisheni kuanzisha marekebisho ya Kanuni za Fedha zilizorekebishwa, kwa mujibu wa Kanuni yake ya 109, ili kuendana na Kifungu cha 12(5) cha Itifaki ya PAP inayomteua Rais na Makamu wa Rais kama mamlaka kuu zinazohusika na mamlaka ya PAP.

63. **LINASISITIZA** kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 12.5 ya Itifaki ya PAP, Katibu Mkuu anawajibika katika usimamizi wa kila siku wa masuala ya utawala na fedha chini ya mamlaka na wajibu wa moja kwa moja wa Ofisi ya PAP ili kuhakikisha usimamizi thabiti na uwajibikaji wa kitaasisi.

64. **LINAPENDEKEZA** kwamba Wakuu wote wa Vyombo, hasa Rais na Makamu wa Rais, wawe na makao kudumu kwenye makao makuu kwa muda wote wa majukumu yao ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa kila siku na **KUIAGIZA** Kamisheni kuandaa ripoti kamili inayoelezea athari za kifedha, kisheria, na kimuundo za sharti hili la ukaazi wa kudumu na **LINAAGIZA** kwamba ripoti hii iwasilishwe kwa Kamati Ndogo husika za Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) kwa ajili ya mapitio ya kiufundi, huku uamuzi wa mwisho ukichukuliwa kupitia mchakato uliowekwa wa AU.

65. **LINAELEZEA WASIWASI** kuhusu salio la mfuko wa washirika wa mwaka 2014 lililoandikwa katika vitabu vya uhasibu vya PAP ambavyo havina nyaraka zinazohalalisha na **KUAGIZA** uchunguzi wa haraka na wa kina ili kubaini matumizi ya fedha hizi na **LINAAMUA** kwamba mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya usimamizi mbaya wa fedha hizi atahitajika kuzirudisha kikamilifu, kwa kufuata Sheria za Fedha na Kanuni na Sheria za Wafanyakazi za Umoja wa Afrika.

## V. RASIMU YA UAMUZI KUHUSU USHIRIKIANO WA KIMATAIFA – Doc. EX.CL/1639(XLVIII)

### A. Kuhusu Ushirikiano wa AU na EU

66. **LINATOA SHUKRANI** kwa rais wa Jamhuri ya Angola, mhe. João Manuel Gonçalves Lourenço na kwa Serikali na watu wa Angola kwa uandaaji mzuri wa Mkutano Mkuu wa 7 wa AU na EU

67. **LINAPENDEKEZA** kwa Mkutano Mkuu K**UIDHINISHA** azimio la Mkutano wa 7 wa AU na EU uliofanyika tarehe 24 na 25 Novemba 2025, huko Luanda, Angola.

68. **LINAIOMBA** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na EU, kuendelea kufanya kazi kwa pamoja katika mpango wa utekelezaji wa Maeneo ya Ushirikiano ya Kisekta, kwa kuzingatia hati iliyowasilishwa na EU, iliyowekwa katika Ajenda 2063, Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) na maamuzi husika ya Mkutano Mkuu, kwa ajili ya kupitishwa na Mkutano wa Maafisa Wakuu wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Ulaya ndani ya miezi sita (6) baada ya Mkutano wa 7 wa AU-EU.

69. **LINAIOMBA ZAIDI** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni, Kikosi cha Kidiplomasia cha Afrika huko Brussels, na EU, kuendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa ahadi zilizotolewa katika Azimio la Mkutano wa 7 wa AU-EU.

### B. Kuhusu Mkutano wa Kimataifa wa Tokyo wa Maendeleo ya Afrika (TICAD)

70. **LINAISHUKURU** na **KUIPONGEZA** Serikali na Watu wa Japani kwa kufanikiwa kwa Mkutano wa TICAD 9 na mikutano yake ya kisheria iliyotangulia.

71. L**INAPENDEKEZA** Mkutano Mkuu **KUIDHINISHA** Azimio la Mkutano Mkuu na **LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika , kwa ushirikiano wa karibu na Japani na Kikosi cha Wanadiplomasia wa Afrika huko Tokyo, kufuatilia utekelezaji wa haraka wa matokeo ya Mkutano Mkuu.

72. **LINAOMBA ZAIDI** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Tume, Kikosi cha Wanadiplomasia wa Afrika huko Tokyo, na Serikali ya Japani, kuanza mchakato wa uteuzi wa nchi mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa TICAD uliopangwa kufanyika Afrika mwaka 2027 na kwa Mkutano wa TICAD 10 kufanyika mwaka 2028.

### C. Kuhusu Ushirikiano wa Afrika na Korea

73. **LINAZINGATIA** ombi lililotolewa na Jamhuri ya Korea la kuahirisha Jukwaa la Mawaziri wa Afrika na Korea hadi 2027.

**74.** **LINAIOMBA** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni, kuendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa katika Jukwaa la Tano (5) la Mawaziri wa Korea na Afrika, lililofanyika tarehe 10 Machi 2022, huko Seoul, Korea, na kuanza mchakato wa kuchagua nchi mwenyeji wa Jukwaa la 6 la Mawaziri wa Afrika-Korea, lililopangwa kufanyika Afrika mwaka 2027.

## D. Kuhusu Ushirikiano wa Afrika na India

**75.** **LINAKARIBISHA** pendekezo la Jamhuri ya India ya kuandaa Mkutano wa Nne (4) wa Afrika na India na **LINAIDHINISHA** pendekezo lililotolewa.

**76.** **LINAIOMBA** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na Kikosi cha Wanadiplomasia wa Afrika huko New Delhi, kukubaliana kuhusu tarehe halisi za Mkutano wa Nne (4) wa Afrika-India na kuendelea na mashauriano yote muhimu kuelekea kukamilisha Nyaraka za Kazi za mkutano huo, ambao utafanyika katika robo ya kwanza au kabla ya mwisho wa robo ya pili ya 2026, nchini India.

**77.** **LINASISITIZA** umuhimu wa kufuata kabisa maamuzi ya AU kuhusu njia za ushiriki na uwakilishi wa Umoja wa Afrika katika mikutano ya ushirikiano wa kisheria, hasa uamuzi Assembly/AU/Dec.762(XXXIII), ambao unasema wazi kwamba AU itawakilishwa katika mikutano ya kisheria ya ushirikiano kati ya Umoja wa Afrika / Bara la Afrika na nchi mshirika kwa muundo maalum, unaojulikana kama "Muundo wa Banjul".

## E. Kuhusu Ushirikiano wa Afrika-Uturuki

**78.** **LINAIOMBA** PRC, ikishirikiana kwa karibu na Kamisheni na Jamhuri ya Libya, kukubaliana na Türkiye kuhusu tarehe za Mkutano wa Nne (4) wa Ushirikiano wa Afrika na Türkiye utakaofanyika Tripoli, Libya, mwaka 2026, na kuanzisha hatua zinazohitajika za maandalizi kwa ajili ya mkutano wake uliofanikiwa, baada ya kuthibitishwa kwa tarehe zilizopendekezwa na nchi mwenyeji.

## F. Kuhusu Kukamilika kwa Sera ya Ushirikiano wa AU na Mfumo wa Kimkakati

**79.** **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1265(XLV) uliopitishwa na Mkutano wa Kawaida wa 45 wa Baraza Kuu uliofanyika Accra, Ghana, Julai 2024, ambao ulitambua kukosekana kwa maelewano kuhusu uainishaji, ushirikishwaji, na utaratibu wa majina wa Sera na Mfumo wa Mkakati wa Ushirikiano wa Umoja wa Afrika (AUPPSF) na kumuomba Mwenyekiti wa Baraza Kuu na Mwenyekiti wa Kamishnei kufanya mashauriano kwa haraka kuhusu masuala yanayohusiana na AUPPSF na kuwasilisha matokeo ya mashauriano hayo kwa Nchi Wanachama kwa wakati ufaao.

**80.** **LINAELEZEA WASIWASI** kuhusu uchelewaji unaoendelea katika kukamilisha AUPPSF.

81. **LINAMUOMBA** Mwenyekiti wa Baraza Kuu, kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Kamisheni, kutoa uongozi wa kisiasa unaohitajika ili kukamilisha mashauriano ya ngazi ya juu mapema iwezekanavyo ili kutatua masuala yaliyosalia ambayo yamezuia ukamilishaji wa AUPPSF.

82. **LINAWAOMBA ZAIDI** Mwenyekiti wa Baraza Kuu na Mwenyekiti wa Kamisheni kutoa ripoti juu ya matokeo ya mashauriano yao kwa Baraza Kuu mnamo Juni 2026.

## G. Kuhusu Kamati ya Uongozi ya AU ya Ushirikiano

83. **LINAKARIBISHA** jukumu muhimu linalofanywa na Kamati ya Uongozi ya Umoja wa Afrika ya Ubia wakati wa michakato ya maandalizi ya mikutano ya ushirikiano ya Umoja wa Afrika na matukio yanayohusiana.

84. **LINAIOMBA** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni, kurasimisha Kamati ya Uongozi ya AU ya Ushirikiano, kabla ya Mkutano wa Kawaida wa 49 wa Baraza Kuu.

## H. Uwezo wa Kitaasisi wa Usimamizi wa Ubia

85. **LINAIAGIZA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuchukua hatua zinazohitajika kutekeleza Maamuzi ya awali, EX.CL/Dec.942(XXX) ya Januari 2017, EX.CL/Dec.1020(XXXIII) ya Juni 2018 na EX.CL/Dec.1310(XLVII) ya Julai 2025, ndani ya muundo, kazi, na uwezo wa PMRMD katika kutimiza mamlaka yake, na kuomba pendekezo la ziada kama inavyohitajika kuwasilishwa kupitia ripoti kamili kwa kamati ndogo husika kwa ajili ya kuzingatiwa na kupelekwa kwa PRC.

**RASIMU YA UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA KAMATI NDOGO YA PRC YA PROGRAMU NA MIKUTANO – EX.CL 1640(XLVIII)**

86. **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1217(XLIII) na uamuzi EX.CL/Dec.1310 (XLVI) kuhusu Mpango Mkakati wa AU, yanayotaka kuandaliwa kwa Mpango Mkakati wa miaka mitano na kuahirisha idhini yake hadi Februari 2026:

87. **LINAZINGATIA** matokeo na mapendekezo ya PRC kuhusu utekelezaji wa mwongozo ili kukamilisha Mpango Mkakati wa AU (2024–2028).

88. **LINAISIFU** Kamisheni mpya na timu za kiufundi kwa Kujitolea kutekeleza mwongozo unaoongoza katika kukamilisha Mpango Mkakati wa AU (2024-2028).

89. **LINAPONGEZA ZAIDI** jitihada za Kamati Ndogo ya PRC ya Programu na Mikutano katika kuimarisha uratibu, kukuza uwiano wa progamu, na kuimarisha ufanisi wa kitaasisi.

90. **LINAZINGATIA** taarifa kuhusu utekelezaji wa mwongozo uliojumuisha kukamilika kwa michakato ya mashauriano, mapitio ya Mpango Mkakati ya Tume mpya, uthibitisho wa kiufundi kupitia ushiriki jumuishi za ngazi ya juu na ufungamanifu na mwitikio kwa mazingira ya nje yanayoathiri utekelezaji.

91. **LINAPITISHA** Mpango Mkakati wa AU (2024–2028).

92. **LINAAGIZA** Kamati Ndogo ya Programu na Mikutano kuendelea kufuatilia upatanishi wa mikakati na bajeti za Umoja wa Afrika na vipaumbele vya Matarajio kama inavyoainishwa katika STYIP ya Ajenda 2063 na vipaumbele vya Mpango Mkakati wa miaka mitano na kufanya kazi zaidi na miundo husika ya AU ili kuhakikisha rasilimali za kutosha za Mpango Mkakati na kupunguza utegemezi mkubwa kwenye ufadhili wa wabia.

93. **LINAAGIZA ZAIDI** Kamisheni kuunda na kurasimisha Mfumo wa Utawala wa Mkakati wa Utekelezaji kwa ajili ya utoaji ripoti, ufuatiliaji, umiliki na uwajibikaji jumuishi wa Mpango wa uongozi mpana wa AU na kuwasilisha maendeleo ya utekelezaji wa mfumo mara kwa mara kwa Baraza Kuu.

**KAMATI NDOGO YA PRC KUHUSU NEPAD – EX.CL/1641(XLVIII)**

94. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Mwaka ya 2025 ya Kamati Ndogo kuhusu NEPAD;

**95.** **PIA LINAZINGATIA** Hadidu za Rejea (TOR) zilizorekebishwa za Kamati Ndogo kuhusu NEPAD kama zilivyopitishwa na PRC kufuatia mabadiliko ya Kamati Ndogo kuhusu NEPAD kuwa Kamati Ndogo ya jumla;

**96.** **LINAIDHINISHA** matokeo ya Mikutano ya Mwaka kati ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu NEPAD na AUDA-NEPAD iliyofanyika tarehe 16 Desemba 2025 ili kuimarisha uratibu na ushirikiano ndani ya vyombo na taasisi za AU kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa sera, programu na miradi ya NEPAD na Ajenda ya 2063;

**97.** **LINAIOMBA** AUDA-NEPAD kutoa kila mwaka, jedwali kamili la miradi/programu zilizopendekezwa, ikijumuisha vigezo na mbinu za kuchagua nchi zinazofaidika, aina ya miradi/programu, mgao wa bajeti unaolingana, na athari ya kila mradi; huku ikihakikisha mgawanyo wa rasilimali na miradi kwa usawa na usawa miongoni mwa Nchi Wanachama na kanda za Umoja wa Afrika;

**98.** **LIINAIOMBA ZAIDI** AUDA-NEPAD kuwasilisha ripoti ya mwaka iliyojumuishwa kuhusu maendeleo ya programu na matokeo yake halisi katika utekelezaji wa Ajenda 2063, ikijumuisha viashirio vya utendaji na mafunzo yaliyopatikana;

**99.** **LINATOA WITO** kwa Sekretarieti ya bara ya AUDA-NEPAD kuboresha ushirikiano na Ofisi za Kitaifa za Nchi Wanachama husika za NEPAD, kwa lengo la kuboresha uratibu, utekelezaji na utoaji wa ripoti kuhusu Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) wa Ajenda 2063, chini ya usimamizi wa Kamisheni.

**100.** **LINAIOMBA** AUDA-NEPAD kuboresha ushirikiano wake na sekta binafsi ya Afrika ili kuongeza mchango wao katika utekelezaji wa Ajenda 2063, na, katika suala hili, linatoa wito wa mashauriano ya mara kwa mara na sekta binafsi ya Afrika kando ya ushirikiano wa Chombo cha Sera cha AU, pale inapobidi.

**101.** **LINAKARIBISHA** mchakato unaoendelea wa kukabidhi mpango wa Uoanishaji wa Udhibiti wa Dawa za Afrika (AMRH) kwa AMA na kuhimiza utekelezaji wake mzuri ili kuhakikisha mwendelezo, uendelevu, na uendeshaji wa mafanikio wa AMA.

**102.** LINASISITIZA TENA umuhimu, kupitia Kitengo cha Uratibu cha AUDA-NEPAD, chini ya usimamizi wa Kamisheni, kuimarisha uratibu miongoni mwa Kamisheni, AUDA-NEPAD, Africa CDC, AfCFTA, AMA na RECs, kupitia mipango, ufuatiliaji na tathmini ya pamoja ili kuhakikisha uwiano, uhusiano na ufanisi, hasa katika ukusanyaji na utumiaji wa rasilimali, kuelekea utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) wa Ajenda 2063;

**103.** **LINAKARIBISHA** maendeleo yaliyopatikana katika kukamilisha rasimu ya upembuzi yakinifu wa Ajenda ya Mfuko wa Maendeleo wa 2063 na **LINAOMBA**

kuharakishwa kwa uwasilishaji wake kwa Kamati Ndogo husika za PRC na Kamati ya Ufuatiliaji ya Mawaziri kuhusu Ajenda 2063 kabla ya kuwasilishwa kwa Baraza Kuu kabla ya kikao chake cha Juni 2026, na **LINAPENDEKEZA ZAIDI** kwamba falsafa ya kifedha ya Mfuko wa Maendeleo inapaswa kutafsiriwa katika ratiba ya kina ya uendeshaji, ikijumuisha hatua za kati zilizofafanuliwa wazi, ili kupunguza hatari ya ucheleweshaji wa kimuundo katika utekelezaji wake;

**104.** **LINAIAGIZA** PRC, kupitia Kamati Ndogo ya NEPAD kuchunguza njia zilizopangwa za ushirikiano na mawasiliano kati ya Kamati Ndogo ya NEPAD na Kamati ya Uendeshaji ya AUDA-NEPAD kwa lengo la kuoanisha mwongozo na msaada wa Nchi Wanachama kwa AUDA-NEPAD katika kutekeleza mamlaka yake.

## VIII. KAMATI NDOGO KUHUSU HAKI ZA BINADAMU, DEMOKRASIA NA UTAWALA (HRDG) – Doc. EX.CL/1643(XLVIII)

**105.** **LINAZINGATIA** ripoti ya Shughuli za Kamati Ndogo ya PRC ya Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala (HRDG) kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2025 na kuwapongeza wajumbe pamoja na sekretarieti kwa ripoti ya kina iliyowasilishwa;

**106.** **LINAKUMBUKA** Uamuzi wake wa awali EX.CL/Dec.1233(XLIV) ambao uliamua kaulimbiu ya mwaka 2025 kuwa "Mwaka wa Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala Barani Afrika" na linapendekeza zaidi kwa uamuzi huu kuendelea hadi miaka ijayo;

**107.** **LINAZINGATIA** umuhimu wa kihistoria wa maadhimisho ya miaka ishirini (2007-2027) ya kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala (ACDEG), ambao hutumika kama kielelezo cha bara cha utawala wa kidemokrasia na uwajibikaji; na ambao ndio chombo kikuu cha kanuni cha Usanifu wa Utawala wa Afrika (AGA) na ushirikiano wake na Usanifu wa Amani na Usalama wa Afrika (APSA); na **LINAZINGATIA ZAIDI** maadhimisho ya miaka kumi na tano ijayo (2012-2027) ya kuanza kutumika kwa Mkataba huu;

**108.** **LINAKUMBUSHA** kwamba Tarajio la 1 (Afrika Yenye Mafanikio Inayotegemea Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu) na Tarajio la 3 (Afrika yenye utawala bora, demokrasia, heshima kwa haki za binadamu, haki, na utawala wa sheria) ya Ajenda 2063 zinategemeana na haziwezi kutenganishwa; **LIKISISITIZA** kwamba taasisi imara za kidemokrasia, uwajibikaji na heshima kwa haki za binadamu na za watu ni masharti muhimu ya awali ya kuvutia uwekezaji endelevu, kukuza biashara ya ndani ya Afrika, kuwezesha taasisi zenye uwezo

na uwazi, na hatimaye, kufikia maono ya pamoja ya bara la Afrika ya ustawi jumuishi;

**109.** **LINAAMUA**, kwa kuzingatia yaliyotangulia hapo juu, kupendekeza kupitishwa na Mkutano kwamba kaulimbiu ya AU kwa mwaka 2027 itakuwa **"**Mwaka wa Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala Barani Afrika"; **LINAIOMBA** Kamisheni ya AU, kwa kushauriana na Nchi Wanachama na Vyombo husika vya AU, kuandaa na kuwasilisha muhtasari wa kina wa dhana na ramani ya utekelezaji wa kaulimbiu hiyo kwa Baraza ili ifikiriwe katika Kikao chake cha Kawaida kijacho;

**110.** **LINAZINGATIA** Muongo wa sasa wa Haki za Binadamu na Watu Barani Afrika 2017-2026 unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2026;

**111.** **LINAZINGATIA PIA** kufanyika kwa Jukwaa la Pili (2) kati ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG kama sehemu ya mazungumzo ya kawaida kati ya Tume ya Banjul na Nchi Wanachama, na **LINATOA WITO** wa kutekeleza hitimisho la mkutano huu;

**112.** **LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama (PAPS) kufanya utafiti wa kina mwaka 2027 kutathmini maendeleo yaliyopatikana chini ya Muongo wa kwanza wa Haki za Binadamu (2017-2026), kwa lengo la kubaini mafanikio, changamoto, na uzoefu uliopatikana, kwa ushirikiano wa karibu na Mashirika husika ya Haki za Binadamu ya Afrika**;**

**113.** **LINAAMUA** kwamba matokeo ya utafiti uliotajwa hapo juu yatasaidia kuangazia uwezekano wa Muongo mpya wa Haki za Binadamu barani Afrika unaojumuisha kipindi cha 2028-2037;

**114.** **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1176(XXVI) aya ya (65) wa kuwasilisha utafiti kuhusu marekebisho yaliyopendekezwa yatakayowasilishwa kwa Kamati Ndogo ya PRC ya HRDG kuhusu kuipa ACERWC ufikiaji wa moja kwa moja wa Mahakama ya Afrika huku kukiwa na mchakato unaostahili;

**115.** **LINAYASIFU** mashirika ya haki za binadamu ya AU kwa maendeleo makubwa yaliyopatikana katika kufanya utafiti wa kina kuhusu hali ya kufuata maamuzi, kama ilivyoagizwa na uamuzi EX.CL/Dec.1245(XLIV), na **LINAZINGATIA** kupitishwa kwake rasmi kama Mradi Mkubwa wa AGA-APSA;

**116.** **LINAZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa AU na vyombo husika vya Utawala wa Afrika na Miundombinu ya Amani na Usalama (AGA-APSA), ikiwa ni pamoja na Kamati Ndogo ya Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala ya PRC, kutoa ushirikiano unaohitajika na uungaji mkono wa kisiasa katika shughuli za

ukusanyaji na uthibitishaji wa data za utafiti ili kuhakikisha kukamilika kwake kwa mafanikio na uadilifu wa utafiti;

**117.** **LINAUSIFU** Ufalme wa Lesotho kwa marekebisho yake ya hivi karibuni ya katiba yanayoimarisha utawala wa kidemokrasia, utawala wa sheria na uwajibikaji wa kitaasisi, na **LINATAMBUA** mageuzi haya kama mchango muhimu kwa ustahimilivu wa kidemokrasia na uzuiaji wa migogoro katika Nchi Mwanachama iliyozingirwa.

**118.** **LINAKUMBUKA** mpango wa Jukwaa la AGA-APSA kuhusu Kuoanisha michakato ya kuripoti ya Nchi Wanachama kuhusu Hati za Maadili ya Pamoja za Kiafrika na kutoa wito wa kukamilika kwa mpango huu.

**119.** **LINAIOMBA** Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Kamati ya Wataalamu ya Afrika, kutengeneza na kutumia Taratibu za Uendeshaji Sawa (SOPs) zilizo wazi kwa ajili ya kutathmini, kuripoti, na kuimarisha utekelezaji wa maamuzi ya haki za binadamu.

**120.** **LINAZINGATIA** maadhimisho yajayo ya miaka ishirini ijayo (2006-2026) ya utekelezaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR); na **LINAIOMBA** Kamisheni ya AU, kwa ushirikiano wa karibu na AfCHPR, kuendeleza na kuhamasisha usaidizi wa hali ya juu wa kisiasa, kifedha, na vifaa kwa ajili ya shughuli za sherehe katika Vyombo vyote husika vya AU na Nchi Wanachama ili kuangazia jukumu muhimu la Mahakama katika kudumisha Mfumo wa Haki za Binadamu wa Afrika;

**121.** **LINASISITIZA** kwamba miaka ishirini ya uendeshaji wa AfCHPR inatoa wakati muhimu wa kuharakisha kuanzishwa kwa Mahakama ya Haki na Haki za Binadamu ya Afrika (ACJHR); **LINASISITIZA** haja muhimu ya Nchi Zilizoridhia Itifaki ya 1998 na Itifaki ya 2003 kuweka kipaumbele katika kuridhia Itifaki ya Sharm El-Sheikh ya 2008 ili kuharakisha muunganiko na kuanza kutumika kwa ACJHR;

**122.** **LINASISITIZA ZAIDI** kwamba kuanzishwa kwa ACJHR ni muhimu kwani majukumu yake maalum ya kimahakama juu ya masuala ya kisheria na kitaasisi ya bara yataimarisha mazingira ya kisheria yanayohitajika kwa utabiri wa soko na shughuli za kibiashara zinazoongezeka mipakani;

**123.** **LINASISITIZA** kwamba miundombinu hii imara na inayotawala ya mahakama ya bara ni sharti la msingi la kulinda mazingira thabiti yanayohitajika ili kutambua kikamilifu uwezo wa Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika (AfCFTA) na kufikia Afrika yenye mafanikio, jumuishi, na amani chini ya Ajenda ya 2063;

**LINAZINGATIA** umuhimu unaoendelea wa Itifaki ya Malabo (2014); na **LINAELEKEZA** kwamba mabadiliko kuelekea ACJHR yafanyike kulingana na mageuzi ya AU na taratibu za bajeti;

**124.** **LINASIHI** kuwepo kwa uratibu ulioboreshwa na ushiriki wa mara kwa mara kati ya Mifumo ya Tahadhari ya Mapema ya Bara (CEWS), Kamati Ndogo ya PRC kuhusu HRDG, RECs na AZAKI katika ubadilishanaji wa taarifa kuhusu afua za kimkakati;

**125.** **LINAPONGEZA** jukumu muhimu la ECOSOCC katika ushiriki wa raia wa Afrika katika masuala ya AU kupitia uundaji wa ripoti za AZAKI kwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kupitia Kamati Ndogo ya HRDG;

**126.** **LINATOA WITO** wa kuwepo uratibu ulioimarishwa kati ya ECOSOCC na Nchi zote Wanachama ili kuharakisha utekelezaji wa Mfumo wa Ithibati wa AZAKI ili kuepuka mchakato sambamba;

**127.** **LINAIOMBA** Kamisheni kufanya mapitio ya Mfumo wa Sera wa Mageuzi ya Sekta ya Usalama (SSR) uliopitishwa mwaka 1993, kulingana na ajenda ya jumla ya mageuzi ya APSA na uzuiaji na usimamizi wa migogoro;

**128.** **LINAIPONGEZA** APRM kwa uzinduzi wa Ripoti ya Utawala wa Afrika ya 2025 kuhusu Utawala wa Maliasili barani Afrika. **LNAIDHINISHA** kaulimbiu na kaulimbiu ndogo zilizopendekezwa kwa Ripoti ya Utawala wa Afrika ya 2027 kuwa " *Vijana na Utawala: Kutoka Ahadi hadi Ustawi";*

**129.** **LINATOA WITO** kwa Nchi zote Wanachama kuendeleza na kutekeleza mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa wafichuzi wa habari inayoongozwa na Mfumo ulioandaliwa na Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika kuhusu Kupambana na Rushwa (AUABC);

**130.** **LINALIOMBA** Bunge la Afrika (PAP) liendelee na juhudi zake za utetezi ili kukuza uidhinishaji wa Hati za Maadili ya Pamoja za AU kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni, na kuhakikisha ufadhili wa kutosha kwa shughuli na mamlaka ya PAP;

**131.** **PIA LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuendelea na utekelezaji wa mipango, programu na shughuli chini ya kaulimbiu ya mwaka ya AU "***Haki kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika kupitia Fidia***, kama sehemu ya juhudi za kuendeleza ajenda ya haki ya fidia;

**132.** **LINASISITIZA** haja ya kutambua "***Siku ya Ukumbusho*** " ambayo itaadhimishwa kila mwaka kama sehemu ya ajenda ya fidia ya AU na **LINAKUMBUKA** uamuzi Assembly/AU/Dec.903(XXXVIII), ambao unaidhinisha pendekezo la Mhe.

Abdelmadjid TEBBOUNE, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria kurasimisha siku ya ukumbusho wa mashahidi wa Afrika na waathirika wa biashara ya utumwa ya kupitia bahari ya Atlantiki, ukoloni na ubaguzi wa rangi.

## IX. KAMATI NDOGO KANUNI, VIWANGO NA SIFA ZA UTAMBULISHO – Doc. EX.CL/1644(XLVIII)

133. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamati Ndogo kuhusu Sheria, Viwango na Sifa na **LINAIPONGEZA** Kamati Ndogo na Kamisheni kwa kazi iliyofanywa;

### A. MAREKEBISHO YALIYOPENDEKEZWA YA SHERIA ZA UTARATIBU WA VYOMBO VYA SERA NA SHERIA YA KAMISHENI KUHUSU UCHAGUZI WA VIONGOZI WA JUU WA KAMISHENI

134. **LINAZINGATIA** marekebisho yaliyopendekezwa ya sheria za utaratibu wa vyombo vya sera na sheria ya Kamisheni kuhusu uchaguzi wa viongozi wa juu wa Kamisheni;

135. **LINAIOMBA** PRC kujadili ripoti hii na kutoa mapendekezo kwa Mkutano wa Kawaida wa 49 wa Baraza Kuu mnamo Juni 2026;

### B. RASIMU YA MFUMO WA KUANZISHA NA KUYAKUBALI MASHIRIKA MAALUM YA UMOJA WA AFRIKA

136. **LINAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana katika uundaji wa Mkataba wa Kuanzisha na Kuyakubali Mashirika Maalumu;

137. **LINAIOMBA** Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Katiba, Viwango na Sifa za Utambulisho kufanya kikao cha pamoja na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Mageuzi ya Miundo ili kukamilisha rasimu ya Mfumo na kuripoti kwa Mkutano wa 49 wa Kawaida wa Baraza Kuu;

### C. UTAFITI KUHUSU UAINISHAJI WA MAAMUZI YA VYOMBO VYA SERA VYA AU

138. **LINAIOMBA** Kamati Ndogo ya Katiba, Viwango na Sifa za Utambulisho kukamilisha kazi ya uainishaji wa maamuzi ya Vyombo vya Sera vya AU, kwa kushirikiana na vyombo na taasisi zingine husika za AU, na kutoa ripoti kwa Mkutano wa 49 wa Kawaida wa Baraza Kuu.

### D. MAPITIO YA KANUNI ZA UTARATIBU ZA BUNGE LA AFRIKA

**139.** **LINAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana katika marekebisho ya Kanuni za Utaratibu za PAP na **LINAAMUA**:

i. **KUSISITIZA** kwamba uchaguzi wa Uongozi wa PAP utafanyika Februari 2026 kama ilivyoelekezwa na Uamuzi EX.CL/Dec.1288(XLVI) na Uongozi mpya utakaochaguliwa utaundwa kama ifuatavyo:

- Rais: Kaskazini
- Makamu wa 1 wa Rais: Mashariki
- Makamu wa 2 wa Rais: Magharibi
- Makamu wa 3 wa Rais: Kati
- Makamu wa 4 wa Rais: Kusini

ii. **KUSISITIZA ZAIDI** kwamba PAP itazingatia maadili na kanuni za Umoja wa Afrika, ikiwa ni pamoja na kanuni ya mzunguko wa kawaida na unaotabirika;

iii. **KUAGIZA** PAP kuheshimu Kanuni zake za Uendeshaji kuhusu muhula wa miaka mitatu ya uongozi ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kanuni ya mzunguko unaozingatia ratiba na unaotabirika;

iv. **KUAGIZA ZAIDI** kwamba kuendelea kujadiliwa kwa Rasimu ya Kanuni za Uendeshaji zilizorekebishwa hakutaathiri kufanyika kwa uchaguzi wa Uongozi wa PAP mwezi Februari 2026;

v. **KUMUOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni kutuma Jopo la Ngazi ya Juu kusimamia uchaguzi wa Uongozi wa PAP Februari 2026 na kutoa ripoti kwenye Mkutano wa 49 wa Kawaida wa Baraza Kuu.

## X. KAMATI NDOGO KUHUSU MASUALA YA MAZINGIRA

**140.** **LINAKUMBUKA** uamuzi wake EX.CL/Dec.987(XXXII) wa Januari 2018, ulioanzisha Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Masuala ya Mazingira.

**141.** **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Masuala ya Mazingira na **LINAISIFU** Kamati Ndogo kwa usimamizi na uratibu inaotoa kuhusu ajenda ya usimamizi wa mazingira na maliasili ya Umoja wa Afrika.

**142.** **LINAZINGATIA** kwamba uthibitisho wa ufadhili wa Mshirika (Umoja wa Ulaya) unaoendelea kwa Programu ya *Intra-ACP Climate Services and Related Applications* (ClimSA) ulikuja baada ya mchakato wa bajeti wa AU kukamilika, na kwamba sambamba na utaratibu uliowekwa, bajeti ya ClimSA ilifutwa kutoka

Bajeti ya Programu ya AUC ya 2026 kwa sababu haikuwa na uthibitisho wa ufadhili.

**143.** **LINATHAMINI** upatikanaji wa fedha za Wabia katika Kamisheni na faida za programu ya ClimSA kwa Nchi Wanachama katika kutoa taarifa za hali ya hewa na tabianchi kwa ajili ya kilimo na upatikanaji wa chakula, upunguzaji wa hatari za majanga, mifumo ya tahadhari ya mapema, nishati, afya, na maji, miongoni mwa mengine.

**144.** **LINATAMBUA** hali za kipekee zilizosababisha bajeti ya ClimSA kutojumuishwa katika bajeti ya programu ya AUC ya 2026, na athari mbaya zinazoweza kutokea kwa Nchi Wanachama pamoja na hatari ya Kamisheni kukiuka majukumu yake ya kimkataba kwa kutowalipa wakandarasi.

**145.** **LINAIDHINISHA KWA UPEKEE** nyongeza ya bajeti inayofikia dola za Marekani 7,500,000.00 ambapo dola za Marekani 4,000,000.00 ni fedha za ufadhili, na dola za Marekani 3,500,000.00 ni bajeti ya programu kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya ClimSA katika Ukanda wa ECCAS na kwa ajili ya shughuli za bara za AUC kwa Nchi Wanachama wa AU.

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI ZA KAMATI MAALUMU ZA KITAALAMU (STCs) NA MIKUTANO MINGINE YA MAWAZIRI

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI ZA KAMATI MAALUMU ZA KITAALAMU (STCs) NA MIKUTANO MINGINE YA MAWAZIRI

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti za kamati Maalumu za Kitaalamu (STCs) na Mikutano mingine ya Mawaziri;

2. **LINAREJELEA** uamuzi EX.CL/Dec.1032(XXXIV) kuhusu kuahirisha kuanzishwa kwa taasisi na ofisi mpya;

3. **LINASISITIZA** kwamba maamuzi yafuatayo hayapaswi kuwa na athari zozote za kifedha, kisheria au kiutendaji kwa AU, na **LINATOA WITO** kwa Kamati zote na mabaraza na mikutano yote ya kitaalamu ya mawaziri kuacha kuanzisha miundo au bajeti yoyote ambayo haikujadiliwa na Vyombo vya Sera vya AU kupitia taratibu stahiki;

4. **LINAOMBA** kwamba STCs zote zipitishe ripoti zao mwishoni mwa mikutano yao.

**(A) KUHUSU RIPOTI YA MKUTANO WA KAWAIDA WA 5 WA STC KUHUSU UHAMAMIAJI, WAKIMBIZI NA WAKIMBIZI WA NDANI – Doc.EX.CL/1646(XLVIII)**

5. **LINAZINGATIA** ripoti ya Mkutano wa Kawaida wa 5 cha Kamati Maalumu ya Kitaalamu kuhusu uhamamiaji, Wakimbizi na Wakimbizi wa Ndani, uliofanyika kuanzia 10–14 Novemba 2025 Addis Ababa, Ethiopia, pamoja na mapendekezo yaliyomo ndani yake;

6. **LINAWAPONGEZA** Waziri na Wataalamu kwa Majadiliano yenye tija na matokeo ya Mkutano Ujao;

7. **LINAIDHINISHA** uamuzi wa Mkutano wa 5 wa STC-MRIDPs kufanya Mkutano Maalumu wa mtandaoni mwaka 2026, na Mkutano wa Kawaida wa 6 wa STC-MRIDP Mwaka 2027;

**KUHUSU UHAMIAJI NA UHURU WA WATU KUTEMBEA**

8. **LINAZINGATIA** ripoti za Utekelezaji kuhusu:

    i. Uanzishaji wa Kituo cha Kikanda cha Uendeshaji cha Sudan cha Kupambana na Uhamamiaji usio Rasmi (COC);
    ii. Uanzishaji wa Kituo cha Afrika cha Taaluma na Utafiti kuhusu Uhamiaji (ACSRM);

iii. Uanzishaji wa Mwangalizi wa Masuala ya Uhamiaji Afrika (AMO);
iv. Utekelezaji wa Mpango wa Afrika wa Mabadiliko ya Tabianchi na Uhuru wa Watu Kutembea (ACMI);
v. Tathmini ya Muda wa Kati ya Mfumo wa Sera za Uhamaji za Afrika (MPFA) na Mpango Wake wa Utekelezaji.

9. **AIDHA, LINAZINGATIA** uhamishaji wa muda wa Kituo cha Kikanda cha Kupambana na Uhamiaji Usio rasmi COC hadi Makao Makuu ya AU na **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuzingatia mipango ya kuwa mwenyeji wa muda ili kurahisisha uendeshaji kituo hicho kikamilifu.

10. **LINAIDHINISHA** nyaraka zifuatazo zilizopitishwa na STC-MRIDP:
i. Miongozo ya Kikanda kuhusu Kurejesha, Kupokelewa Upya na Urejeleaji Endelevu wa Wahamiaji pamoja na zana zinazosaidia mchakato huo;
ii. Nafasi ya Pamoja ya Afrika Kuhusu Uhamamiaji na Maendeleo (CAPMD);
iii. Mpango wa Utekelezaji wa Sera za AU za Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Watu Barani Afrika;
iv. Mpango wa Utekelezaji wa Sera za AU za Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Wahamiaji Barani Afrika;
v. Mpango wa Utekelezaji wa Makubaliano ya Kimataifa Kuhusu Uhamaji Salama, Ulio Pangiliwa na wa Kawaida (GCM) Barani Afrika.

11. **LINAELEKEZA,** kama kiongozi wa ACMI, kuratibu ajenda ya kikanda kuhusu uhamiaji na mabadiliko ya tabianchi na kusaidia Nchi Wanachama pamoja na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda katika kukabiliana na mwenendo na kuhama kwa watu kutokana na tabianchi.

12. **LINAIELEKEZA** Kamisheni:
i. Kuandaa na kutekeleza mpango wa usambazaji, kujenga uwezo, ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya Miongozo ya Kurejesha, Kupokelewa na Urejeleaji endelevu;
ii. Kuandaa Miongozo ya Kikanda kuhusu uratibu, ukusanyaji wa data na kubadilishana taarifa kuhusu wahamiaji waliopotea;
iii. Kuandaa Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Uhamiaji na Mabadiliko ya Tabianchi wa AU;
iv. Kushiriki katika Mkutano wa Pili (2) wa Kimataifa wa Mapitio ya Uhamiaji (IMRF).

**KUHUSU HATUA ZA UTEKELEZAJI WA MATOKEO YA MKUTANO MAALUMU WA MASUALA YA KIBINADAMU WA MALABO (2022)**

13. **LINAZINGATIA** ripoti ya utekelezaji ya Kamisheni kuhusu utekelezaji wa matokeo ya Mkutano Maalumu wa Masuala ya Kibinadamu wa Malabo na Mkutano wa Ahadi.

**14.** **LINATOA SHUKRANI** kwa Nchi Wanachama ambazo zimetimiza ahadi zao za kibinadamu na **LINAHIMIZA** zile ambazo bado hazijatimiza ahadi hizo kuzitekeleza bila kuchelewa.

**15.** **LINAIELEKEZA** Kamisheni:

- **i.** **Kuharakisha** uandaaji wa Kipimo cha Usaidizi wa Kibinadamu na Kipimo cha Fidia, kama ilivyopangwa na Mkutano wa Malabo, ili kuelekeza mgawanyo sawa wa majukumu na utengaji wa rasilimali.
- **ii.** **Kuandaa** Mfumo wa AU wa Afya katika Mchango wa Kibinadamu, Maendeleo, Amani kwa kushirikiana na Vyombo husika vya AU, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, na washirika, kwa ajili ya kuwasilishwa katika Mkutano Ujao wa Kawaida wa STC-MRIDPs.

## KUHUSU WAKALA WA AFRIKA WA MASUALA YA KIBINADAMU (AfHA)

**16.** **LINAZINGATIA** maelezo ya Kamisheni kuhusu uanzishaji wa Wakala wa Masuala ya Kibinadamu wa Afrika (AfHA) na **LINAPONGEZA** maendeleo yaliyofikiwa hadi sasa.

**17.** **LINAIOMBA** Kamisheni, kwa kushirikiana kwa karibu na Jamhuri ya Uganda, kuandaa mwongozo wa pamoja ili kurahisisha uanzishaji wa haraka wa Wakala wa Masuala ya Kibinadamu wa Afrika (AfHA).

**18.** **LINAIELEKEZA** Kamisheni:

- i. **Kuharakisha** mchakato wote wa kiutawala, kisheria na kitaratibu unaohitajika ili kufanya Wakala iweze kufanya kazi kikamilifu.
- ii. **Kuongeza** kasi ya mchakato wa uteuzi wa Bodi ya Utawala ya AfHA, kwa mujibu wa Sheria ya Wakala, na kuwasilisha katika Mkutano wa 5 Maalumu wa MRIDP kwa ajili ya kuidhinishawa.
- iii. **Kuimarisha** utayari wa kitaasisi wa AfHA, ikiwa ni pamoja na utayarishaji wa wafanyakazi, utafutaji wa rasilimali, mifumo ya uratibu, na ushirikiano na RECs/RMs, mashirika ya Umoja wa Mataifa, na wadau wa masuala ya kibinadamu.

## KUHUSU NA MIFUMO YA MISINGI YA KIBINADAMU

**19.** **LINAIDHINISHA** yafuatayo bila kuwa na athari za kifedha, kisheria au kiutendaji:

- i. Mpango wa Utekelezaji wa Uidhinishaji wa Itifaki ya Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki za Binadamu kuhusu Hali ya Utaifa na Kuondoa kutokuwa na Utaifa Afrika.
- ii. Mpango wa Utekelezaji wa Ahadi zilizotolewa katika Mkutano wa Kimataifa wa Wakimbizi (GRF), kama zilivyorekebishwa na STC-MRIDP ya Tano (5).

**20.** **LINAIELEKEZA** Kamisheni:

i. **Kuharakisha** mchakato wa kupokea maoni kutoka Nchi Wanachama kuhusu Mfumo wa Diplomasia ya Kibinadamu wa Umoja wa Afrika, na kuwasilisha rasimu ya mwisho katika Mkutano Maalumu wa Tano (5) wa STC-MRIDP kwa ajili ya kuidhinishwa.

ii. **Kuandaa** Maelezo na Mwongozo wa Ufafanuzi kuhusu Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Ulinzi na Msaada kwa Wakimbizi wa Ndani Barani Afrika (Mkataba wa Kampala), ili kuongoza Nchi Wanachama wa Mkataba katika utekelezaji wa Itifaki; na kuwasilisha katika Mkutano ujao wa Kawaida wa STC kwa ajili ya kuidhinishwa.

iii. **Kutoa Ufafanuzi wa Kisheria wa** Ibara ya I(2) ya Mkataba wa Wakimbizi wa OAU wa 1969 kuhusiana na kuhama kwa watu kutokana na mabadiliko ya tabianchi na maafa, na kuripoti katika Mkutano ujao wa STC-MRIDPs.

**KUHUSU MAJANGA, MABADILIKO YA TABIANCHI NA UHAMAJI KWA LAZIMA**

**21.** **LINAIDHINISHA** yafuatayo bila kuwa na athari za kifedha, kisheria au kiutendaji:
i. Sheria ya Kielelezo ya Umoja wa Afrika kuhusu Utayari na Mwitikio wa Majanga katika Muktadha wa Kibinadamu.

**22.** **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuimarisha utayari wa kitaifa wa kukabiliana na majanga kwa ajili ya mifumo ya tahadhari ya mapema, na uwezo wa jamii kukabiliana na athari za kuhama kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

**23.** **LINAIELEKEZA** Kamisheni kuzisaidia Nchi Wanachama katika kukabiliana na athari zinazotokana na shughuli za binadamu za mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo kupitia hatua za kuchukua tahadhari ya mapema na upangaji unaotegemea tathmini ya vihatarishi.

**KUHUSU UHURU WA WATU KUTEMBEA BARANI AFRIKA**

**24.** **LINAZINGATIA** ripoti ya Hali ya Uhuru wa Watu Kutembea Barani Afrika (2023–2025) na **LINAIAGIZA** Kamisheni kutoa taarifa katika Mkutano Ujao wa Kawaida wa STC.

**25.** **LINAIPONGEZA** Tume na Kamati Ndogo kwa kujumuisha maeneo ya uhamiaji na kazi kwenye dhumuni la jumla la kutoa mwelekeo kamili wa bara wa sera za kimkakati na kushauri kama inavyoelekezwa na uamuzi EX.CL/Dec.1238 (XLIV) wa Februari 2024.

**26.** **LINAIDHINISHA** yafuatayo bila kuwa na athari za kifedha, kisheria au kiutendaji:

i. Mkakati wa Umoja wa Afrika wa Kuhamasisha Utambulisho wa Itifaki ya Uhamaji Huru;

ii. Mfumo wa Uratibu wa Umoja wa Afrika katika utekelezaji wa Itifaki ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika unaohusiana na Uhamaji Huru wa Watu, Haki ya Makazi na uhuru wa kuanzisha biashara ya kudumu katika nchi zingine wanachama.

**(B) KUHUSU RIPOTI YA MKUTANO WA 8 WA KAWAIDA WA KAMATI MAALUM YA KITAALAMU (STC) YA FEDHA, MASUALA YA FEDHA, MIPANGO NA UTANGAMANO WA KIUCHUMI ULIOFANYIKA KUANZIA TAREHE 29 SEPTEMBA HADI 03 OKTOBA 2025, JOHANNESBURG, AFRIKA KUSINI**

**27.** **LINAPOKEA** na **KUPITISHA** ripoti na Azimio la Mkutano wa Nane (8) wa Kawaida wa STC kuhusu Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango na Utangamano wa Kiuchumi, na mapendekezo yaliyomo ndani yake;

**28.** **LINARIDHISHWA** na maendeleo kuelekea kuanzishwa kwa Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika, Taasisi ya Ukadiriaji wa Mikopo Afrika, na mipango mingine ya bara kama vile Jukwaa la Afrika la Uwekezaji kwa njia ya Mtandao, Miongozo ya Huduma ya Malipo Afrika (PSDA) na Kitambulisho cha Taasisi Afrika (AEI);

**29.** **LINASISITIZA** umuhimu wa ufadhili wa afya kama jambo muhimu katika mabadiliko ya Afrika, huku likitambua changamoto ambazo nchi za Afrika hukabiliana nazo katika mazingira ya kiuchumi yanayobadilika duniani;

**30.** **LINASISITIZA** kwamba kuziba pengo la upatikanaji wa gharama za masuala ya afya barani Afrika katika muktadha wa kijiografia unaobadilika ni muhimu kwa kuimarisha uhimilivu wa kifedha na uhuru wa bara, kukuza ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu.

**31.** **LINAAMUA** yafuatayo:

**KUHUSU "KUZIBA PENGO LA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MASUALA YA AFYA AFRIKA KATIKA MUKTADHA WA KIUCHUMI NA KIJIOGRAFIA UNAOBADILIKA: CHANGAMOTO NA MASULUHISHO MUHIMU**

**32.** **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutekeleza ongezeko la kila mwaka la mgao wa bajeti kwa sekta ya afya, kwa lengo la kufikia na kudumisha lengo la Azimio la Abuja la 15%, huku utendaji ukifuatiliwa dhidi ya Kadi ya Alama ya Afrika;

**33.** **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutekeleza Kodi Bunifu za Afya, kwa msisitizo wa kuhamasisha kuanzishwa kwa kodi za afya kwa bidhaa zenye madhara ili kuongeza mapato na kupunguza matumizi yanayotokana na matibabu ya kiafya;

**34.** **LINAZISIHI** Nchi Wanachama kutumia Programu ya Uwekezaji na Ufadhili wa AUDA-NEPAD katika Afya ya Afrika (PIFAH) kwa ajili ya maendeleo na maandalizi ya miradi ya uwekezaji ya kipaumbele kuelekea mabadiliko ya uchumi wa afya wa Afrika;

35. **LINATOA WITO** kwa Kamisheni na RECs kuzisaidia Nchi Wanachama wa AU katika kujadili masuala ya ufadhili wa afya duniani, urekebishaji wa madeni na ugharimiaji wa masuala ya tabianchi;

36. **LINAIOMBA** Kamisheni, AUDA-NEPAD, Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika na wadau wengine husika kusaidia Nchi Wanachama kuboresha sekta ya afya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFM) kwa kuhamia kwenye malengo ya matokeo, yenye vigezo vinavyopimika, kuimarisha uwezo wa kibinadamu na kitaasisi na mifumo ya kisasa ya taarifa ndani ya Wizara za Afya;

37. **LINAZISISHI** Nchi Wanachama kuweka kipaumbele na kutenga fedha kwa ajili ya Huduma ya Afya ya Msingi ya Umma (PHC) na rasilimali watu kwa ajili ya afya kupitia utoaji wa gharama wa Msaada wa Manufaa Muhimu ya Afya ili kupunguza malipo kutoka mfukoni kwa mteja (OOP);

38. **LINAISIHI ZAIDI** AAMFI kutoa msaada wa kitaalamu na kifedha unaohitajika kwa Mfuko wa AU wa Magonjwa ya Mlipuko kwa lengo la kufikia lengo lake; na

39. **LINAIAGIZA** Kamisheni, UNECA, AfDB, AAMFI na AUDA-NEPAD kupitia PIFAH kuunga mkono juhudi za Nchi Wanachama katika kujaribu na kupanua nyenzo bunifu za ufadhili, ikiwa ni pamoja na mifumo mchanganyiko ya fedha inayojumuisha mitaji ya umma, binafsi, na ya uhisani kwa ajili ya miundombinu muhimu kama vile afya ya kidijitali na Mabadilishano ya Madeni kwa Afya.

**KUHUSU KUIMARISHA UTAFUTAJI WA RASILIMALI ZA NDANI BARANI AFRIKA: KUJADILI RIPOTI YA KAMATI NDOGO YA NNE YA STC KUHUSU KODI NA MTIRIRIKO WA FEDHA HARAMU**

40. **LINAPITISHA** ripoti ya Kamati Ndogo ya Nne (4) ya STC kuhusu Kodi;

41. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kupanua misingi ya kodi, kupunguza misamaha, kuoanisha motisha, kurekebisha sera zao za mkataba wa kodi na kutekeleza mageuzi mengine ya sera ya kodi yenye mabadiliko ikiwa ni pamoja na kufanya kazi na Kamisheni, ATAF, TJNA, UNECA, ACBF na wadau wengine husika ili kusaidia kubuni na kutekeleza sheria madhubuti za ushuru wa uchumi wa kidijitali, kwenye usimamizi wa kodi na kanuni ili kushughulikia IFF kwa ufanisi, Mmomonyoko wa Msingi na Ubadilishaji wa Faida;

42. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kushirikiana na Kamisheni, ATAF, TJNA, UNECA, ACBF na wadau wengine kutekeleza mikakati ya kodi ya AU na IFF. Hii ni pamoja na kukuza uwazi, kuanzisha wasajili wa umiliki wenye manufaa, kupitisha hati za bara kwa ajili ya msaada wa kiutawala wa pande zote, kukuza Chombo cha Ufuatiliaji wa Sera ya Kupambana na IFF, na kuimarisha mipango ya urejeshaji mali;

43. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kushirikiana na Kamisheni, ATAF, AfDB, ACBF, UNECA na wadau husika ili kuongeza uwezo wa maafisa. Hii inajumuisha kuwezesha utaratibu wa kujifunza kwa pamoja barani kote na kuimarisha utaalamu katika gharama za uhamishaji, ukaguzi, uchumi wa kidijitali, na ushuru wa maliasili;

44. **LINAHIMIZA** Kamisheni, ATAF, TJNA, ACBF na UNECA kuendelea kuwasaidia wataalamu wa Afrika wanaohusika katika mazungumzo katika majukwaa mbalimbali ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na Umoja wa Mataifa, Mpangp Jumuishi wa OECD, na G20;

45. **PIA LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutekeleza mageuzi ya kodi na fedha muhimu kwa AfCFTA, ikiwa ni pamoja na kupanua mtandao wa mkataba wa kodi na kuratibu au kuoanisha sera za kodi;

46. **LINATOA WITO KWA** Kamisheni na ATAF kushirikiana katika kuhakikisha kwamba Kamati ya Pamoja ya Kitaalamu kuhusu kodi inafanya kazi kwa pampja na kamati Ndogo ya STC kuhusu kodi na IFF, kutoa masuluhisho ya kitaalamu kwa masuala yanayohusiana na kodi barani Afrika; na

47. **LINAZIHIMIZA** Kamisheni, ACBF, ATAF, TJNA kuimarisha ushirikiano wao ili kuendeleza mkakati wa bara kuhusu ushuru wa uchumi wa kidijitali.

**KUHUSU KUIMARISHA USIMAMIZI WA MADENI BARANI AFRIKA: KUJADILI AZIMIO LA LOME NA RASIMU YA MSIMAMO WA PAMOJA WA AFRIKA KUHUSU MADENI KAMA NYARAKA ZA MATOKEO YA MKUTANO WA MADENI WA UMOJA WA AFRIKA**

48. **LINAPOKEA NA KUPITISHA** Azimio la Lome kuhusu Mkutano wa Madeni wa AU na mapendekezo yaliyomo;

49. **LINAPITISHA** Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Madeni na **KUZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuutumia kama nyaraka ya marejeleo kwa ajili ya mazungumzo ya madeni katika mijadala ya kimataifa na kama mpango wa usimamizi endelevu wa madeni;

50. **LINAIOMBA** Kamisheni ifafanue ratiba na majukumu ya utekelezaji ili kuhakikisha kwamba Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Madeni inaweza kutekelezwa na si cha matarajio tu;

51. **LINATOA WITO** kwa Kamisheni kuanzisha na kuendesha Mpango wa Ufuatiliaji wa Madeni wa Afrika (ADMM) ndani ya Idara ya ETTIM kama jukwaa la mtandaoni lisilo na wajibu wa kisheria, kimuundo na kifedha kwa Nchi Wanachama, kwa msaada wa kifedha na kitaalamu wa AAMFI.

**KUHUSU TAARIFA YA TAASISI YA UKADIRIAJI WA MIKOPO WA AFRIKA**

**52.** **LINAKARIBISHA** kutangazwa kwa Mauritius kama mamlaka ya msingi ya AfCRA; na

**53.** **LINAZISIHI** Nchi Wanachama zinazopenda kujiandikisha katika AfCRA kuwasilisha Tamko lao la Dhamira kwa APRM ili lipitiwe na mshauri wa shughuli;

**KUHUSU JUKWAA LA AFRIKA LA UWEKEZAJI KWA NJIA YA MTANDAO (AVIP)**

**54.** **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuonyesha nia yao ya kujiunga na awamu ya majaribio ya AVIP;

**55.** **LINAIOMBA** Kamisheni kutengeneza mwongozo wa ujumuishaji wa data, unaoungwa mkono na mipango ya kuhakikisha ubora, ufuatiliaji na tathmini;

**56.** **PIA LINAIOMBA** Kamisheni kuhakikisha kwamba Jukwaa linawezesha mawasiliano ya mara kwa mara na ya wazi na wawekezaji kwa lengo la kukuza kipimo cha athari za uwekezaji; na

**57.** **LINASISITIZA** Kamisheni na OECD kuharakisha utendaji kazi wa AVIP ili kusaidia Nchi Wanachama kuboresha wasifu wao wa uwekezaji ili kuvutia rasilimali zaidi za kifedha.

**KUHUSU MWONGOZO WA HUDUMA YA MALIPO AFRIKA (PSDA)**

**58.** **LINAIHIMIZA** Kamisheni na AfricanNenda Foundation kuendelea kushauriana na wadau muhimu kuhusu PSDA, hasa AACB na kuripoti maendeleo kupitia Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Uchumi na Ujumuishaji; na

**59.** **PIA LINAHIMIZA** Kamisheni na AfricaNenda Foundation kukamilisha utafiti unaoendelea wa upembuzi yakinifu kuhusu PSDA na kuripoti maendeleo kupitia Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango na Ujumuishaji. wa Kiuchumi

**KUHUSU NAMBA YA UTAMBULISHO YA AFRIKA (AEI)**

**60.** **LINAKARIBISHA** mpango wa AEI na kuzingatia kazi inayoendelea ya kuijumuisha AEI chini ya Protokali ya Biashara ya Kidijitali ya AfCFTA; na

**61.** **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuharakisha ujumuishaji wa AEI na mifumo ya vitambulisho vya kitaifa na miundombinu ya kifedha, ikiwa ni pamoja na usajili wa mikopo, majukwaa ya fedha za simu, na mifumo ya malipo ya kidijitali, ili kupanua utumiaji miongoni mwa biashara ndogo na za kati na kuongeza uaminifu wa Afrika katika masoko ya kimataifa.

**(C) KUHUSU RIPOTI YA STC YA KUMI (10) YA USAWA WA KIJINSIA NA UWEZESHAJI WA WANAWAKE**

**Mkataba wa AU wa Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana (AU CEVAWG) na Kampeni ya Uridhiaji, Uingizaji katika Sheria za Nchi na Utekelezaji wa Mkataba**

**62.** **LINAIDHINISHA** mbinu ya utekelezaji wa awamu tatu ya Mpango wa Kusaini, Uidhinishaji, Uingizaji kwenye mipango ya ndani, na Utekelezaji wa AU-CEVAWG:

(i) Awamu ya 1: Kuanza kutumika ndani ya miezi kumi na minane (18), kuanzia kupitishwa kwake mnamo Februari 2025;
(ii) Awamu ya 2: Uwiano wa kisheria na uimarishaji wa kitaasisi ndani ya miaka mitatu (3);
(iii) Awamu ya 3: Athari endelevu na uwajibikaji ndani ya miaka mitano (5), kwa kuzingatia Sheria, kanuni, na mikakati ya Kitaifa ya Nchi Wanachama

**63.** **LINAIAGIZA** Kamisheni kwa kushirikiana kwa karibu na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu (ACHPR),:
(i) Kuanzisha utaratibu wa kufuatilia maendeleo dhidi ya kila awamu, ikiwa ni pamoja na ukusanyaji na uchambuzi wa data kuhusu uridhiaji, uingizwaji kwenye mipango ya ndani, na utekelezaji katika Nchi Wanachama
(ii) Kutoa msaada wa kitaalamu ulioratibiwa na ujenzi wa uwezo kwa Nchi Wanachama katika michakato ya uridhiaji, ujumuishaji wa sheria, na utekelezaji wa vipengele vya Mkataba.

**64.** **LINAZISIHI** Nchi Wanachama zote kuharakisha michakato ya ndani kwa ajili ya kutiwa saini na kuidhinishwa kwa Mkataba ili kufanikisha kuanza kutumika kwake ndani ya miezi kumi na minane (18), kwa kuzingatia sheria, kanuni, na mikakati ya kitaifa ya Nchi Wanachama.

**65.** **LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kwa kushirikiana na RECs, Vyombo vya AU, Mashirika Maalum na wabia, kuzisaidia Nchi Wanachama kwa utetezi na usaidizi wa kitaalamu ili kuharakisha uridhiaji, uingizwaji kwenye mipango ya ndani na utekelezaji wa AU-CEVAWG na kuripoti maendeleo kwa kikao kijacho cha STC-GEWE.

**Kuhusu Ripoti ya Mwaka 2024 ya Tamko la Usawa wa Kijinsia Barani Afrika**

**66.** **LINAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa Tamko la Usawa wa Kijinsia Barani Afrika.

**67.** **LINAZINGATIA ZAIDI** uamuzi wake wa mwaka 2023 uliopitisha Kitengo cha Uangalizi wa Masuala ya Kijinsia kama mfumo wa kuripoti utekelezaji wa nyaraka zinazohusiana na masuala ya kijinsia, na **LINAIAGIZA** Kamisheni kurekebisha

muundo wa ripoti ya Tamko la Usawa wa Kijinsia Barani Afrika ili kuwezesha Nchi Wanachama kuchambua maendeleo kwa kina katika kuendeleza usawa wa kijinsia na kuwezesha Uangalizi wa Masuala ya Kijinsia kuwa hifadhidata ya ripoti za Nchi Wanachama, kama vile za Tamko la Usawa wa Kijinsia Barani Afrika

68. **LINAPITISHA** ripoti ya Utekelezaji wa Tamko la Usawa wa Kijinsia Barani Afrika.

69. **LINATAMBUA** maamuzi ya Baraza la Amani na Usalama (PSC) kuhusu Wanawake, Amani na Usalama na, kwa muktadha huu, hitimisho lililopitishwa katika Mkutano wa 1309 cha Baraza la Amani na Usalama uliofanyika tarehe 30 Oktoba 2025, na kusisitiza umuhimu wa kuimarisha Ofisi ya Mjumbe Maalum wa AU wa Masuala ya Wanawake, Amani na Usalama kupitia ugharimiaji unaoweza kutegemewa na wa kutosha kutoka bajeti ya kawaida ya AU.

70. **LINATAMBUA** Nchi Wanachama arobaini na sita (46) ambazo tayari zimeridhia Itifaki ya Maputo.

71. **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama tisa (9) ambazo bado hazijasaini au kuridhia Itifaki ya Maputo, huku zikithibitisha uhuru wao, kuchukua hatua zinazofaa katika ngazi ya kitaifa na kuwasilisha hati zao za kuridhia kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika.

**Ripoti ya Kazi za Uongozi (*Bureau*) wa STC ya Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake**

**Mjadala wa Kwanza wa Egumeni kuhusu Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake**

72. **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kujumisha masuala ya usawa wa kijinsia kwa uthabiti katika sera zote na ajenda za maendeleo, ikiwamo mipango ya amani na usalama, pale inapofaa.

73. **LINATAMBUA** kuhusu Uzinduzi wa Kampeni ya Kikanda, ikijumuisha mabaraza ya kiutamaduni/kidini na kujenga hifadhi ya maarifa kuhusu usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana, ikiwamo kuendesha Mjadala wa Egumeni kama jukwaa la kila mwaka kuhusu usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana.

74. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuunda mifumo ya ufuatiliaji inayotegemea ushahidi ili kufuatilia maendeleo katika kushughulikia mitazamo ya kijinsia na viashiria vinavyohusiana.

**Misheni ya Utetezi katika Jamhuri ya Afrika ya Kati na Misri**

75. **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama ambazo bado hazijasaini au kuridhia kuchukua hatua zinazofaa katika ngazi ya kitaifa na kuwasilisha nyaraka zao za kuridhia kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika.

**Taarifa Fupi ya Maendeleo ya Nusu Muhula ya Muongo wa Wanawake wa Afrika kuhusu Ujumuishaji wa Wanawake Kifedha na Kiuchumi, 2020-2030**

76. **LINATAMBUA** matokeo ya Taarifa ya Muda wa Kati ya Muongo wa Wanawake wa Afrika kuhusu Ujumuishaji wa Kifedha na Kiuchumi (AWD-FEI 2020-2030) na kuahidi kujumuisha masuala yanayozingatia masuala ya kijinsia, katika nyanja zote ikiwa ni pamoja na masuala ya fedha, ufadhili na viashiria.

77. **LINATAMBUA** mapengo yaliyopo katika sera, utekelezaji, uratibu, na dhamira ya kuimarisha mifumo ya uwajibikaji ya kitaifa na kikanda kwa ajili ya ujumuishaji wa kifedha na kiuchumi wa wanawake.

78. **LINAIOMBA** Kamisheni kuandaa Mpango wa Kuongeza Kasi ya utekelezaji wa AWD-FEI kupitia Mpango wa Ujumuishaji Kifedha na Kiuchumi wa Wanawake na Vijana (WYFEI 2030*)* na kujitolea kuimarisha mifumo ya uwajibikaji ya kitaifa na kikanda.

**Jukumu la Asasi za Kiraia katika kuendeleza Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake barani Afrika**

79. **LINAZINGATIA** jukumu la asasi za kiraia na mashirika ya wanawake katika kufuatilia na kukuza usawa wa kijinsia katika nchi wanachama zote

80. **LINAZINGATIA PIA** ombi la ECOSOCC la kuitisha AZAKI ikiwa ni pamoja na vyama vinavyofanya kazi katika nyanja za masuala ya wanawake, ili kutafakari masuala yanayoibuka ya kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na kutoa taarifa kwenye sera na ufanyaji maamuzi wa Kamati Maalumu ya Kitaalamu Kuhusu Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake.

81. **LINAIMARISHA** ushirikiano kati ya wizara zinazohusika na masuala ya jinsia na wanawake katika ngazi ya kitaifa na mashirika/mitandao ya wanawake na AZAKI.

**Kuhusu Ripoti ya Shirika la Wanawake wa Afrika**

82. **INAZINGATIA ZAIDI** maendeleo yaliyofanywa na Shirika la Wanawake wa Afrika (PAWO), huku pia likitambua changamoto za kifedha zinazoendelea zinazozuia uwezo wake kamili wa kiuendeshaji, ikiwa ni pamoja na hitaji la angalau dola za Marekani milioni Sita 6 (Dola milioni 6) kila mwaka ili kutekeleza vizuri programu na shughuli zake.

**Taarifa Fupi ya Uwezeshaji wa Kikundi Kazi cha Wanawake20 Kinachojikita kwenye Kazi ya Uangalizi**

83. **LINAIOMBA** AUC kuwezesha uandaaji wa Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Kazi ya Uangalizi, kwa kutumia mbinu inayozingatia Afrika ambayo inaakisi hali halisi na vipaumbele vya Afrika.

84. **LINAIOMBA PIA** Kamisheni kuitisha Jukwaa la Uangalizi la Afrika kama jukwaa la bara la kubadilishana maarifa, mazungumzo ya sera na ukuzaji wa masuluhisho na uvumbuzi wa Afrika ili kubadilisha kazi ya utunzaji.

85. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuandaa mikakati ya kitaifa ya utunzaji.

86. **LINATOA WITO KWA** AUC, kwa kushirikiana na wabia husika, kupanga na kuandika ushahidi kuhusu faida za kijamii na kiuchumi za kuwekeza katika miundombinu ya kijamii.

**KUPITISHWA KWA MSIMAMO WA PAMOJA WA AFRIKA KWA AJILI YA CSW70**

87. **LINAANZISHA** utaratibu rasmi wa mzunguko na ECOSOCC ili kuhakikisha uandaaji sawa wa vikao vya CSW na kupendekeza kwamba Afrika iandae Kikao cha kwanza cha CSW;

## (D) KUHUSU RIPOTI YA KIKAO CHA KAWAIDA CHA TANO (5) CHA KAMATI MAALUM YA KITAALAMU (STC) YA UMOJA WA AFRIKA KUHUSU VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO STC-YCS(V)

88. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kikao cha Kawaida cha Tano (5) cha Kamati Maalum ya Kitaalamu ya AU kuhusu Vijana, Utamaduni na Michezo (STC-YCS5) kilichofanyika tarehe 9 - 13 Desemba 2025 mjini Bujumbura, Burundi

89. **LINAIDHINISHA**:

a) Uchaguzi wa wajumbe wapya wa Ofisi ya STC-YCS5.

b) Mapendekezo ya Ripoti ya Mkutano wa Mawaziri wa STC-YCS ni kama ifuatavyo

**KUHUSU MAENDELEO YA VIJANA**

**(1) KUHUSU MKATABA WA VIJANA WA AFRIKA @20**

90. **LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuanzisha mapitio ya Mkataba wa Vijana wa Afrika kwa kufufua Ibara ya 31 na kufuata masharti yake ya kiutaratibu.

91. **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama ambazo bado hazijaridhia Mkataba huo kuharakisha mchakato wa kufikia uridhiaji wa wote ifikapo mwisho wa 2026.

92. **LINAOMBA PIA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kushirikiana na Nchi Wanachama, RECs, AUDA-NEPAD, Umoja wa Vijana wa Afrika, Mabaraza ya Vijana ya Kitaifa, na wadau wengine muhimu kufanya majadiliano ya kikanda yanayoongozwa na vijana mwaka 2026 kuhusu masuala yanayoibuka ya vijana.

### *(2)* KUHUSU MPANGO WA *ONE (1) MILLION NEXT LEVEL (1MNL)*

93. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama kushirikiana kikamilifu katika kuwasilisha ripoti za kila mwaka na katika kuandaa Mikakati ya Kuongeza Kasi ya Nchi inayoendana na nguzo na shabaha za Mpango wa *1 Million Next Level (1MNL)*.

94. **LINAOMBA** Kamisheni kutoa msaada wa kitaalamu kwa Nchi Wanachama na kuitisha vikao vya kujenga uwezo kuhusu Kadi ya Alama na Mikakati ya Kuongeza Kasi ya Nchi kwa kushirikiana na wadau

95. **LINAIOMBA PIA** Kamisheni kuchapisha ripoti ya hali ya bara kwenye Kadi ya Alama ya 1MNL na kuwasilisha matokeo kwenye kikao kijacho cha STC-YCS.

96. **LINAIPONGEZA** Kamisheni, kwa kushirikiana na Nchi Wanachama na washirika, kwa kuongoza uandaaji na uthibitishaji wa Jedwali la Alama (Scoreboard) la Mpango wa "One Million at the Next Level", kwa mujibu wa maamuzi ya STC-YCS-4.

97. **LINAUPONGEZA PIA** uongozi wa Algeria, Burundi, Jibouti, Misri, Kenya, Namibia na Uganda katika kuendeleza uwezeshaji wa vijana wa Afrika kupitia uzinduzi wa Mpango wa "*One Million at the Next Level*", na **LINAZIOMBA ZAIDI** Nchi Wanachama zote kuzindua mpango huu katika muktadha huo.

98. **LINAKARIBISHA NA KUIDHINISHA** Jedwali la Alama (Scoreboard) la Mpango huu kama utaratibu wa bara kwa ajili ya kupima utendaji na uwajibikaji wa vijana, unaoendana na Mkataba wa Vijana ya Afrika na Ajenda yam waka 2063.

### (3) KUHUSU MWAKA WA KIMATAIFA WA WANAOJITEOLEA WA 2026

99. **LINAKARIBISHA** Azimio 78/127 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) linalotangaza 2026 kama Mwaka wa Kimataifa wa Wanaojitolea kwa Maendeleo Endelevu na **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama wa AU kuimarisha kujitolea kupitia sera, programu thabiti na rasilimali endelevu za kitaifa.

100. **LINAYAOMBA** mashirika ya uratibu wa kujitolea ya kikanda na kitaifa kufanya kazi kwa karibu na Kamisheni katika kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Mwaka wa Kimataifa wa Wanaojitolea.

### (4) KUHUSU RIPOTI ZA UMOJA WA VIJANA

**101.** **LINAREJELEA** pendekezo la STC-YCS 4 kuhusu kufufua uhusiano kati ya Umoja wa Vijana Afrika (PYU) na Kamisheni kupitia mkataba wa makubaliano;

**102.** **LINASIFU** kutiwa saini kwa Hati ya Makubaliano kati ya Kamisheni na PYU kama nyenzo muhimu ya kufufua, kurekebisha na kuimarisha PYU;

**103.** **LINAZIOMBA** Kamisheni na PYU kwa pamoja kuandaa Mpango wa utekelezaji wa haraka wa Hati ya Makubaliano na kuwasilisha taarifa ya maendeleo katika kikao kijacho cha STC-YCS.

**(5) KUHUSU RIPOTI ZA JUKWAA LA VIJANA WA AFRIKA**

**104.** **LINAISIFU** na **KUIPONGEZA** Algeria na Djibouti kwa kuwa wenyeji na kuandaa Majukwaa ya Vijana wa Afrika ya 2024 na 2025, mtawalia, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Nchi Wanachama, mashirika ya vijana, wabia na wadau.

**105.** **LINATAMBUA** jukumu la Jukwaa katika kukuza ushiriki na uwezeshaji wa vijana na linahimiza kuandaliwa kwake kila mwaka kulingana na maamuzi ya STC-YCS (2) ya kulianzisha.

**106.** **LINAPITISHA** Azimio la Oran la 2024 na Azimio la Djibouti la 2025 kama ilivyowasilishwa na vijana kutoka kwenye majukwaa hayo mawili ya vijana.

**KUHUSU MATOKEO YA UTAMADUNI**

**(1) KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI ZA SEKTA YA SANAA, UTAMADUNI NA URITHI KWA KIPINDI CHA 2023–2025**

**107.** **LINAIOMBA** Kamisheni ya AU kuhakikisha kwamba taarifa kuhusu programu zake za sanaa, utamaduni na urithi zinasambazwa kwa karibu na kwa uendelevu kwa Wizara zinazohusika na sanaa, utamaduni na urithi.

**108.** **LINAZIOMBA PIA** Nchi Wanachama kuchukua hatua za kuharakisha mchakato wa kuridhia hati muhimu za sanaa, utamaduni na urithi, ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Mwamko wa Utamaduni wa Afrika na Sheria ya Tume ya Sauti na Picha na Sinema ya Afrika (*African Audio-Visual and Cinema Commission*)

**109.** **LINAZISIHI** Nchi Wanachama kuharakisha mchakato wa utekelezaji wa uamuzi Assembly/AU/Dec/872 (XXXIV), ambao **UNATOA WITO KWA** Nchi Wanachama kutoa angalau 1% ya bajeti za kitaifa kwa sekta ya sanaa, utamaduni na urithi. Ahadi hii ya fedha ni muhimu kwa ajili ya kutoa msaada unaoendelea kwa mipango ya kitamaduni, ukuzaji wa uwezo na ulinzi wa urithi tajiri wa Afrika.

**(2) KUHUSU MSWADA WA SERA YA ELIMU YA SANAA YA UMOJA WA AFRIKA**

110. **LINAIDHINISHA** Rasimu ya Sera ya Elimu ya Sanaa ya Umoja wa Afrika, **LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kufungamanisha sera za kitaifa na Sera ya Elimu ya Sanaa.

111. **LINAZIOMBA PIA** Nchi Wanachama kuingiza elimu ya sanaa katika mtaala wa shule katika ngazi zote.

112. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuanzisha majukwaa ya kitaifa ya uratibu pamoja na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya elimu ya sanaa.

**(3) KUHUSU HATUA ZILIZOFIKIWA KATIKA UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA MAKUMBUSHO KUU YA AFRIKA PAMOJA NA KUJADILI MSWADA WA SHERIA YAKE (GMA)**

113. **LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kuendela kuiunga mkono Makumbusho Kuu ya Afrika iliyopo Algeria ambayo ni Mradi Kielelzo wa Ajenda ya Umoja wa Afrika wa mwaka 2063.

114. **LINAIDHINISHA** Rasimu ya Sheria ya Makumbusho Kuu ya Afrika (GMA): Mradi mkubwa wa Ajenda 2063 ya AU, na **LINAIOMBA PIA** Kamisheni kuwasilisha hati ya kisheria kwa STC ya Haki na Masuala ya Kisheria kwa ajili ya kujadiliwa.

115. **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama kuiunga mkono Algeria katika utekelezaji kamili wa Eneo la Muda Mfupi la Jumba Kuu la Makumbusho la Afrika na shughuli zake za bara;

116. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuharakisha uandaaji wa Maonyesho ya 2 ya Bara ya Jumba Kuu la Makumbusho la Afrika.

**(4) KUHUSU MFUMO WA UTEKELEZAJI WA KONGAMANO LA SITA (6) LA UTAMADUNI LA AFRIKA LA UMOJA WA AFRIKA (AU/PACC6)**

117. **LINAIDHINISHA** Mfumo wa Utekelezaji wa Kongamano la Sita (6) la Utamaduni la Umoja wa Afrika (AU/PACC6), kwa ajili ya utekelezaji unaofuata unaofanywa na wadau wote.

118. **LINAIOMBA** Kamisheni kukuza Sekta za Utamaduni na Ubunifu za Afrika katika nyanja zake zote ili kuhakikisha ukuaji wake na mchango ulioimarishwa katika kujenga Afrika Tunayoitaka, kama ilivyobainishwa katika matarajio na mpango kabambe wa Ajenda ya mwaka 2063, hususan Lengo kuu la 5.

119. **LINAHIMIZA** kuanzishwa kwa Orodha ya Urithi wa Afrika ya maeneo ya kiutamaduni na maeneo asili ili kusaidia Nchi Wanachama katika kutangaza na kutambulisha utajiri wa urithi wao, pamoja na kuboresha usimamizi wa rasilimali za urithi, hasa zile zilizomo katika Orodha ya Hatari ya UNESCO.

120. **LINAZIOMBA PIA** Nchi Wanachama kuunga mkono programu zinazohamasisha vijana kufurahia na kuelewa urithi wao wa kiutamaduni na maeneo asilia, pamoja na kuendeleza shughuli za ujasiriamali zinazohusiana na urithi huo.

### (5) KUHUSU MFUMO WA UTEKELEZAJI WA KUIMARISHA NA KUKUZA SEKTA SANAA YA SAUTI, PICHA NA FILAMU BARANI AFRIKA

121. **LINAIDHINISHA** Mpango wa Utekelezaji wa Tukio la Wadau kuhusu Sauti na Filamu kwa ajili ya utekelezaji na Tume ya Afrika ya Sauti na Filamu (AACC) na **LINAINAPONGEZA** Jamhuri ya Kenya kwa kuzindua Sekretarieti ya Muda ya Tume ya Afrika ya Sauti na Filamu.

122. **LINAIAGIZA** Tume ya Sauti na Filamu ya Afrika (AACC) kuongoza juhudi za kubadilisha simulizi kuhusu Afrika kupitia usimulizi wa kimkakati na kukuza maudhui ya ndani katika uzalishaji wa filamu na kazi za sauti na picha.

123. **LINATETEA** Afrika kuandaa mfumo wake wa ndani wa ukusanyaji wa takwimu za Sekta za Utamaduni na Ubunifu, ambao utapanua vyanzo vya ukusanyaji wa data kutoka vile vya jadi hadi kujumuisha data za kiutawala, usajili wa biashara, vyama vya kitaaluma, watoa huduma wa takwimu kubwa na vituo vya ufuatiliaji wa utamaduni, ili kuzalisha takwimu sahihi, za kuaminika na za wakati unaofaa kwa ajili ya kusaidia maamuzi ya kibiashara na uwekezaji katika sekta hiyo.

### (6) KUHUSU RIPOTI YA AKADAMIA YA LUGHA ZA AFRIKA (ACALAN)

124. **LINAOMBA** Nchi Wanachama na wabia kuunga mkono kazi ya ACALAN kupitia ubia, uhamishaji wa muda mfupi wa wafanyakazi, wanaojitolea na wanafunzi wa mafunzo ili kufidia mapengo ya rasilimali watu ndani ya taasisi.

125. **LINAOMBA PIA** Nchi Wanachama ambazo hazina vyombo vya kitaifa vya wataalamu wa lugha kufikiria kuunda vyombo hivi ili kusaidia tafsiri ya hati za kitaifa za kimkakati katika lugha za Afrika.

126. **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama kuhakikisha utambuzi na maadhimisho makubwa ya Wiki ya Lugha za Afrika barani Afrika kupitia ushirikiano na wadau muhimu ili kuhakikisha ufadhili wa kutosha na kuhamasisha umma kwa kuzingatia vijana na taasisi za elimu.

### (7) KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI ZA KITUO CHA TAALUMA ZA LUGHA NA HISTORIA KUPITIA FASIHI SIIMULIZI (CELHTO) NA MSWADA WA SHERIA

127. **LINAIDHINISHA** Rasimu ya Sheria ya Kituo cha Taaluma za Lugha na Historia kwa kutumia fasihi Simulizi (CELHTO), **LINAIAGIZA** Kamisheni kuwasilisha rasimu ya

hati ya kisheria kwa STC kuhusu Haki na Masuala ya Kisheria kwa ajili ya kujadiliwa.

**128.** **LINAAGIZA** CELHTO kuendelea kukuza na kuhifadhi mila simulizi na usimulizi wa hadithi za Kiafrika ili kukuza utambulisho wa Kiafrika na kuiwezesha Afrika kuchukua jukumu na kuandika historia yake halisi.

### (8) KUHUSU AZIMIO LA KWADUDUKUZA LA MAWAZIRI WA UTAMADUNI WA G2O

**129.** **LINAIDHINISHA** Azimio la KwaDukuza la Mawaziri wa Utamaduni wa G20 kwa ajili ya utekelezaji wa Nchi Wanachama wa AU.

**130.** **LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kupitisha mifumo ya kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa Azimio hilo kupitia matokeo ya muda mfupi, wa kati na mrefu kwa ushirikiano na Wanachama wa G20 na Taasisi za Utamaduni za Afrika.

### (9) KUHUSU NYARAKA YA MATOKEO MJADALA HURU WA MAWAZIRI KUHUSU SAUTI NA FILAMU ILIYOANDALIWA NA BENKI YA AFREXIM KWA USHIRIKIANO NA ALGERIA NA KAMISHENI YA UMOJA WA AFRIKA (AUC/KAMISHENI)

**131.** **LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kuimarisha sera za kitaifa na kikanda zinazoweka Sekta za Utamaduni na Ubunifu (CCIs) ndani ya mipango ya maendeleo ya kiuchumi ya kikanda.

**132.** **LINAZIOMBA PIA** Nchi Wanachama kuharakisha mchakato wa kuthibitisha Sheria ya Tume ya Sauti na Filamu ya Afrika (AACC) ili kuhakikisha inaanza kutumika haraka na kwa wakati unaofaa kufanikisha uendeshaji kamili wa wakala maalumu.

**133.** **LINAZITAKA** taasisi za fedha kuongeza uwekezaji na fursa za kifedha kwa wasanii na mashirika ya ubunifu.

**134.** **AIDHA LINAZITAKA** Nchi Wanachama wa AU na Nchi za Karibe kuongeza utangazaji wa bidhaa na huduma za kiutamaduni za Afrika na Karibe katika masoko ya kikanda na kimataifa, na kuboresha mifumo ya data na utafiti ili kusaidia uundaji wa sera za CCIs zinazotegemea ushahidi

### (10) KUHUSU RIPOTI YA MWANGALIZI WA MASUALA YA SERA ZA UTAMADUNI BARANI AFRIKA (OCPA)

**135.** **LINAOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Kituo cha Kuchunguza Sera za Utamaduni barani Afrika (OCPA) kurasimisha uhusiano kati ya taasisi hizo mbili kupitia Mkataba wa Maridhiano (MoU).

136. **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama Kuimarisha Umoja wa Afrika/UNESCO/Kituo cha Kuchunguza Sera za Utamaduni barani Afrika (OCPA) ambacho tayari kipo.

137. **LINAZIOMBA ZAIDI** Nchi Wanachama kuunga mkono mpango wa Moroko wa kuwa mwenyeji wa ofisi ya Miji Mikuu ya Utamaduni ya Afrika kama sehemu ya utekelezaji wa Ajenda 2063 ya AU.

### (11) KUHUSU RIPOTI YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MFUKO WA URITHI WA DUNIA WA AFRIKA (AWHF)

138. **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama wa AU kuendelea kuunga mkono kazi ya Mfuko wa Urithi wa Dunia wa Afrika (AWHF) kwa ajili ya kuongeza ukuzaji, ulinzi na utambuzi wa urithi tajiri wa kitamaduni na asili wa Afrika.

139. **LINATOA WITO ZAIDI KWA** Nchi Wanachama kuimarisha utetezi na ushiriki wa Sekta Binafsi kwa ajili ya uwekezaji endelevu katika programu za urithi.

140. **LINAALIKA** Nchi Wanachama kushiriki katika Tukio la Utetezi la Ngazi ya Juu la Mfuko wa Urithi wa Dunia wa Afrika kusherehekea Maadhimisho yake ya Ishirini (20), lililoandaliwa na Mhe. José Maria Neves, Rais wa Jamhuri ya Cabo Verde na Kiongozi wa AU wa masula ya Urithi wa Kiutamaduni na Urithi wa Asili, litakalofanyika mjini Addis Ababa, Ethiopia, mnamo Februari 2026 sambamba na Mkutano Mkuu wa 39 wa AU.

### (12) KUHUSU MPANGO WA PAMOJA WA KUKUZA KAZI ZA STAHA KATIKA SEKTA YA UTAMADUNI NA UBUNIFU BARANI AFRIKA (CREATE)

141. **LINAIDHINISHA** mpango wa CREATE kama mpango wa bara unaoendana na Ajenda 2063 ya AU na Mpango wa Utekelezaji wa AU uliorekebishwa kuhusu Sekta za Utamaduni na Ubunifu.

142. **LINAOMBA** Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Wabia kuunga mkono Utekelezaji wa mpango wa CREATE katika ngazi za kikanda na kitaifa.

143. **LINAIAGIZA** Kamisheni, ILO na UNESCO kuratibu, kufuatilia na kuripoti maendeleo ya utekelezaji wa CREATE kwa STC-YCS (VI).

### (13) KUHUSU RIPOTI YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SELAM

144. **LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kushirikiana na SELAM kupanua utafiti katika Sekta za Utamaduni na Ubunifu.

145. **AIDHA LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kuharakisha utekelezaji wa uamuzi Assembly/AU/Dec.772(XXXIII) wa kutenga angalau asilimia moja (1%) ya bajeti za

kitaifa katika sanaa, utamaduni na urithi kufikia mwaka 2030, kwa mujibu wa mradi wa *Selam's Connect for Culture Africa (CfCA).*

**146. LINATOA WITO** kwa SELAM na Kamisheni kuandaa mpango wa pamoja wa utekelezaji na ufuatiliaji wa MoU yao.

**(14) KUHUSU MRADI WA FILAMU WA AMBIKA AFRIKA (AAFP) – KUIMARISHA UUNGANISHAJI WA FILAMU ZA AFRIKA NA KUTIMIZA AJENDA MWAKA 2063 YA UMOJA WA AFRIKA**

**147. LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kuimarisha simulizi ya Kiafrika, kukuza vipaji vya watengeneza filamu wa Afrika kwa kuwajengea uwezo, uzalishaji na usambazaji wa filamu za Afrika.

**148. PIA LINAIOMBA** AUC kushirikiana na AAFP kuhimiza uridhiaji wa Sheria ya Tume ya Sauti na Picha na Sinema ya Afrika (*African Audio-Visual and Cinema Commission*) (AACC).

(15) **KUHUSU UANZISHWAJI WA KITUO CHA URITHI WA UHURU WA AFRIKA (ALHC) KAMA WAKALA MAALUM WA UMOJA WA AFRIKA**

**149. LINAIDHINISHA** Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika (ALHC) kama Wakala Maalum wa AU.

**150. LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama vyombo vya kanda, na wabia wa kimataifa kutoa msaada kwa mpango huu, kwa kutambua umuhimu wake katika kuhifadhi urithi wa ukombozi wa Afrika kwa ajili ya vizazi vijavyo na kuunganisha urithi wa ukombozi katika sera za kitaifa za elimu na utamaduni.

**(16) KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI ZA CHAMA CHA WAANDISHI WA AFRIKA (PAWA)**

**151. LINAOMBA** Nchi Wanachama, taasisi za kiutamaduni za Afrika, kuunga mkono kazi ya Chama cha Waandishi wa Afrika (PAWA).

**152. LINAHIMIZA** Kamisheni, ACALAN, CELHTO, GMA, AACC kuimarisha ushirikiano wao na PAWA kwa ajili ya kukuza fasihi na usomaji.

<u>**KUHUSU MICHEZO**</u>

**(1) KUHUSU RIPOTI YA UTEKELEZAJI WA MAAMUZI YA KAMATI YA KUDUMU YA KITAALAMU YA VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO) KATIKA SEKTA YA MICHEZO**

**153. LINALIOMBA** Baraza la Michezo la AU kutekeleza mkakati thabiti wa mawasiliano ili kuongeza mafanikio katika michezo ya Afrika na Michezo kwa ajili ya Maendeleo.

154. **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama zenye madeni yasiyolipwa kwa Baraza Kuu la Michezo barani Afrika lililovunjwa kutimiza ahadi zao na kufanya malipo kabla ya toleo lijalo la Michezo ya Afrika mwaka 2027

**(2) KUHUSU KUJADILI RIPOTI YA BODI YA USHAURI YA BARAZA LA MICHEZO LA UMOJA WA AFRIKA**

155. **LINAAGIZA** Baraza la Michezo la AU kuunda kamati ya kitaalamu ya kuchanganua Sheria ya Baraza la Michezo la AU, kubaini mapengo yanayoleta changamoto kwenye utekelezaji na kupendekeza marekebisho kulingana na Ibara ya 32 ya Sheria ya Baraza la Michezo la AU

156. **LINAIOMBA** STC-YCS (V) kuidhinisha wajumbe wapya wa Kamati ya Kitaalamu ya Fedha na Kamati ya Kitaalamu ya Michezo ya Afrika, kwa mujibu wa Ibara ya 10 (f) ya Katiba ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika

157. **LINAZIOMBA PIA** Nchi Wanachama zote kushiriki kikamilifu katika shughuli za Kanda za Maendeleo ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika, na kuhimiza Nchi Wanachama kuzingatia kuwa na watumishi wenye uwezo katika Sekretarieti za Kikanda ili kuunga mkono shughuli za uendeshaji na utekelezaji wa programu.

158. **LINAPENDEKEZA** kufungua tena zabuni ya kuandaa Michezo ya Afrika ya 2027 kwa kuzingatia ucheleweshaji wa kusaini Mkataba wa Itifaki ya Mwenyeji kati ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na AU ikiwa hautasainiwa ifikapo tarehe 28 Februari 2026.

159. **LINAPENDEKEZA ZAIDI** kufungua tena zabuni ya kuandaa Michezo ya Afrika ikiwa nchi mwenyeji itashindwa kuzingatia Ibara ya 18 ya Sheria ya Baraza la Michezo la AU ambayo iliidhinishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali mnamo 2016.

160. **LINAIOMBA ZAIDI** Kamisheni kuitisha *Indaba* (kongamano) unaowashirikisha wadau wote wa Michezo ya Afrika kwa madhumuni ya kufafanua kwa uwazi na kuoanisha majukumu na wajibu wa wadau.

161. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama kutoshiriki katika Tukio lolote la Michezo ya Afrika lililofanyika kinyume na Sheria ya Baraza la Michezo la AU ambayo iliidhinishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na linapendekeza zaidi kutengwa kwa nchi yoyote inayokiuka Sheria ya Baraza la Michezo la AU na Mkataba wa Nchi Mwenyeji wa Michezo ya Afrika kushiriki katika tukio lijalo la Michezo ya Afrika baada ya ukiukwaji huo kufanywa.

162. **LINAZIAGIZA** Nchi Wanachama kuzingatia mzunguko wa kuandaa Michezo ya Afrika kulingana na mfumo wa kijiografia wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha fursa sawa za uandaaji katika Kanda zote kwa manufaa ya wanariadha. Katika mazingira ambapo Ukanda hauwezi kupata nchi mwenyeji, mchakato wa zabuni utafunguliwa

kwa Nchi zote Wanachama. Mfumo huu wa mzunguko utaanza kutumika kuanzia Michezo ya Afrika ya 2035 na kuendelea.

163. **LINAIDHINISHA** Mpango Mkakati wa AUSC na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa kipindi cha 2024-2028.

**(3) KUHUSU KUJADILI KANUNI ZA MSINGI ZA MICHEZO YA AFRIKA ZILIZOFANYIWA MAPITIO**

164. **LINAPENDEKEZA** kwamba Nchi Wanachama ziwasilishe maoni zaidi kuhusu marekebisho yaliyopendekezwa ya rasimu ya Kanuni za Msingi za Michezo ya Afrika kupitia Kanda za Maendeleo za Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika ifikapo tarehe 31 Januari 2026.

165. **LINAIAGIZA** Kamati ya Kitaalamu ya Michezo ya Afrika kukamilisha Rasimu ya Kanuni za Msingi na kuwasilisha katika Kikao Maalum cha STC-YCSV kupitia Bodi ya Ushauri ya Michezo.

166. **LINAIAGIZA PIA** Kamisheni kuandaa Mkutano Maalum wa STC-YCS V mapema mwaka 2026 ili kujadili na kuidhinisha rasimu ya Kanuni za Msingi za Michezo ya Afrika.

**(4) KUHUSU MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KUSISIMUA MISULI NA UZINGATIAJI WA KANUNI ZA WADA**

167. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kufungamanisha hati za kisheria za kitaifa ikiwamo sheria, sera, kanuni na Hati ya Dunia iliyorekebishwa ya 2027 ya Kupinga Matumizi ya Dawa za Kusisimua Misuli Michezoni na Viwango vya Kimataifa, kwa kushauriana na WADA.

168. **LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kuunga mkono maandalizi ya Kongamano la Kikanda la Afrika la Kupambana na dawa za kusisimua misuli la mwaka 2026, kwa lengo la kutoa jukwaa kwa mamlaka za umma za Afrika, harakati za michezo za Afrika, Mashirika ya Kitaifa na Kikanda ya Kupambana na dawa za kusisimua misuli, wanamichezo na wadau wengine kujadili mikakati ya kusaidia wadau katika utekelezaji wa Kanuni Iliyofanyiwa Marekebisho.

169. **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba michango yote kwa WADA inalipwa, ikiwa ni pamoja na madeni ya miaka iliyopita.

170. **LINAIDHINISHA** uteuzi wa Gambia kuchukua nafasi ya Ghana kwa kipindi cha 2028-2031.

171. **LINATAMBUA,** kwa shukrani, ofa ya Jamhuri ya Kiarabu ya Misri ya kuwa mwenyeji wa Kongamano la Kikanda la Afrika la Kupambana na Dawa za

kusisimua misuli la mwaka 2026, litakalofanyika Cairo, Misri, kuanzia tarehe 27–29 Aprili 2026, na inawahimiza wadau wote husika wa Afrika kuunga mkono tukio hilo.

**(5) KUHUSU SHULE ZA MICHEZO ZILIZOANZISHWA NA FIFA**

**172. LINAZITAKA** Nchi Wanachama za Au kuimarisha ushirikiano na FIFA na Vyama vya Wanachama katika utekelezaji wa awamu ya pili ya mipango ya Soka kwa Shule na Uwanja wa FIFA, ili kuhakikisha mipango iliyoratibiwa, utekelezaji mzuri, na uendelevu wa muda mrefu. Mipango hii inalenga kupanua ufikiaji wa soka, kuongeza ushiriki, njia za kufundisha, utambuzi wa vipaji, na kutumia soka kama chombo cha maendeleo ya kijamii na kielimu.

**(6) KUHUSIANA NA MISHENI NA. 89: ULINZI WA MUSTAKABALI WA MICHEZO YA AFRIKA – MAPAMBANO DHIDI YA USAFIRISHAJI/BIASHARA HARAMU YA MICHEZO BARANI AFRIKA**

**173. LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kuandaa sera zinazoshughulikia usafirishaji haramu wa wanamichezo na kuweka kipaumbele ulinzi katika programu zote za michezo ya vijana ikiwa ni pamoja na adhabu kwa vyuo vya michezo na mawakala wa michezo wanaowezesha usafirishaji haramu wa wanamichezo.

(7) **KUHUSU RIPOTI YA MJADALA HURU WA WATUNGA SERA NA WADAU: MICHEZO KAMA KICHOCHEO CHA MAENDELEO YA AFRIKA – KUWIANISHA SERA, DIRA, UWEKEZAJI NA UTEKELEZAJI**

**174. LINAZISIHI** Nchi Wanachama kushirikiana na Jukwaa la *SportBiz Africa Platform* ili kufungamanisha maendeleo ya michezo na matarajio ya Ajenda 2063 ya AU, fursa za AfCFTA, kutafuta rasilimali za ndani na za kimataifa.

**175. LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kushiriki kikamilifu katika Michezo ya 4 ya Olimpiki ya Vijana ya Majira ya Joto, itakayofanyika kwa mara ya kwanza Barani Afrika mjini Dakar, Senegal, kuanzia tarehe 31 Oktoba hadi 14 Novemba 2026.

**(E) KUHUSU MKUTANO WA KAWAIDA WA KUMI NA MOJA (11) WA STC YA MASUALA YA HAKI NA KISHERIA – EX.CL/**

**176. LINAZINGATIA** Ripoti na Mapendekezo ya Mkutano wa Kawaida wa 11 wa Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Masuala ya Haki na Kisheria uliofanyika Tarehe 08 hadi 17 Desemba 2025 huko Nairobi, Jamhuri ya Kenya.

**177. LINAPITISHA** Rasimu ya Nyaraka zifuatazo za Kisheria:

(i) Rasimu ya Sheria ya Mfano ya Uhamishaji Madeni
(ii) Rasimu ya Sheria ya Mfano ya Kanuni za Bidhaa za Tiba

**178. LINAAMUA** kupendekeza Rasimu ya Nyaraka za Kisheria zifuatazo kwa ajili ya kujadiliwa na kupitisha na Wakuu wa Nchi na Serikali:

i. Rasimu ya Sheria ya Taasisi ya Fedha ya Afrika[1]

ii. Rasimu ya Marekebisho ya Sheria ya Baraza la Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni la Umoja wa Afrika.

iii. Rasimu ya Viambatisho vya Itifaki ya Makubaliano ya Kuanzisha Eneo Huru la Biashara Afrika Kuhusu Haki za Miliki ya Ubunifu;
   a. Kiambatisho kuhusu Aina za Matumizi
   b. Kiambatisho kuhusu Maarifa ya Jadi, Utamaduni wa Jadi na Rasilimali za Kijenetiki
   c. Kiambatisho kuhusu Ulinzi wa Aina za Mimea
   d. Kiambatisho kuhusu Hataza
   e. Kiambatisho kuhusu Alama
   f. Kiambatisho kuhusu Ubunifu Viwandani
   g. Kiambatisho kuhusu Alama za Kijiografia
   h. Kiambatisho kuhusu Hakimiliki na Haki Zinazohusiana

**179.** **LINAIOMBA** Kamisheni kufanyia kazi upya rasimu ya hati ya kisheria ya Mfuko wa Afrika na nchi za Kiarabu kabla ya kuwasilishwa tena kwa Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Kilimo, Maendeleo ya Vijijini, Maji na Mazingira (STC-ARDWE).

**180.** **LINAAMUA** kuomba idara zinazohusika za Kamisheni na ECOSOCC kufanya utafiti juu ya ufafanuzi upya wa neno “Diaspora” na kuwasilisha matokeo yake kwa Baraza Kuu kwa ajili ya kujadiliwa.

## (F) KUHUSU MKUTANO WA KAWAIDA WA SITA (6) WA KAMATI MAALUMU YA KITAALAMU YA KILIMO, MAENDELEO YA VIJIJINI, MAJI NA MAZINGIRA (STC-ARDWE)

**181.** **LIKIKUMBUKA** maamuzi Assembly/AU/Dec.227 (XII) na Assembly/AU/Dec.365 (XVII) yaliyoanzisha Kamati Maalumu za Kitaalamu kama Vyombo vya Umoja wa Afrika, kwa mujibu wa Ibara ya 5(1)(g) ya Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika;

**182.** **LIKIKUMBUKA ZAIDI** Azimio la Kampala la CAADP lililopitishwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika mwezi Januari 2025, pamoja na mamlaka ya STC-ARDWE ya kuongoza sera za mageuzi ya kilimo, maendeleo ya vijijini, maji, mazingira na uchumi wa buluu;

**183.** **LINAAMUA:**

(i) **KUPITISHA** Ripoti ya Mawaziri ya Mkutano wa Kawaida wa Sita wa STC-ARDWE, pamoja na mapendekezo ya Mkutano wa Wataalamu.

[1] Reservation entered by the Republic of South Africa and the Arab Republic of Egypt on Article 30.

(ii) **KUIDHINISHA** Ripoti ya Tano ya Tathmini ya Kila Miaka Miwili ya CAADP na **KUPENDEKEZ**A iwasilishwe katika Mkutano wa Kawaida waThelathini na Tisa (39) wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tarehe 14–15 Februari 2026, kwa ajili ya kupitishwa.

(iii) **KUIDHINISHA** Miongozo ya Utekelezaji wa Mkakati wa Mpango Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa CAADP wa Kampala (2026–2036).

(iv) **KUIDHINISHA** CAADP kama Mpango Mkuu wa Ajenda ya Mwaka 2063, kwa kuzingatia mchango wake uliothibitishwa katika mageuzi ya kilimo, usalama wa chakula na ukuaji wa uchumi jumuishi barani Afrika.

(v) **KUIDHINISHA** utekelezaji wa Vipaumbele vya Siku 100 vya Kamishna kuhusu Usalama wa Chakula Barani Afrika na **KURIDHIA** kuanzishwa kwa Kamati ya Uongozi ya Bara inayoongozwa na AUC-DARBE.

(vi) **KUIDHINISHA** Mpango Mkakati wa Kufufua Kituo cha Maendeleo ya Mbolea cha Afrika kilichopo Harare, Zimbabwe, na **KUZIHIMIZA** Nchi Wanachama kusaini, kuthibitisha na kuwasilisha hati husika.

(vii) **KUIDHINISHA** Miongozo ya Kuharakisha Fursa za Sekta ya Umma katika Ufadhili wa Mifumo ya Chakula na Kilimo.

(viii) **KUIDHINISHA** Mikakati ya Afrika ya kutokomeza kichaa cha mbwa kinachosambazwa na mbwa na ugonjwa wa traipanosomiasisi kwa kipindi cha 2026–2035.

(ix) **KUIDHINISHA** Mfumo wa Sera kwa Sekta Ndogo za Malisho na Chakula cha Mifugo Barani Afrika na kuanzishwa kwa *Dairy Africa Alliance*, na **KUOMBA** uungaji mkono kwa ajili ya uuingizaji katika mifumo ya Nchi Wanachama na utekelezaji.

(x) **KUIDHINISHA** Miongozo ya Uendeshaji Iliyofanyiwa Marekebisho ya Jukwaa la Ushirikiano wa Mbegu na Bayoteknolojia la Afrika (ASBPP), pamoja na kuhamishwa kwa Sekretarieti ya ASBPP kutoka Jukwaa la Utafiti wa Kilimo Barani Afrika (FARA) kwenda AUDA-NEPAD; na kuimarisha Vikosikazi vya Kimaeneo.

(xi) **KUAGIZA** kuitishwa kwa Mkutano Maalumu wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Mifumo ya Mbegu na Bayoteknolojia kwa mwaka 2026.

(xii) **KUIDHINISHA** Mfumo wa Sera, Mkakati na Mpango wa Hatua wa Mifumo ya Mbegu Inayosimamiwa na Wakulima (2026–2035), unaoendana na kanuni za Upatikanaji na Ugawaji wa Manufaa ya pamoja na Ibara ya 9 ya Mkataba wa Kimataifa wa Rasilimali za Mimea na Jenetiki kwa Chakula na Kilimo.

(xiii) **KUPITISHA** Mfumo wa Bara wa Uchambuzi wa Mandhari ya Urekebishaji wa Jeni

(xiv) **KUIDHINISHA** marekebisho ya Sheria Kielelezo ya Umoja wa Afrika kuhusu Usalamabio, pamoja na Miongozo ya AU kuhusu Bayoteknolojia kwa ajili ya Chakula na Kilimo.

(xv) **KUUNGA MKONO** uhuishaji na utekelezaji wa miongozo inayowiana na viwango vya vihatarishi.

(xvi) **KUIDHINISHA** kuanzishwa kwa Hifadhi/Benki tano (5) za Mbegu/Jeni za Kikanda kama Vituo vya Umahiri, kwa mwenyeji mmoja katika kila kanda.

(xvii) **KUIDHINISHA** vielelezo vya nyaraka za kisheria kuhusu Upatikanaji na Mgawanyo wa Manufaa, ikijumuisha masharti ya uhamishaji, usimamizi wa Taarifa za Mfuatano wa Kidijitali (Digital Sequence Information), pamoja na kanuni za upande wa tatu.

(xviii) **KUIDHINISHA** rasimu ya msimamo wa pamoja wa Afrika kuhusu ITPGRFA na **KUUNGA MKONO** ushiriki wa wanamajadiliano watano katika majukwaa mbalimbali.

(xix) **KUIDHINISHA** Mfumo wa Sera, Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Viashiria vya Kijiografia (2026–2035).

(xx) **KUIDHINISHA** Mpango wa Afrika wa Kuokoa Bioanuwai ya Mboga (2025–2035).

(xxi) **KUIDHINISH**A Azimio la Addis Ababa lililotokana na Mkutano wa Pili wa Afrika kuhusu Tabianchi na **KUIAGIZA** Kamisheni kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Utoaji wa Taarifa.

(xxii) **KUIDHINISHA** Dira na Sera ya Maji ya Afrika ya mwaka 2063 na **KUPENDEKEZA** kupitishwa kwake na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kama Msimamo wa Pamoja wa Afrika katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Maji wa mwaka 2026.

(xxiii) **KUOMBA** AMCOW, Kamisheni, AfDB, AWF, na UNECA kuandaa Mpango wa Kwanza wa Utekelezaji (2026–2033) na kuitisha mkutano wa kimataifa wa kushughulikia upatikanaji wa fedha wa mwaka 2026.

(xxiv) **KUAGIZA** Kamisheni kujumuisha maamuzi yaliyopitishwa ndani ya mifumo ya kikanda, kuhakikisha utafutaji wa rasilimali, na kuripoti maendeleo ya utekelezaji katika Mkutano wa Saba wa STC-ARDWE.

(xxv) **KUZIOMBA** Nchi Wanachama, RECs, AUDA-NEPAD, na washirika kuunga mkono utekelezaji wa kikamilifu wa mifumo iliyopitishwa.

(xxvi) **KUIOMBA** Kamisheni kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji, tathmini, na uwajibikaji, na kuwasilisha ripoti za maendeleo zilizounganishwa kwa Baraza la Utekelezaji.

## (G) KUHUSU RIPOTI MKUTANO WA KAWAIDA WA KUMI NA SABA (17) WA KAMATI MAALUMU YA KITAALAMU (STC) YA ULINZI, USALAMA NA HUDUMA ZA USALAMA (STCDSS)

**184.** **LINAKARIBISHA** ripoti iliyopitishwa na Mkutano wa Kawaida wa Kumi na Saba (17) wa Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Ulinzi, Usalama na Huduma za Usalama (STCDSS) uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, kuanzia tarehe 8 hadi 11 Desemba 2025, na **LINAIDHINISHA** mapendekezo yaliyojumuishwa ndani yake;

**185.** **LINAIDHINISHA PIA** Wazo la Umoja wa Afrika kuhusu Amri, Udhibiti, Mawasiliano na Mifumo ya Taarifa kwa Jeshi la Dharura Afrika na Operesheni za Kusaidia Amani, pamoja na Sera kuhusu Hatua za Marekebisho kwa Waathirika wa Vitendo Viovu na Madhara katika Operesheni za Kusaidia Amani za Umoja wa Afrika, vilivyopitishwa na Mkutano wa Kawaida wa 17 wa STCDSS;

186. **LINAIDHINISHA ZAIDI** ripoti ya Mapitio ya Kimkakati ya Jeshi la Dharura la Afrika iliyopitishwa na Mkutano wa Kawaida wa 17 wa STCDSS na LINAIOMBA Kamisheni kupanua na kuharakisha majadiliano jumuishi na Nchi Wanachama wa AU, Vitengo vya Mipango vya RECs/RMs (PLANELMs) na vyombo vyake husika vya sera, pamoja na Vyombo husika vya Sera vya AU, ili kutekeleza matokeo ya Mapitio ya Kimkakati ya Jeshi la Dharura la Afrika.

187. **LINAKUMBUKA** uamuzi Assembly/AU/Dec.918(XXXVIII) wa Februari 2025 kuhusu umuhimu wa kukamilisha Rasimu ya Makubaliano kati ya AU na RECs na RMs kuhusu Matumizi ya Jeshi la Dharura la Afrika, kukamilishwa katika Mkutano wa Kawaida wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mwezi Februari 2026, na **LINAOMBA** kupitishwa kwa Rasimu ya Makubaliano pamoja na Ripoti ya Mapitio ya Kimkakati ya Jeshi la Dharura la Afrika.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI ZA KAMISHENI JUU YA MASUALA YA KIBINADAMU NA USAFIRI HURU WA WATU BARANI AFRIKA
## Doc. EX.CL/1655(XLVIII)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamisheni kuhusu Hali ya Kibinadamu barani Afrika kwa kipindi cha Januari-Desemba 2025, na **LINAPONGEZA** Kamisheni kwa uchambuzi wa kina na tathmini za nyanjani zilizofanywa katika Nchi Wanachama zilizoathiriwa.

2. **LINAELEZA WASIWASI WA KINA** kuhusu hali ya kibinadamu kuzidi kuwa mbaya barani kote, huku zaidi ya watu milioni 160 wakihitaji msaada, ikiwa ni pamoja na watu milioni 45 waliolazimika kupoteza makazi yao, kwa sababu za migogoro ya kutumia silaha, misukosuko ya tabianchi, uhaba wa chakula, na udhaifu wa kiuchumi.

3. **LINAELEZA ZAIDI WASIWASI** kuhusu janga la kibinadamu nchini Sudan, ambalo kwa sasa ni janga kubwa zaidi duniani la kuhama kwa watu likiwa na watu milioni kumi na mbili (12) waliopoteza makazi yao, na Mashariki mwa DRC, ambako kuibuka tena kwa migogoro kunaweka maisha ya mamilioni hatarini, na athari kubwa kwa nchi jirani.

4. **LINALAANI** kuendelea kwa ukiukwaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu (IHL) na Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu (IHRL), ikiwa ni pamoja na mashambulizi dhidi ya raia, unyanyasaji wa kijinsia unaohusiana na migogoro, kuzuiwa kwa ufikiaji wa msaada wa kibinadamu, na kuwalenga kimakusudi wafanyakazi wa misaada, ikibainisha ongezeko la 20% la mashambulizi dhidi ya wafanyakazi wa kibinadamu kwa mwaka 2025.

5. **LINATAMBUA** athari kubwa ya majanga yanayosababishwa na tabianchi—ikiwa ni pamoja na ukame, mafuriko, vimbunga, na matukio mabaya ya hali ya hewa—ambayo yamewaacha zaidi ya Waafrika milioni mia moja na ishirini (120) wakikabiliwa na uhaba wa chakula unaotokana na mgogoro au ulio mbaya, hasa katika Pembe ya Afrika, Sahel, na Ukanda wa Kusini mwa Afrika.

6. **LINATAMBUA** mzigo mzito unaobebwa na nchi zinazowahifadhi wakimbizi, na **LINATOA WITO WA** kuwa na ushirikiano bora wa majukumu ya kimataifa na ufadhili unaotabirika kwa jamii wenyeji na nchi wenyeji.

7. **LINAZINGATIA** ripoti kuhusu hali ya kibinadamu Afrika Magharibi, hasa nchini Nigeria ambapo watu milioni 8.1 wanahitaji msaada wa kibinadamu, na **KUSISITIZA** hitaji la dharura la ujumbe wa tathmini ya msaada wa kibinadamu nchini Nigeria, kwa lengo la kutoa msaada kwa watu/jamii zilizoathiriwa.

**Kuhusu Mwitikio na Uratibu wa Kitaasisi wa AU**

8. **LINAPONGEZA** Kamisheni na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi, Wanaorejea makwao na IDPs, kwa misheni za tathmini ya msaada wa kibinadamu zilizofanywa nchini Burundi, Msumbiji, Sudan Kusini, na Sudan, na kwa utoaji wa misaada ya msingi kwa watu walioathiriwa.

9. **LINAIOMBA** Kamisheni kuharakisha mchakato wa utoaji wa fedha za mshikamano zilizolimbikizwa na **LINAPENDEKEZA** Kamisheni kurekodi mafanikio yaliyopatikana kutokana na fedha zilizotolewa na kuripoti ipasavyo.

10. **LINAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana kuelekea uendeshaji wa Shirika la Masuala ya Kibinadamu la Afrika (AfHA) na **LINAIAGIZA** Kamisheni na Kamati Ndogo husika za PRC kuharakisha uanzishwaji wa mifumo yake ya uendeshaji, fedha, na uratibu kulingana na Azimio la Malabo (2022).

11. **LINAIOMBA PIA** Kamisheni kuimarisha uratibu na RECs, RMs, mashirika ya Umoja wa Mataifa, na wabia wa msaada wa kibinadamu ili kuhakikisha miitikio thabiti na inayoongozwa na Waafrika, hasa katika hali za uhamaji kinguvu wa kuvuka mipaka ya nchi.

12. **LINAIAGIZA PIA** Kamisheni kuboresha uhusiano wa tahadhari za mapema-utekelezaji wa mapema kati ya AfHA, Africa CDC, *Africa Risk Capacity (ARC),* Uwezo wa Raia wa Bara la Afrika wa Kukabiliana na Majanga, Mfumo wa Tahadhari ya Mapema wa Bara la Afrika (CEWS), na taasisi za kitaifa za usimamizi wa majanga.

**Kuhusu Ufadhili wa Msaada wa Kibinadamu**

13. **LINAZINGATIA KWA WASIWASI ufadhili usiotosha** wa Mipango ya Mwitikio wa Kibinadamu (HRPs), huku chini ya asilimia 45 ya dola za Marekani bilioni 11 zinazohitajika kwa mwaka 2025 zikitolewa kama ufadhili, na L**INATOA WITO KWA** Nchi Wanachama, wabia, na sekta binafsi kuongeza ufadhili wa kibinadamu unaotabirika na endelevu.

14. **LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama zilizotimiza ahadi zilizotolewa wakati wa Mkutano Maalum wa masuala ya Kibinadamu wa Malabo wa 2022 na Mkutano wa Kuahidi, **LINAZISIHI** Nchi Wanachama ambazo bado hazijatimiza ahadi hizo kufanya hivyo bila kuchelewa.

15. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuandaa mifumo muhimu ya matumizi ya fedha zilizopo zilizotolewa kwa ajili ya msaada wa kibinadamu barani Afrika, na kwa ajili ya uendeshaji wa Shirika la Kibinadamu la Afrika (AfHA).

16. **LINAIOMBA** Kamisheni kushirikiana na wadau husika na kuchunguza mifumo bunifu ya ufadhili, ikiwa ni pamoja na kuunganisha hatari, bima ya tabianchi, na vyombo vya ufadhili wa kibinadamu vinavyoongozwa na Afrika.

**Kuhusu Ulinzi wa Raia na Vikwazo vya Ufikiaji**

17. **LINALAANI VIKALI** aina zote za ukatili dhidi ya raia, wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu na mali zao, ikiwa ni pamoja na ukatili wa kijinsia unaohusiana na migogoro, uhamaji wa kulazimishwa, na mashambulizi kwenye shule, hospitali, na miundombinu mingine ya raia.

18. **LINATOA WITO** kwa pande zote zilizo katika migogoro ya kutumia silaha kuheshimu IHL, kuhakikisha ufikiaji salama na usiozuiliwa wa msaada wa kibinadamu, na kulinda wafanyakazi na mali za msaada wa kibinadamu.

19. **LINAOMBA** Kamisheni kuongeza juhudi za kidiplomasia za kibinadamu, ikiwa ni pamoja na kupitia Baraza la Amani na Usalama la AU (PSC), kushughulikia vikwazo vya ufikiaji katika Sudan, Mashariki mwa DRC, Sahel, kaskazini mwa Msumbiji, na maeneo mengine yaliyoathiriwa.

**Kuhusu Tabianchi, Uwepo wa Chakula, na Ustahimilivu**

20. **LINAELEZA WASIWASI MKUBWA** kuhusu uhaba wa chakula unaozidi kuwa mbaya barani Afrika, hasa katika Pembe ya Afrika, Sahel, na Kusini mwa Afrika, na **LINATOA WITO** wa kuongeza uwekezaji katika kukabiliana na tabianchi, hatua za tahadhari, na mifumo ya chakula inayostahimili.

21. **LINAIOMBA** Kamisheni, kwa ushirikiano na wadau wote husika, kuzisaidia Nchi Wanachama katika kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema, usimamizi wa hatari za tabianchi, na mipango ya ustahimilivu inayotegemea jamii.

**Kuhusu Upotezaji Makazi na Masuluhisho ya Kudumu**

22. **LINATOA WITO kwa** Nchi Wanachama kutekeleza Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Ulinzi na Msaada wa Watu Waliopoteza Makazi Nchini Mwao (2009), Mkataba Unaosimamia Vipengele Maalum vya Matatizo ya Wakimbizi Barani Afrika (1969), na Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Vipengele Maalum vya Haki ya Uraia na Utokomezaji wa Hali ya Kukosa Uraia Barani Afrika (2024), na kuunganisha masuluhisho ya kudumu katika mipango ya maendeleo ya kitaifa na **LINAIOMBA** Kamisheni kuziunga mkono Nchi Wanachama katika utekelezaji wa Mikataba ya AU iliyotajwa hapo juu, na kuunganisha masuluhisho ya kudumu katika mipango ya maendeleo ya kitaifa.

23. **LINAMPONGEZA** Mheshimiwa Teodoro Obiang Nguema Mbasogo, Rais wa Jamhuri ya Equatorial Guinea, Kiongozi wa Mada ya Mwaka ya 2019 kwa juhudi zake thabiti katika AU za kushughulikia changamoto za upotezaji wa makazi wa lazima na **LINAUOMBA** Mkutano Mkuu kumteua kama Mtetezi wa Umoja wa

Afrika katika kukabiliana na masuala ya kibinadamu na ulinzi wa watu walio katika hatari;

24. **LINAIPONGEZA** Burundi kwa kuwa mwenyeji wa zaidi ya Wakongo 177 000 katika ardhi yake;

**Kuhusu Afua za Kibinadamu kwa Nchi Wanachama Waliosimamishwa kupitia Shughuli za AU za Utoaji msaada wa Kibinadamu na za Afya**

25. **LINAZINGATIA** shughuli zilizopendekezwa na Kamisheni za kusaidia Nchi Wanachama zilizosimamishwa kutokana na Mabadiliko ya Serikali yaliyo Kinyume cha Katiba ambazo zinapitia majanga ya kibinadamu yanayozidi kuwa mbaya.

26. **LINAKUMBUKA** Mifumo ya Kisheria ya AU kuhusu Mabadiliko ya Serikali Kinyume cha Katiba, ambayo inasisitiza haja ya kuhakikisha kwamba raia wa kawaida katika Nchi Wanachama zilizosimamishwa hawateseki kupita kiasi kutokana na kutekeleza vikwazo hivyo.

27. **LINAKUMBUKA ZAIDI** Azimio la Lomé kuhusu Mfumo wa Mwitikio wa AU kwa Mabadiliko ya Serikali Kinyume na Katiba na Ibara ya 7(p) ya Itifaki Inayohusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la AU, ambayo huipa Baraza la Amani na Usalama mamlaka ya "kuunga mkono na kuwezesha hatua za kibinadamu katika mazingira ya kutumia migogoro ya silaha au majanga makubwa ya asili."

28. **LINAIOMBA** Kamisheni, kwa kushauriana kwa karibu na Baraza la Amani na Usalama, kutoa msaada muhimu wa kibinadamu kwa nchi wanachama zilizoathiriwa kupitia shughuli za kibinadamu na za afya za AU.

Kuhusu Msaada wa Kutoka Nje wa usimamizi wa uhamiaji na udhibiti wa mipaka

29. **LINAAMUA**:

    **i)** **Kukataa** msaada wa kutoka nje wa usimamizi wa uhamiaji na udhibiti wa mipaka ambao unadhoofisha haki za binadamu na utu.
    **ii)** **Kuunga mkono** mipango inayoongozwa na Waafrika ya kushughulikia vyanzo vikuu vya uhamiaji, ikiwa ni pamoja na umaskini, migogoro, na mabadiliko ya tabianchi.
    **iii)** **Kuwasihi** wabia wa kimataifa kutoa msaada na rasilimali ili kuimarisha uwezo wa Afrika wa kukabiliana na majanga ya kibinadamu na usimamizi wa uhamiaji.
    iv) Kusisitiza umuhimu wa kulinda haki za binadamu na utu wa wahamiaji, wakimbizi, na watu waliopoteza makazi.

# UAMUZI KUHUSU UAJIRI WA WAJUMBE WA KIKUNDI HURU CHA TATHMINI UNAOFANYWA NA JOPO LA WAAFRIKA MAARUFU - EX.CL/1657(XLVIII)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAREJELEA** Uamuzi wa Baraza Kuu EX.CL/Dec.1240(XLIV), uliopitishwa wakati wa Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Tano (45) uliofanyika Julai 2024 huko Addis Ababa, Ethiopia, ambao uliiomba Kamisheni kukamilisha uanzishaji wa Kikundi Huru cha Tathmini na kutekeleza mchakato wa uteuzi kupitia Jopo la Waafrika Maarufu ili kuhakikisha uwazi;

2. **PIA LINAREJELEA** ripoti ya Jopo la Waafrika Maarufu, pamoja na ombi la Baraza Kuu la kukamilisha mchakato wa uteuzi wakati wa Mkutano wake wa Kawaida wa 46 na kuripoti kwa Baraza Kuu;

3. **LINAZINGATIA** mapendekezo ya Jopo la Waafrika Maarufu kuhusu uteuzi wa wanachama wa Kikundi Huru cha Tathmini cha Mfuko wa Amani, pamoja na mapendekezo ya Kamati ya Usimamizi wa Utendaji, na uteuzi uliofuata wa wanachama wa Kikundi Huru cha Tathmini uliofanywa na Bodi ya Wadhamini, ikijumuisha wanachama watano (5) wanaowakilisha kila kanda ya bara;

4. **LINAWAPONGEZA** wajumbe wa Jopo kwa mchango wao muhimu katika kusaidia Kamisheni kwenye mchakato mzima wa uteuzi wa Kikundi Huru cha Tathmini cha Mfuko wa Amani wa AU;

5. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuendelea kutoa taarifa za mara kwa mara kwa Baraza Kuu kuhusu uendeshaji wa Kikundi Huru cha Tathmini na katika ripoti zake zitakazofuata.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA TUME YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU (ACHPR)**
**Doc. EX.CL/1659(XLVIII)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti za Shughuli za Hamsini na nane (58) na Hamsini na tisa (59) za Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR);

2. **PIA LINAZINGATIA** uchaguzi wa Uongozi mpya wa ACHPR kwa muhula wa miaka miwili na **LINAWAPONGEZA** wajumbe wake wapya, Mhe. Kamishna Idrissa SOW, Mwenyekiti, na Mhe. Kamishna Hatem ESSAIEM, Makamu Mwenyekiti, kwa kuchaguliwa kwao na **LINAWAHIMIZA** kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mamlaka ya ACHPR;

3. **LINAKARIBISHA** juhudi zilizofanywa na ACHPR wakati wa kipindi cha mapitio ili kukuza na kulinda haki za binadamu barani;

4. **LINAZINGATIA ZAIDI** uandaaji wa Jukwaa la Pili la Pamoja la Mifumo Maalum, lenye kaulimbiu: *Haki za Binadamu kama kitu Muhimu kwa Maendeleo Endelevu Yanayozingatia Watu barani Afrika;*

5. **LINAPONGEZA** ACHPR kwa kuandaa Jukwaa la Pili la Kabla ya Kikao la Nchi Zilizoridhia Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu, lililohudhuriwa na Nchi Zilizoridhia na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Haki za Binadamu, Demokrasia, na Utawala, na kwa kuandaa **Mkutano kuhusu Utetezi wa Uidhinishaji wa Bara wa Mikataba iliyo chini ya Ufuatiliaji wa ACHPR** huko Accra, Ghana, chini ya Kaulimbiu: Kuelekea Kufikia Uridhiaji wa Kimataifa wa Mikataba yote ya Afrika ya Haki za Binadamu, ambayo ilitoa jukwaa la kutetea uridhiaji wa kimataifa wa hati za msingi za haki za binadamu zinazofuatiliwa na ACHPR;

6. **LINAKARIBISHA PIA** kupitishwa kwa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana; na **LINASISITIZA** ombi lake kwa Nchi Wanachama ambazo bado hazijaridhia mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ya Umoja wa Afrika, kufanya kila linalowezekana ili kuhakikisha zinaridhia;

7. **LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama wa mkataba wa Afrika ambazo zimetimiza majukumu yao ya kutoa ripoti na **KUZIHAMASISHA** zile ambazo hazijawahi kuwasilisha ripoti, pamoja na zile ambazo tayari zina ripoti za vipindi lakini hazijaziwasilisha, kuziwasilisha kwa mujibu wa Ibara ya 62 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu, Ibara ya 26 ya Protokali ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Haki za Wanawake katika Afrika, na Ibara ya 14 ya Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Ulinzi na Msaada kwa Wakimbizi wa Ndani katika Afrika;

8. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuheshimu uamuzi wa ACHPR kuhusu Mawasilisho yanayowahusu, pamoja na mapendekezo yaliyotolewa kulingana na Tume za Ufuatiliaji na Hitimisho na Maoni; na LINATOA WITO ZAIDI kwa Nchi Wanachama kuendelea kuziruhusu Tume za Ufuatiliaji za ACHPR kwenda katika Nchi Wanachama;

9. **LINAZINGATIA** uchapishaji wa Ripoti ya Misheni ya Pamoja ya Kutafuta Ukweli wa Mambo nchini Sudani**,** iliyotolewa na Baraza la Amani na Usalama la UA na kufanyika kwa njia ya mtandao, na **LINAISIHI** Serikali ya Sudani na nchi za jirani, kushirikiana na ACHPR kuiruhusu tume ya kutafuta ukweli wa mambo iliyopo eneo husika, kupata taarifa za moja kwa moja, kutoka vyanzo asili kwa wakimbizi na watu wengine walioathirika na mgogoro wa Sudani;

10. **LINAPONGEZA** jitihada zilizofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Gambia katika ujenzi wa makao makuu ya kudumu ya ACHPR, na jengo mbadala linalopendekezwa lenye nafasi zaidi za ofisi ili kutoa nafasi ya muda kwa Sekretarieti hadi hapo Makao Makuu yatakapokamilika, na **LINASISITIZA** maelekezo yake kwa Kamisheni kushirikiana kwa pamoja na Serikali ya Gambia na ACHPR katika kutafuta fedha na kuharakisha jitihada za ujenzi wa makao makuu;

11. **LINAZINGATIA** upungufu wa wafanyakazi wa ACHPR na **LINAKARIBISHA** juhudi zinazoendelea za kupitia muundo wa shirika la ACHPR, kwa kushauriana na Kamisheni, kufuatia maamuzi yake EX.CL/Dec. 995 (2018), EX.CL/Dec. 1080 (2020) na EX.CL/Dec. 11 (2024);

12. **LINASISITIZA** uamuzi wake EX.CL/Dec. 1244(XLIV) na **LINAIAGIZA** PRC kuharakisha mapitio ya muundo mpya wa ACHPR, ili kufungamanisha na mamlaka yake yaliyopanuliwa, na kutoa ripoti kwa Baraza Kuu katika kikao chake kijacho cha kawaida.

13. **LINAZINGATIA** changamoto ya bajeti inayoikabili ACHPR katika utekelezaji wa majukumu yake, na **LINAIAGIZA** PRC kutenga fedha za kutosha na kuisaidia ACHPR, kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

14. **LINAHIMIZA** ACHPR kuimarisha ushirikiano na Nchi Wanachama na Kamisheni ya UA, kwa ajili ya kuongeza usimamizi na ulinzi wa haki za binadamu katika Afrika; na **LINAZISIHI** Nchi Wanachama kusaidia kuandaa Mikutano ya Kamisheni; na

15. **LINAIDHINISHA** kuchapishwa kwa ripoti za shughuli za ACHPR zilizounganishwa, za 58 na 59, kwa kuzingatia michango na maoni yaliyotolewa na Nchi Zilizotia sainiA.

# UAMUZI
# KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA MAHAKAMA YA AFRIKA KUHUSU HAKI ZA BINADAMU NA WATU (AfCHPR)
# Doc. EX.CL/1660(XLVIII)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Shughuli ya Mahakama ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) kwa kipindi cha kuanzia Januari 1 hadi Desemba 31, 2025.

2. **LINATAMBUA** juhudi zilizofanywa na Mahakama ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu katika utekelezaji wa mamlaka yake, na **LINAHIMIZA** Mahakama, kwa kushirikiana na Nchi Wanachama na wadau husika, kuimarisha hatua zinazolenga kuboresha uzingatiaji wa maamuzi yake na kupanua ufikiaji wa mamlaka yake, kwa mujibu wa Itifaki.

3. **LINAZINGATIA KWA WASIWASI** kwamba zaidi ya miongo miwili baada ya kupitishwa kwake, ni Nchi Wanachama thelathini na nne (34) pekee za AU ndizo zilizoridhia Itifaki na ni Nchi nane (8) pekee kati ya Nchi 34 Zilizoridhia, ndizo zenye Azimio linalohitajika chini ya Ibara ya 34 (6), hivyo kuruhusu watu binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) kuwasilisha kesi moja kwa moja Mahakamani.

4. **LINATAMBUA PIA** kujitolea kunakooneshwa na Nchi Zilizoridhia Itifaki na **LINASISITIZA** haja ya hatua za haraka za kushughulikia mapengo yaliyobaki katika uridhiaji, uwekaji wa matamko chini ya Ibara ya 34(6), na ufuataji maamuzi ya Mahakama.

5. **LINAZIPONGEZA** Nchi Zilizoridhia nane (8) ambazo kwa sasa zina Azimio chini ya Ibara ya 34(6) ya Itifaki, yaani: Burkina Faso, Gambia, Ghana, Guinea Bissau, Malawi, Mali, Niger na Tunisia; likisifu uongozi wao na kujitolea kwao kikamilifu katika kufikia upatikanaji wa haki kwa kuondoa vikwazo vya ufikiaji wa mtu binafsi na hivyo kuwezesha utekelezaji kamili wa mamlaka ya ulinzi ya Mahakama.

6. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama ambazo zimeondoa Matamko yao chini ya Ibara ya 34(6) kufikiria upya uamuzi wao na kuweka tena Azimio hilo, na kuthibitisha kujitolea kwao kwa uadilifu na ufikiaji kamili wa mfumo wa mahakama wa haki za binadamu wa Afrika.

7. **LINATOA WITO ZAIDI** kwa Nchi Wanachama ambazo bado hazijakubali Itifaki na kuweka Azimio hilo chini ya Ibara ya 34(6) kuchukua hatua muhimu za kisheria na kiutawala na **LINAIOMBA** Kamisheni kutoa ripoti kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika suala hili katika Mkutano ujao wa Kawaida wa Baraza Kuu.

8. **LINAZIPONGEZA PIA** Nchi ishirini na nne (24) Wanachama ambazo zimeteua Vituo Vikuu vya Kitaifa vya Mahakama, ambazo ni: Algeria,Benin, Botswana, Burkina Faso, Burundi, Cameroon, Cape Verde, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ghana, Lesotho, Liberia, Madagascar, Malawi, Mauritania, Mauritius, Msumbiji, Nigeria, Uganda, Senegal, Afrika Kusini, Tanzania na Zimbabwe, kulingana na Uamuzi EX.CL/Dec.1153 (XL), uliopitishwa wakati wa Kikao cha Kawaida cha 40 40th cha Baraza Kuu, kilichofanyika kuanzia tarehe 2 - 3 Februari 2022, huko Addis Ababa, Ethiopia.

9. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama ambazo bado hazijafanya hivyo, zichukue hatua za haraka za kuteua Wawakilishi Maalumu wa Kitaifa katika kutambua jukumu muhimua la Wawakilishi Maalumu wa Kitaifa katika kutumika kama kiungo maalumu na mfumo wa uratibu kwa mawasiliano muhimu na ufuatiliaji wa shughuli zinazohusu Mahakama;

10. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama ambazo zimeteua Wawakilishi Maalumu wa Kitaifa kuhakikisha mifumo hii inafanya kazi kikamilifu na inaimarishwa kisheria ndani ya mfumo wa utawala wa kitaifa, na ina rasilimali za kutosha za kibajeti, kuratibu kazi za mashirika anuwai ya serikali na kuwashirikisha kikamilifu wadau wa ndani katika mchakato wa utekelezaji.

11. **LINAZINGATIA** kwa wasiwasi mkubwa kiwango cha chini cha kufuata maamuzi ya Mahakama na **LINAAGIZA** Kamati Ndogo ya PRC ya Haki za Binadamu, Demokrasia na Utawala (HRDG) kuanzisha vikao vya mara kwa mara vya mapitio ya ufuataji sheria vinavyolenga ufuatiliaji wa kimfumo wa juhudi za utekelezaji na changamoto.

12. **LINAELEZA WASIWASI MKUBWA** juu ya kiwango cha chini cha uzingatiaji wa maamuzi ya Mahakama ya Afrika, na **LINAZISIHI** Nchi Wanachama kuwasilisha, ndani ya mzunguko wa utoaji ripoti uliobainishwa, taarifa kuhusu hatua zilizochukuliwa kutekeleza maamuzi kama hayo, ikiwa ni Pamoja na changamoto zilizotokea.

13. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kushirikiana kikamilifu na Mahakama kuandaa vikao vya majadiliano kuhusu utekelezaji wa maamuzi ya Mahakama; na **LINAZIOMBA** Nchi Wanachama zitoe rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya uandaaji wa vikao hivi vya majadiliano, kwa kutambua thamani ya vikao hivyo kwa ajili ya uzingatiaji wa kina.

14. **LINAIPONGEZA** Mahakama katika kupata rasilimali kwa njia ya usaidizi wa kiufundi kwa ajili ya utekelezaji wa Uamuzi EX.CL/Dec.1245(XLIV), likitoa wito kwa Mahakama ya Afrika na Tume "*kufanya utafiti kuhusu hali ya uzingatiaji wa maamuzi ya mashirika ya haki za binadamu ya Umoja wa Afrika, ikiwa ni pamoja na, hasa sababu za kiwango cha chini cha uzingatiaji na kutoa mapendekezo thabiti kwa Baraza kuu, kuhusu jinsi ya kuimarisha utekelezaji wa maamuzi hayo unaofanywa na Nchi Wanachama*."

15. **LINAIDHINISHA** Kalenda ya kazi kuhusu utafiti wa kina juu ya utekelezaji wa maamuzi ya mashirika ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Afrika kama ilivyoidhinishwa na Mkutano wa 4 wa Kamati Ndogo ya Wawakilishi wa Kudumu kuhusu Demokrasia ya Haki za Binadamu, na Utawala na kwa lengo hili, **LINAOMBA** Mahakama ya Afrika kuripoti kwa Baraza Kuu mnamo Januari 2027.

16. **LINAIELEKEZA** Kamisheni kupitia Usanifu wa Utawala wa Afrika - Sekretarieti ya Usanifu wa Amani na Usalama ya Afrika kuanzisha Mwakilishi Maalumu au Kitengo cha Uratibu ili kuweka mahali pamoja usaidizi wa kiufundi, uhamasishaji wa rasilimali, na uratibu wa utekelezaji na usambazaji wa maamuzi yaliyotolewa na Mahakama na mapendekezo yaliyotolewa na Mashirika mengine ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Afrika.

17. **LINARUDIA** Maamuzi yake yaliyopita EX.CL/Dec.973 (XXXI); EX.CL/Dec.994 (XXXII); EX.CL/Dec.1044 (XXXIV); EX.CL/Dec.1064 (XXXV); na EX.CL/Dec.1079), ya kuchukua hatua zote muhimu kufanya Mfuko wa Msaada wa Kisheria kwa Vyombo vya Haki za Binadamu vya Umoja wa Afrika utekelezwe, na kulingana na hayo, **LINAZIALIKA** na **KUZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika, na wadau wengine wa haki za binadamu katika bara la Afrika, kutoa michango ya hiari ya ukarimu kwa ajili ya Mfuko huu ili kuhakikisha uendelevu na mafanikio yake;

18. **LINAIELEKEZA** Mahakama ya Afrika, kwa kushirikiana na Kamisheni ya AU, kuandaa pendekezo kamili la kuanzishwa kwa Wakfu wa Mfuko wa Mahakama ya Afrika ili kupata ufadhili wa muda mrefu, ulio endelevu kwa shughuli zake za msingi, kujenga uwezo na utekelezaji wa maamuzi muhimu, na kuripoti juu ya hali ya pendekezo hili katika Kikao kijacho cha Kawaida.

19. **LINAZINGATIA** kwamba Mahakama ya Afrika itaadhimisha miaka ishirini (20) ya uendeshaji wake mwaka 2026, na **LINAZIALIKA** Nchi zote Wanachama na wadau husika kufanya kazi na Mahakama ya Afrika ili kutekeleza shughuli thabiti za kuadhimisha Miaka 20 ya kuanzishwa kwake, na kutoa michango thabiti, kuhusu jinsi ya kuimarisha Mahakama, kufanya ijulikane zaidi barani Afrika, na kuifanya ifae kwa kusudi lililo ndani ya mabadiliko yanayoendelea kutokea kijamii na kiuchumi na kisiasa barani Afrika.

20. **LINAPONGEZA** hatua zilizochukuliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ukamilishaji wa majengo ya kudumu ya Mahakama.

21. **LINAIOMBA** Mahakama, kwa kushirikiana na RPC na Kamisheni, kuripoti katika Mkutano wa Kawaida wa 49 wa Baraza Kuu mnamo Juni 2026, kuhusu utekelezaji wa Uamuzi huu.

## UMAMUZI

## KUHUSU RIPOTI YA BARAZA LA UCHUMI, UTAMADUNI NA MASUALA YA KIJAMII (ECOSOCC)
## Doc. EX.CL/ 1661(XLVIII)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Shughuli za Mwaka 2025 ya Baraza la Uchumi, Utamaduni na Masuala ya Kijamii (ECOSOCC) pamoja na mawasilisho yake ya mifumo ya kitaasisi na mafanikio ya utekelezaji wa programu.

**KUHUSU TOLEO JIPYA LA NYARAKA ZA KISHERIA ZA ECOSOCC**

2. **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1157(XL) ulioelekeza Sekretarieti ya Baraza la Uchumi, Utamaduni na Masuala ya Kijamii (ECOSOCC), kwa kushauriana na Ofisi ya Mshauri wa Kisheria na Ofisi ya Usimamizi wa Ndani, kufanya mapitio ya kina na ya jumla ya nyaraka za kisheria za ECOSOCC kwa kujumuisha mapendekezo ya Utafiti wa Kina wa ECOSOCC na Ripoti ya Uchunguzi ya Ofisi ya Usimamizi wa Ndani (OIO);

3. **LINATAMBUA** Jopokazi la Kiufundi, linalojumuisha Sekretarieti ya ECOSOCC, Ofisi ya Mshauri wa Kisheria na Ofisi ya Usimamizi wa Ndani, kukamilisha marekebisho ya kiufundi ya Sheria za ECOSOCC, na kwamba toleo jipya la nyaraka limethibitishwa na Mkutano Mkuu wa 4 wa ECOSOCC Oktoba 2025 na [kuidhinishwa katika Kikao cha 11 cha Kawaida cha Kamati ya Kiufundi Maalum ya Masuala ya Haki na Sheria (STC-JLA)] Desemba 2025.

4. **LINAKUBALI** Sheria za ECOSOCC zilizorekebishwa, kama zilivyoidhinishwa na STC-JLA, zinashughulikia mianya, migongano na kutokuwiana katika mfumo wa kisheria wa chombo hicho, na kurahisisha muundo wa wanachama, mifumo ya uchaguzi, uendeshaji wa Kamati za Vikundi vya Kisekta, na miundo ya usimamizi wa taasisi.

**KUHUSU MIFUMO YA KITAASISI YA AU KWA USHIRIKI WA ASASI ZA KIRAIA (AZAKI)**

5. **LINAZINGATIA** maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Mfumo ya Pamoja ya AU Kuangazia Hali ya Ushiriki na Ushauri kwa Asasi za Kiraia (CSO) na Mfumo wa Kisheria wa Diaspora ya ECOSOCC Februari 2025 (EX.CL/Dec.1286(XLVI)), pamoja na ushirikiano wa ECOSOCC na Nchi Wanachama katika mchakato wa utekelezaji.

6. **LINAELEKEZA** ECOSOCC kuasisi jukwaa la mtandaoni la Usajili wa CSO za AU na kuanzisha mchakato wa utekelezaji wa kina na vyombo vyote vya AU kuhakikisha mpangilio wa usajili unatekelezwa kwa urahisi, kwa ushauriano wa karibu na Nchi Wanachama.

**KUHUSU UWEZO WA KITAASISI NA UFANISI WA KIUENDESHAJI**

7. **LINAPONGEZA** ECOSOCC kwa mafanikio yake ya kuimarisha ushiriki wa asasi za kiraia katika mfumo wa Umoja wa Afrika, hasa kupitia Jukwaa la Wananchi la 2025, Mjadala wa Watu kwa Watu Afrika-Uchina, nafasi yake ya uongozi katika Mkutano wa Kijamii wa G20 kwa kuhamasisha asasi za kiraia za Afrika kabla ya Mkutano huo, na shughuli zake za kimuundo zinazoendana na Kaulimbiu ya Mwaka ya Umoja wa Afrika;

8. **LINATAMBUA** kuwa kwa sasa ECOSOCC inafanya kazi ikiwa na nafasi 19 tu kati ya 34 zilizoidhinishwa (asimilia 56 ya uwezo wa wafanyakazi), jambo linalopunguza uwezo wa Sekretarieti kutekeleza ajenda ya kiufundi na kufanikisha wajibu wake;

9. **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1199(XLII) wa Februari 2023, uliyoomba Kamisheni kuchukua hatua haraka kumalizia tathmini ya ujuzi na uwezo wa wafanyakazi wa kudumu wa ECOSOCC**.**

10. **LINATAMBUA KWA WASIWASI** kucheleweshwa kwa muda mrefu katika kumaliza tathmini inayozingatia ujuzi na uwezo ya wafanyakazi waliopo, jambo lililosababisha kutokuwa na uhakika na kupungua morali ya kitaasisi;

11. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuweka kipaumbele kwenye kukamilika kwa muundo wa wafanyakazi wa ECOSOCC uliopitishwa wa nafasi 34, kwa lengo la kufikia uwezo wa wafanyakazi kwa asilimia 80 ifikapo Desemba 2026, kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Wafanyakazi wa Umoja wa Afrika na Mfumo wa Ajira Kulingana na Ustadi.

**KUHUSU BAJETI YA PROGRAMU NA UKUSANYAJI WA RASILIMALI**

12. **LINATAMBUA** kwamba tangu kuhamia Lusaka na kuanzisha kituo huru cha kiutendaji, ECOSOCC imeonesha uwezo mkubwa zaidi wa kutekeleza programu na kuvutia riba kubwa kutoka kwa washirika wa kimataifa wanaotoa rasilimali muhimu;

13. **LINATAMBUA PIA** kiwango cha sasa cha bajeti ya programu, kilichowekwa wakati ECOSOCC ilipoendesha Sekretarieti ya sehemu ya muda katika Tume, hakiwiani na kiwango cha sasa cha uendeshaji na umuhimu wake wa kimkakati, hivyo kukwamisha upatikanaji wa fedha za ushirikiano.

14. **LINAIOMBA** PRC kupitia Kamati yake Ndogo ya Usimamizi na Kuratibu Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala (GSCBFAM) na wataalamu wa F15 kutathmini na kuruhusu ongezeko la kiwango cha bajeti ya programu ya ECOSOCC, ili kiwe sawa na uwezo wake uliopanuka wa kiutendaji, fursa za ushirikiano zilizoongezeka, na mahitaji yanayokua ya ushiriki wa asasi za kiraia katika mfumo wa AU, na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika shughuli na programu za AU na vyombo vyake.

**KUHUSU MUONGO WA FIDIA WA AU**

15. **LINAKUMBUKA** tamko la Umoja wa Afrika la Muongo wa Fidia (2026–2036), ukijenga katika Mwaka wa Fidia wa 2025 na Tamko la Kihistoria la Abuja la 1993.

16. **LINAIDHINISHA** uzingatiaji wa kimuundo wa ECOSOCC katika kuendeleza Miaka Kumi ya Fidia ya AU, ikiwa ni pamoja na utumiaji wa waraka mweupe wa ECOSOCC wa asasi za kiraia kuunda Msimamo wa Pamoja wa Bara na Mpango wa Kutekeleza Fidia.

**KUHUSU BARAZA KUU LA KUDUMU LA TANO (5)**

17. **LINAKUBALI** kuwa kwa mara ya kwanza katika historia ya ECOSOCC, kufanya Mkutano Mkuu wa tano (5) wa ECOSOCC katika robo ya nne ya 2025 kulihusisha ujumlishaji wa asasi za kiraia za Diaspora kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa katika Mfumo wa Kisheria wa Diaspora ya ECOSOCC.

18. **LINABAINI** kutokuwapo kwa rasilimali za bajeti za kuunda upya na kuitisha Kikao cha Kawaida cha Baraza Kuu la Kudumu la tano (5) la ECOSOCC mwaka 2026;

19. **LINATAMBUA** uwezekano wa athari hasi ya kisheria na kiutendaji kutokana na kutoundwa upya kwa Baraza Kuu la tano (5) na kutekelezwa kwa kikao cha kwanza, kukiwamo kurudiwa kwa changamoto za usimamizi na kisheria zilizokumbwa na Mkutano Mkuu uliopita, jambo linalohitaji uingiliaji wa Baraza Kuu Tendaji.

20. **LINAOMBA** Tume kushirikiana na ECOSOCC kutekeleza suluhisho kupitia bajeti ya ziada au uhamisho wa fedha (virement) ili kuiwezesha ECOSOCC kuunda Baraza Kuu la tano (5) na kuitisha Kikao cha Kwanza cha Baraza Kuu la Kudumu la tano (5) kulingana na matakwa ya kisheria.

**KUHUSU PROGRAMU YA UTOAJI HUDUMA KWA JAMII YA CHUO KIKUU YA ECOSOCC 2025**

21. **LINAIHIMIZA** ECOSOCC kuendelea kupanua programu yake ya uhamasishaji wa vyuo vikuu ili kuipanua katika maeneo mengine ambayo hayajahusika kwa sasa, haswa kanda za Afrika Magharibi na Kati.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA KAMATI YA WATAALAMU YA AFRIKA KUHUSU HAKI NA USTAWI WA MTOTO (ACERWC)
## Doc. EX.CL/1662(XLVIII)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamati ya Wataalamu ya Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto (**ACERWC**).

2. **LINAZINGATIA** PIA uchaguzi wa Uongozi (*Bureau*) mpya wa ACERWC kwa muhula wa miaka miwili (Novemba 2025 hadi Novemba 2027) na LINAWAPONGEZA wajumbe wake wapya, Mhe. Sabrina Gahar, Mwenyekiti, Mhe. Ghislain Roch Etsan, Makamu Mwenyekiti kwa kuchaguliwa kwao na **LINAWAHIMIZA** kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mamlaka ya ACERWC.

3. **LINAIPONGEZA** Kamati kwa kazi iliyofanywa katika kufuatilia utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto na kwa ushiriki ulioongezeka na Nchi Wanachama.

4. **LINAHIMIZA PIA** Nchi Wanachama ambazo bado hazijaridhia Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto kuharakisha kuridhia Mkataba huo.

5. **LINAISIFU PIA** Jamhuri ya Shirikisho la Somalia kwa uidhinishaji kwa ngazi ya kitaifa na **LINAISIHI** Nchi hiyo Mwanachama kuwasilisha hati yake ya kuridhia kwa Umoja wa Afrika kwa wakati unaofaa.

6. **LINAIPONGEZA PIA** Jamhuri ya Burundi, Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Kiarabu ya Misri; Nchi ya Eritrea; Jamhuri ya Gambia, na Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania kwa kuwasilisha ripoti zao za Nchi Zilizoridhia kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Watoto wa Afrika na **LINAZISIHI PIA** Nchi Zilizoridhia, ambazo bado hazijaripoti kwa Kamati kuzingatia majukumu yao ya kuripoti.

7. **LINASHUKURU** Jamhuri ya Burundi kwa hatua ilizochukua katika kutekeleza mapendekezo ya Kamati kwenye ripoti yake ya awali na **LINAIHIMIZA ZAIDI** kufuata kikamilifu Maoni na Mapendekezo ya Mwisho ya Kamati.

8. **LINASHUKURU PIA** Nchi Zilizoridhia zinazoshirikiana na Kamati katika kutekeleza maamuzi yake kuhusu Mawasiliano yaliyowasilishwa dhidi yao na **LINAZIHIMIZA** kutekeleza kikamilifu maamuzi ya Kamati na kuwasilisha ripoti kuhusu hali ya utekelezaji.

9. **LINAISIFU** Jamhuri ya Burundi kwa kuwasilisha ripoti yake kuhusu hali ya utekelezaji wa Suluhu ya Amani iliyofikiwa chini ya usimamizi wa Kamati katika Mawasiliano Na. 0022/Com/004/22 na **LINAHIMIZA PIA** utekelezaji kamili wa masharti ya suluhu hiyo.

10. **LINASHUKURU ZAIDI** Jamhuri ya Botswana kwa suluhu ya amani na linaihimiza kutekeleza kikamilifu masharti ya suluhu hiyo.

11. **LINAPITISHA** kaulimbiu ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka 2026 kuwa: **"*Kuhakikisha upatikanaji wa maji, usafi wa mazingira na huduma za usafi kwa kila mtoto barani Afrika*"** na **LINAHIMIZA ZAIDI** Nchi Wanachama kutekeleza shughuli zilizobainishwa na Kamati na kuwasilisha ripoti kuhusu utekelezaji wake.

12. **LINASIFU** Nchi Wanachama kwa hatua walizochukua katika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka 2025 yenye kaulimbiu: "Mipango na Bajeti kwa Watoto Barani Afrika: Maendeleo Tangu 2010" na **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutekeleza mapendekezo ya Kamati na kuripoti kuhusu utekelezaji huo.

13. **LINAZIHIMIZA PIA** Nchi Wanachama:

    (i). Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya watoto na kuhakikisha wanaonekana katika bajeti na programu za kitaifa; kuzingatia maoni ya watoto katika upangaji bajeti; kuwa na data ya kisasa na data iliyogawanywa ili kutathmini mahitaji ya watoto; na kufanya tathmini za haki za watoto za upangaji bajeti na programu.

    (ii). Kutumia na kutekeleza Maoni ya Jumla Namba 9 kwenye Ibara ya 11 ya Mkataba wa Watoto wa Afrika kuhusu Haki ya Elimu; na Maoni ya Jumla Namba 10 kuhusu Ibara ya 25 ya Mkataba wa Watoto wa Afrika kuhusu Watoto Wasio na Matunzo ya Wazazi katika kulinda vifungu vya Mkataba.

    (iii). Kutumia Miongozo ya Kuripoti Haki na Ustawi wa Watoto Wenye Ualbino na kujumuisha hatua zilizochukuliwa ili kutoa hatua maalum za ulinzi kwa watoto wenye ualbino katika ripoti zao za Nchi Zilizoridhia kulingana na Miongozo.

    (iv). Kutumia Utaratibu Uliolengwa wa Kuripoti wa Nchi Zilizoridhia na kushirikiana na Kamati kushiriki katika utaratibu huu na kuwasilisha ripoti kulingana na orodha ya masuala yatakayotolewa kabla ya kuripoti.

14. **LINASIFU PIA** ushiriki wa Nchi Wanachama katika maadhimisho ya Miaka 35 ya kupitishwa kwa Mkataba wa Afrika wa Haki za Mtoto na linazihimiza kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa wakati wa maadhimisho hayo.

15. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama husika kushughulikia matatizo ya watoto katika hali za migogoro.

16. **LINAHIMIZA ZAIDI** Nchi Wanachama kutekeleza ahadi zao wakati wa Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri wa Dunia kuhusu Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Watoto (Mkutano wa Bogotá).

17. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama kutekeleza mapendekezo ya Utafiti kuhusu Utekelezaji wa Maamuzi na Mapendekezo ya Kamati na Utafiti kuhusu Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Haki za Watoto Barani Afrika.

18. **LINAHIMIZA PIA** Nchi Wanachama kuanzisha **Taratibu za Kitaifa za Utekelezaji, Utoaji ripoti na Ufuatiliaji (NMIRFs) zilizoanzishwa kisheria na zenye rasilimali nyingi**. Uzoefu uliotolewa ulionesha kuwa NMIRF zilizo na mamlaka wazi, bajeti endelevu, na muundo jumuishi wa wadau mbalimbali, unaohusisha serikali, NHRIs, AZAKI, na watoto, ni muhimu kwa kusimamia mzunguko wa kuripoti.

19. **LINATOA WITO** kwa Kamati kushirikiana na Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Demokrasia, Utawala na Haki za Binadamu kushughulikia changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa jukumu lake la ufuatiliaji; na **LINAIOMBA** Kamati kuripoti kwa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu hali ya utekelezaji wa maamuzi yake.

20. **LINAHIMIZA ZAIDI** Nchi Wanachama kupitisha na kufadhili vya kutosha Mipango ya Kitaifa ya Utekelezaji kuhusu Biashara na Haki za Binadamu inayojumuisha uangalifu wa haki za watoto, mifumo ya utekelezaji, na mifumo imara ya ufuatiliaji, pamoja na ushiriki wenye tija wa jamii na watoto walioathiriwa.

21. **LINAHIMIZA** Jamhuri ya Ghana kushirikiana na Kamati katika muktadha wa Mawasiliano yanayosubiri na kukamilisha suluhu ya amani inayoendelea.

22. Likikaribisha hatua za Gambia za kushughulikia kesi ya kusikitisha ya mtoto wa mwezi 1 aliyefariki kutokana na ukeketaji, likitambua hatua za haraka zilizochukuliwa kuwashtaki wahalifu wakuu, huku mshukiwa mkuu akikabiliwa na kifungo cha maisha jela, likizingatia mchakato unaoendelea wa mahakama na ahadi ya kuruhusu mchakato unaofaa kutokea, **LINAISIFU** Gambia kwa kuchukua hatua madhubuti za kuwawajibisha wahalifu na kuonyesha kujitolea kupambana na ukeketaji na kulinda haki za watoto. **LINAUNGA MKONO** juhudi zinazoendelea za kutokomeza ukeketaji na **LINAHIMIZA PIA** Gambia kuendeleza juhudi za kuzuia ukeketaji na kulinda watu walio katika hatari.

23. **LINAIHIMIZA ZAIDI** Jamhuri ya Gambia kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya kutokomeza ukeketaji na kuwashtaki wahusika wa ukeketaji wanaokiuka haki ya kuishi na maendeleo ya watoto na kuripoti kuhusu hali ya utekelezaji wa mapendekezo hayo katika barua za pamoja za maombi ya dharura za ACHPR na ACERWC.

24. **LINATOA PONGEZI** kwa wajumbe wa ACERWC wanaomaliza muda wao wa kuhudumu, **LINAWAPOKEA** wale walioteuliwa upya, na **LINAZIHIMIZA** Nchi

Wanachama ambazo raia wake wameteuliwa kuwezesha ushiriki wa maana wa wajumbe hao katika kazi za Kamati ikiwa ni pamoja na ushiriki wao kwenye mikutano ya kawaida ya ACERWC.

**25.** **LINAAMUA** kuoanisha manufaa ya wajumbe wa Kamati kwa kutoa posho ya mahakama na posho ya kati ya vikao kwa mujibu wa mamlaka yake ya kisheria na manufaa ya maafisa wengine waliochaguliwa wa vyombo vingine kulingana na uamuzi EX.CL/Dec.1057(XXXV) na **LINAIOMBA** Kamisheni kufanya kazi na KAmati ndogo ya PRC kuhudu Usimamizi na uratibu wa Jumla juu ya Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala ili kutekeleza hilo.

**26.** **LINAKARIBISHA** shughuli zilizofanywa, maazimio, tafiti na viwango vilivyotengenezwa na Vikundi vya Kazi vya ACERWC na **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutumia utaratibu huo ndani ya ACERWC.

**27.** **LINARUDIA** uamuzi EX.CL/Dec. 1248 (XLIV) unaoiomba Tume kuharakisha kukamilisha utoaji ajira kwa wafanyakazi wa Sekretarieti ya Kamati na kutoa mwongozo kuhusu uwezekano wa kuruhusu ACERWC kuajiri wafanyakazi wake yenyewe.

**28.** **LINAHIMIZA PIA** Nchi Wanachama kuimarisha zaidi ushirikiano wao na ACERWC, ikiwemo kuzingatia kuandaa Vikao vya Kawaida vya ACERWC na kupeleka wafanyakazi wenye sifa ili kushughulikia upungufu mkubwa wa rasilimali watu ndani ya Sekretarieti ya Kamati.

**29.** **LINATOA PONGEZI** kwa Ufalme wa Lesotho kwa kuhakikisha uendeshaji mzuri wa Sekretarieti ya ACERWC; na linaihimiza nchi mwenyeji kuendelea kutoa msaada unaohitajika kwa mujibu wa makubaliano ya mwenyeji, ikiwemo ujenzi wa haraka wa majengo ya kudumu ya ofisi na kuendelea kuwezesha Vikao vyake vya Kawaida.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI YA BUNGE LA AFRIKA (PAP) - EX.CL/1663(XLVIII)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Shughuli ya Bunge la Afrika (PAP) kwa mwaka 2025.

2. **LINALIPONGEZA** Bunge la Afrika na Sekretarieti yake kwa maendeleo ambayo limeyapata tangu kuingia madarakani kwa Uongozi wa sasa na kurejeshwa kwa Katibu wa Bunge.

3. **LINASIFU PIA** shughuli zilizotekelezwa na Bunge la Afrika zinazoendana na Mpango wake Mkakati wa 2024–2028, na **LINASIFU** shughuli za usimamizi za Bunge la Afrika, ikiwa ni pamoja na ushiriki katika Misheni za AU za Uangalizi wa Uchaguzi na majadiliano kuhusu haki na fidia.

4. **LINAZINGATIA PIA** maendeleo yaliyopatikana katika utekelezaji wa uamuzi EX.CL/Dec.1242(XLIV) kuhusu Kanuni za Utaratibu na **LINAHIMIZA** PRC na PAP kukamilisha kupitishwa kwa Kanuni za Utaratibu zilizorekebishwa.

5. **LINAKUMBUKA** uamuzi EX.CL/Dec.1288 (XLVII), ambao uliagiza mapitio ya PRC ya mgao wa bajeti kwa PAP na mapitio ya uamuzi EX.CL/Dec.1057(XXXV) kuhusu malipo ya **misha**hara kwa maafisa waliochaguliwa kwa lengo la kurejesha posho za Wabunge wa PAP. **LINAIOMBA** PAP, PRC na Kamisheni kutoa ripoti kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa uamuzi EX.CL/Dec.1288(XLVII), katika Kikao kijacho.

6. **LINAZINGATIA ZAIDI** maendeleo yaliyopatikana katika marekebisho ya Kanuni za Utaratibu za PAP na **LINAAMUA**:

   i. **KUSISITIZA** kwamba uchaguzi wa Uongozi wa PAP utafanyika Februari 2026, kwa mujibu wa uamuzi EX.CL/Dec.1288(XLVI), na kwamba Uongozi mpya utakaochaguliwa utaundwa kama ifuatavyo:
      - Rais: Ukanda wa Afrika ya Kaskazini
      - Makamu wa Rais wa Kwanza: Ukanda wa Afrika Mashariki
      - Makamu wa Rais wa Pili: Ukanda wa Afrika Magharibi
      - Makamu wa Rais wa Tatu: Ukanda wa Afrika ya Kati
      - Makamu wa Rais wa Nne: Ukanda wa Afrika ya Kusini

   ii. **KUTHIBITISHA** kwamba PAP lazima izingatie maadili na kanuni za Umoja wa Afrika, ikiwa ni pamoja na kanuni ya mzunguko wa kawaida na unaotabirika;

   iii. **KUIOMBA** PAP kudumisha katika Kanuni zake za Utaratibu muhula wa miaka mitatu wa Uongozi (Bureau) ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kanuni ya mzunguko wa kawaida na unaotabirika;

iv. **KUIOMBA PIA** kwamba mwendelezo wa kujadiliwa kwa rasimu ya Kanuni za Utaratibu zilizorekebishwa hautakuwa na athari yoyote katika kufanyika kwa uchaguzi wa Uongozi wa PAP mwezi Februari 2026;

v. **KUMUOMBA ZAIDI** Mwenyekiti wa Kamisheni kupeleka Kundi la Ngazi ya Juu lililopewa jukumu la kusimamia uchaguzi wa Uongozi wa PAP mwezi Februari 2026 na kuwasilisha ripoti kwa Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Tisa (49) wa Baraza kuu.

7. **LINAIPONGEZA,** Bunge la Afrika, kwa ushirikiano wake uliofanikiwa na Bunge la Afrika Kusini katika kuwezesha mkutano wa P20 wa Maspika na mchango uliotolewa na Mabunge na Watu wa Afrika kwa G20 na ajenda ya maendeleo ya kimataifa.

8. **LINAIPONGEZA ZAIDI** Bunge la Afrika kwa ushirikiano wake na Bunge la Ulaya katika kuandaa mkutano wa Bunge hadi Bunge huko Midrand, Afrika Kusini na kupitia hili, usemi wa Mabunge ya Afrika na Raia kuhusu sera za bara zinazofanana kwa Afrika na Ulaya na **LINAKARIBISHA** diplomasia ya bunge, ikiwa ni pamoja na Azimio la Pamoja na Bunge la Ulaya juu ya urejeshaji wa mali za kihistoria za Afrika

9. **LINAZINGATIA ZAIDI** kuundwa na Mkutano Mkuu wa Bunge la Afrika kwa Sheria tatu (3) mpya za Mfano za Bara kuhusu

I. Sheria ya Mfano kuhusu Uhamiaji wa Ajira Barani Afrika;
II. Sheria ya Mfano kuhusu Usawa wa Kijinsia na Usawa; na
III. Sheria ya Mfano kuhusu Usimamizi Endelevu wa Udongo barani Afrika

na maendeleo yake katika sheria ya mfano na inasisitiza kuhimiza kwake uundaji wa sheria zake za mfano kwa kushirikiana na kamati Maalum za Ufundi kwa ajili ya kuimarisha mshikamano wa kanuni na kisheria katika maandishi ya Umoja wa Afrika na **LINAHIMIZA ZAIDI** Nchi Wanachama kutumia Sheria hizi za Mfano kama vyombo vya kuongoza kwa kuimarisha mifumo yao ya kitaifa ya kisheria na sera katika maeneo husika ya kimaudhui, baada ya kupitishwa kwake na Vyombo vya Sera.

   (i) **Kuwapangia kazi wafanyakazi wataalamu sita (6) "Wanaokidhi" waliotathminwa na kuonekana wanakidhi** ambao wanaweza kujumuishwa katika idadi zao za ukomo (*quota*) zilizosasishwa za nchi, kupitia Kamati ya Uhamasishaji na Uhamaji chini ya Kanuni na Sheria za Wafanyakazi (SRR), huku kanuni ya sifa ikifuatwa.

   (ii) **Kuwabakisha wafanyakazi wataalamu sita (6) waliosalia ambao walitathminiwa na kuonekana "Wanakidhi" lakini** hawawezi kupangiwa kazi kutokana na vikwazo vya idadi ya ukomo, chini ya makubaliano yao ya kimkataba ya ajira, kulingana na Kanuni na Sheria za Wafanyakazi, na kuwapangia kazi iwapo idadi ya ukomo ya nchi itafunguliwa.

   (iii) **Kuwapa wafanyakazi wanne (4) wa Huduma za Uendeshaji waliotathminiwa na kupendekezwa kwa ajili ya kupangiwa kazi katika nafasi ya daraja la juu (mtaalamu)** lakini hawakuweza kupangiwa kazi kutokanana na kizuizi cha idadi ya ukomo, uamuzi wa kubaki katika daraja la Huduma za Uendeshaji kufuatia upangaji kazi uliofanywa na Kamati ya Uhamasishaji na Uhamaji chini ya SRR.

(iv) **Kubakiza Wafanyakazi ishirini na wanane (28) wa Huduma za Uendeshaji** ambao hawakuweza kupangiwa kazi kwa sababu ya kukosekana kwa nafasi zinazooana, katika mipango yao ya sasa ya kimkataba, na kubainisha nafasi mbadala ndani ya muundo ulioidhinishwa kwa Wafanyakazi hawa ishirini na wanane (28) wa Huduma za Uendeshaji, na kuwapangia ipasavyo kulingana na Uamuzi Ex.CL/Dec.1321(XLVII), kupitia Kamati ya Ukuzaji na Uhamaji chini ya SRR.

(i) **Kufanya mapitio** ya matokeo ya tathmini ya SACA kwa Wafanyakazi Wataalamu ishirini na moja (21) waliotangazwa kuwa "Hawakidhi" kupitia Kamati ya Uhamasishaji na Uhamaji chini ya SRR ili kushughulikia mapungufu yanayohusiana na mchakato katika zoezi la tathmini. **Kuidhinisha na kutekeleza matokeo** ya Kamati ya Uhamasishaji na Uhamaji, kabla ya tarehe 30 Aprili 2026.

**6.** Kwa mujibu wa uamuzi EX.CL/Dec.1321(XLVII) **LINAIAGIZA** Kamisheni kuwasilisha ripoti kwa PRC ili kuwezesha majadiliano yanayoendelea kuhusu masuala mengine yote yanayosubiriwa yanayohusiana na mchakato wa SACA, ikiwa ni pamoja na:

i. Mchakato wa kuajiri watu uliopewa kipaumbele ili kujaza nafasi zilizo wazi katika muundo mpya
ii. Hali ya wafanyakazi wanaofadhiliwa na wabia
iii. Wafanyakazi wa P5 na P6 waliopandishwa cheo chini ya SACA lakini walibakia katika madaraja yao ya awali
iv. Wafanyakazi ambao shahada zao hazikuweza kuthibitishwa
v. Masuala mengine yoyote ambayo hayajashughulikiwa kwenye SACA

**7.** **LINAIAGIZA** kamisheni kutekeleza uamuzi huo mara moja, ili kutoa muda wa kutosha kwa Kamati ya Ukuzaji na Uhamaji kukamilisha kazi yake na kuwasilisha mapendekezo yake kwa Mwenyekiti wa kamisheni kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

**8.** **LINAIOMBA** Kamisheni kuchunguza mafunzo yaliyopatikana kutoka kwenye zoezi la SACA, ikiwa ni pamoja na mbinu za kuhamasisha na kuunganisha utaalamu kutoka nje katika michakato ya kufanya maamuzi.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA KIKAO CHA PAMOJA CHA KAMATI YA MAWAZIRI YA VIWANGO VYA MAKADIRIO NA MICHANGO NA KAMATI YA MAWAZIRI KUMI NA WATANO WA FEDHA (F15)
# Doc. EX.CL/1688(XLVIII)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kikao cha Pamoja cha Kamati ya Mawaziri ya Viwango vya Makadirio na Michango na Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha (F15) kilichofanyika tarehe 6 Februari, 2026.

**A. Kuhusu Hali ya Michango ya Nchi Wanachama kwenye Bajeti ya Kawaida na Mfuko wa Amani:**

2. **LINAREJEA** uamuzi Assembly/AU/Dec. 802(XXXIV) wa Februari 2021 huko Addis Ababa, Ethiopia, ambapo Mkutano Mkuu uliamua kukasimu mamlaka yake kwa Baraza Kuu, ili kutumia Utaratibu wa Vikwazo wa AU, kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 23 (1) ya Sheria Anzilishi na Sheria ya 36 ya Kanuni za Utaratibu wa Mkutano Mkuu.

3. **LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa kuchangia **dola za Marekani 167,902,992.67**, sawa na **84%** ya **dola milioni 200** za michango iliyotathminiwa kwa ajili ya Bajeti ya Kawaida ya mwaka 2025.

4. **PIA LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa kuchangia tangu 2017, **dola za Marekani 349,310,029.63,** kwenye Mfuko wa Amani wa AU, na hivyo kuonesha kiwango cha juu cha kujitolea kwa Umoja huo katika kutekeleza kikamilifu Mfuko huo na **KUZITOLEA WITO** Nchi Wanachama ambazo bado hazijakamilisha michango yao kufanya hivyo ili kutimiza majukumu yao ya kifedha kwa Umoja huo.

5. **LINAZIPONGEZA PIA** Nchi Wanachama zilizokamilisha michango yao iliyotathminiwa mwaka 2025 na **KUZIOMBA** Nchi Wanachama kutoa michango yao iliyokadiriwa ya mwaka 2026 kwa mujibu wa Kanuni ya 23(1) ya Sheria za Fedha za AU, kwa kuzingatia tofauti katika miaka ya fedha ya Nchi Wanachama.

6. **LINAAMUA** kuziwekea vikwazo Nchi Wanachama zifuatazo ambazo zinasuasua kutoa michango yao iliyokadiriwa:

   a. **Vikwazo vya kati:** Libya, Sudan Kusini, Jamhuri ya Afrika ya Kati, na São Tomé na Príncipe.

   b. **Vikwazo vya kina:** Guinea, Burkina Faso, Mali, na Niger.

**B. Kuhusu Nchi Wanachama zinazopitia hali ngumu na hivyo kushindwa kwa muda kutoa michango yao iliyokadiriwa:**

7. **LINAREJEA** uamuzi EX.CL/Dec.1071(XXXV) wa Julai 2019 ambao ulizingatia hali ya usalama na kisiasa ya Somalia na kuzuia nchi hiyo kuwekewa vikwazo kwa kutotoa michango, na ambao uliiomba Kamisheni kushauriana na nchi hiyo ili kukubaliana kuhusu utaratibu wa kutoa michango yake ndani ya miaka minne (4) tangu kupitishwa kwa Uamuzi huo.

8. **PIA LINAREJEA** uamuzi EX.CL/Dec.1119(XXXVIII) wa Februari 2021 ambao ulizingatia ombi la Jamhuri ya Sudani kuhusu haja ya kupitia mchango wake uliokadiriwa na kuiomba Kamisheni kushauriana na Jamhuri ya Sudani kulingana na Kiwango cha sasa cha Makadirio ili kukubaliana kuhusu utaratibu wa kulipa madeni yake haraka iwezekanavyo, ndani ya miaka minne (4) tangu kupitishwa kwa Uamuzi huo.

9. **LINAREJEA** uamuzi Assembly/AU/Dec.802(XXXIV) la Februari 2021 ambao uliidhinisha utaratibu wa kutoa michango wa Jamhuri ya Shirikisho la Somalia ili kulipa madeni yake.

10. **LINAREJEA PIA** Uamuzi Na. Assembly/AU/Dec.938(XXXVIII) wa Februari 2025 ambao ulibainisha kuwa mwaka 2024 ulikuwa mwaka wa mwisho wa kutekeleza utaratibu wa malipo uliokubaliwa mwaka 2021 na Jamhuri ya Shirikisho la Somalia na kuidhinisha utaratibu mpya wa malipo kwa nchi hiyo ili kulipa madeni yake ya jumla ya dola za Marekani 1,722,316.95 kufikia tarehe 1 Januari 2025, kwa kipindi cha miaka mitano pamoja na michango yake ya kila mwaka iliyokadiriwa kuanzia mwaka 2025 hadi 2029.

11. **LINAZINGATIA** kwamba Jamhuri ya Shirikisho la Somalia haikufuata utaratibu mpya wa malipo na **LINAIHIMIZA** Nchi hiyo Mwanachama kutimiza ahadi zake za kulipa madeni yake.

**C. Kuhusu kiwango kipya cha makadirio**

12. **LINAREJEA** uamuzi Assembly/AU/Dec.635(XXVIII) wa Februari 2017 ambao ulieleza kwamba Kiwango cha michango kinapaswa kurekebishwa kulingana na kanuni za uwezo wa kulipa, mshikamano, na usawa katika kugawana mizigo, ili kuepuka mkusanyiko wa athari.

13. **LINAREJEA PIA** uamuzi Assembly/AU/Dec.938(XXXVIII) wa Februari 2025 ambao ulibainisha kuwa mwaka 2026 ni mwisho wa kutekelezaa kiwango cha sasa cha madadirio kwa michango ya Nchi Wanachama (2024-2026) na kuiagiza Kamisheni kuanza mchakato wa kuweka kiwango kipya cha makadirio kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu mwezi Februari 2026 kwa kufuata mchakato unaostahili.

14. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kikao cha Pamoja cha Kamati ya Mawaziri ya Viwango na Makadirio na Michango na Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha kilichofanyika tarehe 6 Februari 2026 na machaguo mawili yaliyopendekezwa kwa ajili ya Kiwango cha Makadirio cha AU kinachofuata kwa kipindi cha 2027-2029.

15. **LINAZINGATIA PIA** chaguo la 4, ambalo lilipendelewa zaidi miongoni mwa baadhi ya Nchi Wanachama na Kanda, na ombi la muda wa ziada wa kufanya mashauriano zaidi baina ya baadhi ya Nchi Wanachama na Kanda.

16. **LINAZINGATIA PIA** ombi la Jamhuri ya Angola la kuendelea na hadhi yake ya ngazi ya 1 ikithibitisha kujitolea kwa Nchi hiyo kwa uendelevu wa kifedha na utendaji kazi mzuri wa AU, **LIKIELEZA** kwamba uamuzi huu utachangia kupunguza mzigo wa kifedha kwa uanachama mpana wa Umoja huo.

17. **LINAIDHINISHA** ombi la Nchi Wanachama la muda wa ziada wa kufanya mashauriano zaidi na wataalamu husika katika Nchi zao, wakitambua changamoto za kijamii na kiuchumi zinazoendelea kuzuia uwezo wa Nchi Wanachama kutimiza majukumu yao ya kifedha na **KUIOMBA** Kamisheni na Wataalamu wa F15 kuoanisha chaguo la 3 na la 4, kujumuisha ombi la Jamhuri ya Angola, na kufanya mashauriano ya kikanda **kabla ya Aprili 2026.**

18. **LINAAMUA** kwamba chaguo lililooanishwa liwasilishwe kwenye kikao cha 49 cha kawaida cha Baraza Kuu, mwezi Juni 2026, kwa ajili ya kuidhinishwa na kupitishwa.

19. **LINAPENDEKEZA** kwa Mkutano Mkuu kukasimu kwa Baraza Kuu mamlaka yake ya kupitisha kiwango kipya cha makadirio kwa kipindi cha mwaka 2027 hadi 2029 mwezi Juni 2026.

## UAMUZI KUHUSU WAGOMBEA WA AFRIKA KATIKA MFUMO WA KIMATAIFA
## Doc. EX.CL/1689(XLVIII)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamati ya Mawaziri kuhusu Wagombea wa Afrika katika Mfumo wa Kimataifa.

2. **LINAZIPONGEZA** Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jamhuri ya Laiberia kwa kuchaguliwa kuwa Wajumbe Wasio wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2026–2027.

3. **PIA, LINAZIPONGEZA** Jamhuri ya Angola, Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, Jamhuri ya Mauritius na Jamhuri ya Afrika Kusini kwa kuchaguliwa kuwa Wajumbe wa Baraza la Haki za Binadamu kwa kipindi cha 2026–2028.

4. **VILEVILE LINAIPONGEZA** Jamhuri ya Kiarabu ya Misri kwa uchaguzi wa **Dkt. Khaled El-Anany** katika Nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) kwa kipindi cha 2026–2031.

5. **LINAREJELEA** uamuzi wake EX.CL/1516(XLIV) wa Februari 2024 ulioidhinisha maombi ya Jamhuri ya Zimbabwe kwa nafasi isiyo ya Kudumu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha 2027–2028, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, na **LINASISITIZA** kutoa msaada wake kamilifu kwa maombi hayo;
6. **LINAZIAGIZA** nchi zote wanachama kuendelea kuunga mkono Kamati hii muhimu ili kutimiza dhamira yake kwa kuzingatia kanuni za Uafrika na umoja wa Afrika.
7. **PIA LINAYAAGIZA** Makundi ya Afrika huko New York na Geneva kuendelea kushirikiana kwa karibu na Sekretarieti ya Kamati, iliyo chini ya Idara ya Masuala ya Kisiasa, Amani na Usalama (DPAPS), na kuwianisha miongozo yao ya ndani ya kazi na Sheria za taratibu zilizopitishwa.

8. **LINAIDHINISHA WAGOMBEA WA SERIKALI WALIOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

   A. Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Kamisheni ya Maendeleo ya Kijamii (CSOED) kwa kipindi cha 2027–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya wa:

   - **Jamhuri ya Ghana** (Kanda ya Afrika Magharibi)
   - **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo** (Kanda ya Afrika ya Kati)
   - **Jamhuri ya Tunisia** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
   - **Jamhuri ya Malawi** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
   - **Jamhuri ya Kenya (**Kanda ya Afrika Mashariki**)**

**B.** Kwa nafasi ya **Makamu wa Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa wakati wa Mkutano wa 81 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Gaboni** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Zimbabwe** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Jamhuri ya Cabo Verde** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Mauritius** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**C.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Bodi ya Kuratibu ya Mpango wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa wa VVU/UKIMWI (UNAIDS) kwa kipindi cha 2027–2029,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Burundi** (Kanda ya Afrika ya Kati)

**D.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamisheni ya Takwimu kwa kipindi cha 2027–2030,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Equatorial Guinea** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu ya Algeria** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Côte d'Ivoire** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**E.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamisheni ya Idadi ya Watu na Maendeleo kwa kipindi cha 2028–2031**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Gambia** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**F.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake (CSW) kwa kipindi cha 2027–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kameruni** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Namibia** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Jamhuri ya Benin** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**G.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Bodi ya Uendeshaji ya Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Watoto (UNICEF) kwa kipindi cha 2027–2029**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Senegal** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Shirikisho la Ethiopia (**Afrika Mashariki**)**

**H.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Bodi ya Uendeshaji ya UNDP, UNFPA, na UNOPS kwa kipindi cha 2027–2029**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**I.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Bodi ya Uendeshaji ya Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa kipindi cha 2027–2029**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Zimbabwe** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**J.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Asasi Zisizo za Sserikali (NGOs) kwa kipindi cha 2027–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kameruni (**Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Afrika Kusini** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Jamhuri ya Côte d'Ivoire** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Tunisia** (Kanda ya Afrika Kaskazini)

**K.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo kwa kipindi cha 2027–2030,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Djibouti** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Uganda** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Nchi ya Libya** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Malawi** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**L.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamisheni ya Masuala ya Kuzuia Uhalifu na Haki za Jinai** (CCPCJ) **kwa kipindi cha 2027–2029**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kameruni** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Gaboni** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Rwanda(**Kanda ya Afrika Mashariki**)**
- **Jamhuri ya Kenya** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Afrika Kusini**(Kanda ya Afrika ya Kusini)

**M.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kikosikazi cha Kimataifa cha Wataalamu kuhusu Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu na Utoaji Ripoti (ISAR) kwa kipindi cha 2027–2029**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Aprili 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Ufalme wa Moroko** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Gambia** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**N.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Kiuchumi na Kijamii la Umoja wa Mataifa (ECOSOC) kwa kipindi cha 2027–2029,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, maombi ya:

- **Ufalme wa Moroko** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Guinea** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Senegali** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Angola** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**O.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Kiserikali ya UNESCO kwa Uhifadhi wa Urithi wa Utamaduni Usioshikika kwa kipindi cha 2026–2029,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini Paris, Ufaransa, maombi ya:

- **Jamhuri ya Tunisia** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Shirikishi la Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**9. LINAZINGATIA MAOMBI YA SERIKALI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

**A.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Umoja wa Kimataifa la Mawasiliano ya Simu (ITU) kwa kipindi cha 2027–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika **Juni 2026**, mjini **Doha, Qatar**, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kenya** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Maurius** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Muungano ya Tanzania(**Kanda ya Afrika Mashariki**)**
- **Jamhuri ya Cote d’Ivoire (**Kanda ya Afrika Magharibi**)**
- **Jamhuri ya Ghana** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Nchi ya Libya** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu ya Algeria** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Ufalme wa Moroko** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Senegali** (Kanda ya Afrika Magharibi)

- **Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Afrika Kusini (Kanda ya Kusini mwa Afrika)**

**B.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Tume ya Kujenga Amani (PBC) chini ya ECOSOC ya UN kwa kipindi cha 2027–2028**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika **Desemba 2026**, mjini **New York, Marekani,** maombi ya:

- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Uganda** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**A.** Kwa kuwa **na Makao Makuu ya Kituo cha Ushauri kuhusu Uamuzi wa Migogoro ya Uwekezaji wa Kimataifa, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Septemba 2026,** mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Moroko** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Ghana (**Kanda ya Afrika Magharibi**)**
- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (**Kanda ya Afrika ya Kati**)**

**D.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Haki za Binadamu kwa kipindi cha 2027–2029,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Ghana** (Kanda ya Afrika Magharibi) **– Kuchaguliwa tena**
- **Jamhuri ya Zambia** (Kanda ya Afrika ya Kusini)
- **Jamhuri ya Burundi** (Kanda ya Afrika ya Kati) **– Kuchaguliwa tena**

**E.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Haki za Binadamu kwa kipindi cha 2028–2030**, katika uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2027, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Nchi ya Rwanda** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Kenya** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**F.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Haki za Binadamu kwa kipindi cha 2029–2031**, katika uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2028, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Nchi ya Libya** (Kanda ya Afrika Kaskazini)

**G.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Bodi ya Utendaji ya UNESCO kwa kipindi cha 2027–2031**, katika uchaguzi utakaofanyika Novemba 2026 mjini Paris, Ufaransa, maombi ya:

- **Jamhuri ya Senegal** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Tunisia** (Kanda ya Afrika Kaskazini)

**H.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Urithi wa Dunia ya UNESCO kwa kipindi cha 2029–2033,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 2028 mjini Paris, Ufaransa, maombi ya:

- **Jamhuri ya Tunisia** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria (**Kanda ya Afrika Magharibi**)**

**I.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Mamlaka ya Kimataifa ya Sakafu ya Bahari (ISA) kwa kipindi cha 2027–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika **Novemba 2026**, mjini **Kingston, Jamaika**, maombi ya:

- **Jamhuri ya Ghana** (Kanda ya Afrika Magharibi) ***Kuchaguliwa tena***

**J.** Kwa Nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Programu na Uratibu kwa kipindi cha 2027–2029, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 2026, mjini New** York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kameruni** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Djibouti** (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Afrika Kusini** (Kanda ya Kusini mwa Afrika)
- **Jamhuri ya Guinea** (Kanda ya Afrika Magharibi)

**K.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Mikutano kwa kipindi cha 2027–2029**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya

- **Jamhuri ya Senegal** (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Ufalme wa Eswatini** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**L.** Kwa nafasi ya **Mjumbe Asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2028–2029,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2027, mjini New York, Marekani, maombi ya

- **Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria (**Kanda ya Afrika Magharibi
- **Ufalme wa Moroko** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Nchi ya Libya** (Kanda ya Afrika Kaskazini)

***ZINGATIA: Kanda ya Afrika Kaskazini inashauriwa kujadiliana na kukubaliana kuwa na mgombea*** *MMOJA* ***kwa nafasi hii. Kundi la Afrika mjini New York linaombwa kushughulikia suala hili na kutoa ripoti kwa Kamati ya Mawaziri.***

**M.** Kwa nafasi ya **Mjumbe Asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2029–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2028, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**N.** Kwa nafasi ya **Mjumbe Asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2030–2031**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2029, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria (**Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Burundi** (Kanda ya Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Chad** (Kanda ya Afrika ya Kati)

**O.** Kwa nafasi ya **Mjumbe Asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2031–2032**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2030, mjini New York, Marekani, maombi ya

- **Jamhuri ya Afrika Kusini** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**P.** Kwa nafasi ya Mjumbe **Asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2032–2033, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2031, mjini New York, Marekani**, maombi ya

- **Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania (Kanda ya Afrika Kaskazini)**

**Q.** Kwa nafasi ya **Mjumbe Asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2033–2034,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2032, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Uganda** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**R.** Kwa nafasi ya **Rais** wa **Mkutano wa 84 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (PGA84) kwa kipindi cha 2029–2030,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2029, mjini New York, maombi ya:

- **Jamhuri ya Afrika Kusini** (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**S.** Kwa nafasi ya **Rais wa Mkutano wa 89 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (PGA89)** kwa **kipindi cha 2034–2035**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2034, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Kanda ya Afrika Kaskazini)
- **Jamhuri ya Burundi** (Kanda ya Afrika Mashariki)

**10. LINAIDHINISHA MAOMBI BINAFSI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

- Kwa Nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Nchi za Kiislam (OIC) kwa kipindi cha mwaka 2027-2032 , kwa uchaguzi utakaofanyika Aprili 2026 jijini Bagdag, Iraq, maombi ya:

  - **MHE. Bwn. Ismail Ould Cheikh Ahmed** kutoka Jamhuri ya Kiislam ya Mauritania (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)

- Kwa nafasi ya Mjumbe wa Bodi ya Kimataifa ya Kupambana na Madawa ya kulevya (INCB) kwa kipindi cha 2027-2032, kwa uchaguzi utakaofanyika Aprili 2026 ,New York, USA, jina na mgombea:
  - **Professor ZEBICHE Younes** wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Algeria (Kanda ya Afrika ya Kaskazini)

- Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) kwa kipindi cha 2027–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, mgombea

  - **Dkt. Brenda Akia** wa Jamhuri ya Uganda (Kanda ya Afrika Mashariki) – **Kuchaguliwa tena**
  - **Wakili ON Sepanya Mogale** wa Jamhuri ya Afrika Kusini (Kanda ya Afrika ya Kusini)
  - **Bi. Esther Eghobamien Mshelia** wa Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria (Kanda ya Afrika Magharibi) – **Kuchaguliwa tena**
  - **Balozi Nada Deraz** wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri (Kanda ya Afrika Kaskazini) – **Kuchaguliwa tena**

- Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Baraza la Haki za Binadamu** kwa **kipindi cha 2027–2030,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, mgombea:

  - **Mhe. Bw. Delbe Zirignon Constant** wa Jamhuri ya Côte d'Ivoire (Kanda ya Afrika Magharibi)
  - **Bi. Tchamdja Kobauyah Epouse Kpatcha** wa Jamhuri ya Togo (Kanda ya Afrika Magharibi)

- Kwa nafasi ya **Jaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Sheria ya Bahari (ITLOS) kwa kipindi cha 2026–2035**, unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, jina la mgombea:

  - **Dkt. Sylvia Adusu** wa Jamhuri ya Ghana (Kanda ya Afrika Magharibi)
  - **Prof. Slim Laghmani** wa Jamhuri ya Tunisia (Kanda ya Afrika Kaskazini)

- Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD) kwa kipindi cha 2027–2030,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, mgombea:

  - **Bi. Rigbe Gebrehawaria Hagos** wa Jamhuri ya Shirikisho ya Kidemokrasia ya Ethiopia (Kanda ya Afrika Mashariki

- **Bwn**. **Abdel Rahman Ourou Bare** wa Jamhuri ya Benin (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Bwn**. **Robert Ssewagudde Mukasa** wa Jamhuri ya Uganda (Kanda ya Afrika Mashariki)

- Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (CESCR) kwa kipindi cha 2027–2030,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

  - **Dkt. Abdi Jibril Ali** wa Jamhuri ya Shirikisho ya Kidemokrasia ya Ethiopia (Kanda ya Afrika Mashariki)

- Kwa nafasi ya **Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Tatu (Masuala ya Kijamii, Kibinadamu & Kitamaduni) ya Mkutano wa 81 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

  - **Bi. Flavia Umulia** wa Jamhuri ya Rwanda (Kanda ya Afrika Mashariki)

- Kwa nafasi ya **Mwenyekiti wa Kamati ya Nne (Maalum Siasa na Utoaji Ukoloni) ya Mkutano wa 81 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

  - **Mhe. Balozi Coly Seck** wa Jamhuri ya Senegal (Kanda ya Afrika Magharibi)

- Kwa nafasi ya **Mwenyekiti wa Kamati ya Tano (Utawala na Bajeti) ya Mkutano wa 81 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

  - **Bw. Syndoph P. Endoni** wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria (Kanda ya Afrika Magharibi)

- Kwa nafasi ya **Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sita (Sheria) ya Mkutano wa 81 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Juni 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

  - **Bi. Mantsho Annastacia Motsepe** wa Jamhuri ya Afrika Kusini (Kanda ya Afrika ya Kusini)

**11. LINAZINGATIA MAOMBI MAPYA BINAFSI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

i. Kwa nafasi ya **Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kimataifa la Sukari (ISO) kwa kipindi cha 2027–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Desemba 2026, mjini London, Uingereza, maombi ya:
   - **Bw. Devesh Dukhira** wa Jamhuri ya Mauritius (Kanda ya Afrika Mashariki

ii. Kwa nafasi ya **Mjumbe na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Kimataifa ya Utumishi wa Umma ya Umoja wa Mataifa (ICSC) kwa kipindi cha 2027–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 2026, mjini New York, Marekani, mgombea

   - **Bw. Ali Ayad Ali Kurer** wa Nchi ya Libya (Kanda ya Afrika Kaskazini)
   - **Balozi Andrew Gbebay Bangali** wa Jamhuri ya Sierra Leone (Kanda ya Afrika Magharibi)
   - **Balozi Zéphyrin Maniratanga** wa Jamhuri ya Burundi (Kanda ya Afrika ya Kati)
   - **Balozi Sidi Mohamed Laghdaf** wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania (Kanda ya Afrika Kaskazini)
   - **Bi. Henrietta Maria de Beer** wa Jamhuri ya Zimbabwe (Kanda ya Afrika ya Kusini)

   ***ZINGATIA*: *Nafasi mbili zimetengwa kwa ajili ya Afrika na hakuna maelekezo ya mgawanyo wa kijiografia kwa nafasi hii.***

**iii.** Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati Huru ya Ushauri ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa (AAC) kwa kipindi cha 2026–2029**, katika uchaguzi unaofanyika Novemba 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya

   - **Dkt. Oduro Osae** wa Jamhuri ya Ghana (Kanda ya Afrika Magharibi)

iv. Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kitengo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Umoja wa Mataifa (JIU)** kwa kipindi cha 2028–2032, katika uchaguzi utakaofanyika Novemba 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

   - **Bw. Gaeimelwe Goitsemang** wa Jamhuri ya Botswana (Kanda ya Afrika ya Kusini) – ***Kuchaguliwa tena***
   - **Mhe. Balozi Amr Ramadan** wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri (Kanda ya Afrika Kaskazini)

v. Kwa nafasi ya **Katibu Mkuu wa Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu (ITU) kwa kipindi cha 2027–2030,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Julai 2026, mjini Abuja, Nigeria, maombi ya:

   - **Bw. Kezias Mwale** wa Jamhuri ya Zambia (Ukanda wa Kusini mwa Afrika)
   - **Bi. Cynthia Lesufi wa Jamhuri ya Afrika Kusini** (Ukanda wa Kusini mwa Afrika)

vi. Kwa nafasi ya **Mkurugenzi wa Bodi ya Maendeleo ya Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu (ITU) Ofisi ya Maendeleo (DB) kwa kipindi cha 2027–2030**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 2026, mjini Doha, Qatar, maombi ya:

- **Dkt. Cosmas L. Zavazava** wa Jamhuri ya Zimbabwe (Kanda ya Afrika ya Kusini**)**

vii. Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Bodi ya Kanuni za Redio ya Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu kwa kipindi cha 2027–2030,** katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 2026, mjini Doha, Qatar, maombi ya:

- **Mch. Inj. Edmund Yirenkyi Fianko** wa Jamhuri ya Ghana (Kanda ya Afrika Magharibi) ***Kuchaguliwa tena***
- **Bi. Sana Zairi** wa Ufalme wa Moroko (Kanda ya Afrika Kaskazini)

viii. Kwa nafasi **ya Jaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kwa kipindi cha 2027–2036**, katika uchaguzi uliofanyika Desemba 2026, New York, Marekani, maombi ya wa:

- **Bi. Evelyn Ama Ankumah** wa Jamhuri ya Ghana (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Bi. Rosette Muzigo Morrison** wa Jamhuri ya Uganda (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Mhe. Jaji Dkt. Deo John Nangela** wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Kanda ya Afrika Mashariki)

ix. Kwa nafasi ya **Jaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) kwa kipindi cha 2028–2036**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Prof. Phoebe Okowa** wa Jamhuri ya Kenya (Kanda ya Afrika Mashariki)
- **Prof. Paul Kuruk** wa Jamhuri ya Ghana (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Dkt. Taoheed Olufemi Elias** wa Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria (Kanda ya Afrika Magharibi)
- **Prof. Charles Chernor Jalloh** wa Jamhuri ya Sierra Leone (Kanda ya Afrika Magharibi)

x. Kwa nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Ushauri wa Masuala ya Utawala na Bajeti (ACABQ) kwa kipindi cha 2027–2029**, katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 2026, mjini New York, Marekani, maombi ya

- **Bw. Felix Eboa** wa Jamhuri ya Kameruni (Kanda ya Afrika ya Kati)

***ZINGATIA: Awali Baraza Kuu liliidhinisha maombi ya Balozi Osama Abdelkhalek wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri (Kanda ya Afrika Kaskazini), Bw. Adou Mohamed Ali wa Jamhuri ya Djibouti (Kanda ya Afrika Mashariki).***

xi. Kwa nafasi ya Mjumbe wa Kamisheni ya Sheria za Kimataifa (ILC) kwa kipindi cha 2028-2032, kwa uchaguzi utakaofanyika November 2027,New York, USA, jina la Maombi ya:
- **Prof**. **Dr. Mohamed S. Helal** kutoka Jamhuri ya Kiarab ya Misri (Kanda ya Kaskazini)

xii. Kwa ajili ya Nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa kipindi cha 2027–2031, katika uchaguzi utakaofanyika Julai 2027 mjini Roma, Italia, maombi ya:
- **Mhe. Balozi Josefa Leonel Correia Sacko** wa Jamhuri ya Angola (Kanda ya Afrika ya Kusini)

## 12. MASUALA MENGINE

**Baraza,**

**A. LINAPONGEZA** kazi ya Sekretarieti ya Kamati ya Mawaziri ya Wagombea wa Afrika katika Mfumo wa Kimataifa, inayoongozwa na Jamhuri ya Botswana, pamoja na Sekretarieti yake iliyoko chini ya uongozi wa Kamishna wa Masuala ya Kisiasa, Amani na Usalama.

**B. LINATOA WITO** kwa nchi zote wanachama kuendelea kutoa msaada wa kisiasa unaohitajika kwa Kamati, kwa msingi wa umoja wa Afrika na lengo kuu la kuhakikisha uimara wa Afrika katika Mfumo wa Kimataifa.

**C. LINAIAGIZA** PRC kutenga bajeti na rasilimali watu ya kutosha ili kusaidia shughuli za Kamati ya Mawaziri ya Wagombea wa Afrika katika Mfumo wa Kimataifa.

**D. LINAYAAGIZA** Makundi ya Afrika huko Geneva na New York kulinganisha muundo wa Kamati ya Wagombea na Muundo wa Kamati ya Mawaziri.

**E. LINAIAGIZA** Kamisheni kuzindua haraka mfumo wa kielektoni (E-Portal) na kuandaa mwongozo wa mafunzo kwa ajili ya matumizi ya Nchi Wanachama.

**UAMUZI WA BARAZA KUU KUHUSU HALI YA UTEKELEZAJI WA AJENDA 2063 NA RIPOTI YA KWANZA YA UTENDAJI WA MIAKA MIWILI YA MPANGO WA PILI WA UTEKELEZAJI WA MIAKA KUMI (STYIP)**
**Doc.EX.CL/1690(XLVIII)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamati ya Ufuatiliaji ya Mawaziri kuhusu utekelezaji wa Ajenda 2063.

2. **LINAZINGATIA PIA** matokeo ya awali ya Ripoti ya kwanza ya Utendaji ya Miaka Miwili (2024-2025) kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) wa Ajenda 2063 na ripoti ya Kikosi Kazi cha Ufundi (TWG) kwa mwaka 2025 ambayo inajumuisha, Hali ya Utekelezaji wa Maamuzi kwenye Mradi Maalum wa Ajenda 2063.

3. **LINAIPONGEZA** Kamati ya Ufuatiliaji ya Mawaziri kuhusu utekelezaji wa Ajenda ya 2063, Kamati ya Mabalozi na wawakilishi wa Kinara wa Ajenda 2063 kwa uongozi na mwongozo wao kuhusu Ajenda 2063.

4. **LINAMPONGEZA PIA** Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na uongozi wa washirika na taasisi zote zinazoendelea kutoa rasilimali zao za kifedha na kiufundi kwa kazi ya Kikosi Kazi cha Kiufundi kuhusu Ajenda 2063.

5. **LINAZIPONGEZA ZAIDI** Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs), Vyombo vya Umoja wa Afrika, washirika na TWG kwenye Ajenda 2063 kwa ushiriki wao katika kuandaa ripoti ya kwanza ya kila baada ya miaka miwili, pamoja na uwasilishaji kutoka Nchi Wanachama arobaini na moja (41), Vyombo vya Umoja wa Afrika na RECs, na hivyo kuimarisha ripoti za bara zenye msingi wa ushahidi.

6. **LINAZINGATIA KWA MASIKITIKO** kwamba, licha ya maendeleo katika Marajio kadhaa, utendaji wa jumla wa STYIP wakati wa kipindi cha 2024-2025 unabaki chini ya kasi inayohitajika ili kufikia malengo ya Ajenda 2063, kutokana na udhaifu wa uchumi mkuu, misukosuko ya tabianchi, ukosefu wa usalama, ufadhili mdogo na uwezo mdogo wa kitaasisi.

7. **LINAKUMBUSHA** uamuzi EX.CL/Dec. 1260 (XLIV) ambao uliidhinisha kuongeza "Mradi Maalum" ili kutekeleza STYIP ya Ajenda 2063 na **KUIOMBA** Kamisheni kuwasilisha bajeti kamili ya kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa "Mradi Maalum".

8. **LINAKUMBUSHA PIA** uamuzi EX.CL/Dec.1307 (XLVI), ambao ulipitisha Mifumo na zana muhimu za STYIP ya Ajenda 2063, yaani Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini, Kitabu cha Viashiria, Mkakati wa Utangazaji na Utetezi wa Mawasiliano, Miongozo ya Utawala wa Ndani na baadaye Mkakati wa Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani (DRM), iliyoidhinishwa kupitia uamuzi EX.CL/Dec.1315(XLVII)

na **LINAAMUA** kwamba mfuko maalum uanzishwe ili kutekeleza zana zilizoidhinishwa za STYIP kwa gharama ya dola milioni 5 za Kimarekani, fedha zinapaswa kupatikana ili kuanza mwaka wa 2026 kupitia chanzo cha fedha kinachopatikana ambacho kinajumuisha michango ya hiari kutoka kwa Nchi Wanachama na Taasisi za kifedha za Afrika ili kufidia muda uliopotea kwani zana hizo zilitarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka 2024.

9. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama na RECs kuharakisha kuingiza STYIP kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa na Kikanda, bajeti na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini, kuimarisha mifumo ikolojia ya data ya kitaifa, kuhakikisha zinaripoti kwa wakati na ubora kwa kutumia zana na vyombo vilivyopitishwa vya bara, na kutekeleza Mkakati wa DRM ili kupunguza utegemezi wa ufadhili wa nje.

10. **LINAKUMBUSHA ZAIDI** uamuzi wake EX.CL/Dec.1307(XLVI) uliohimiza Kamisheni na AUDA-NEPAD kukamilisha utafiti wa upembuzi yakinifu wa Ajenda ya Mfuko wa Maendeleo wa 2063 na hivyo kutaka Kamisheni na AUDA-NEPAD kuharakisha kukamilisha utafiti wa upembuzi yakinifu na wadau husika kwa ajili ya kupitishwa katika Kikao kijacho cha Baraza Kuu mwezi Juni 2026. Zaidi ya hayo, **LINAZIELEKEZA** Kamisheni na AUDA-NEPAD kuharakisha juhudi katika kuhamasisha na kupeleka rasilimali za kiufundi na kifedha katika utekelezaji wa miradi na programu kuu za STYIP ya Ajenda 2063.

11. **LINAAMUA PIA** kwamba muda wa kuripoti uongezwe kwa Nchi Wanachama na RECs ambazo hazijaripoti na **KUIOMBA** Kamisheni kuzisaidia Nchi hizi Wanachama.

12. **LINAIPONGEZA** Kikosi Kazi cha Kiufundi kuhusu Ajenda 2063, kwa kuendeleza hatua madhubuti za kusaidia utekelezaji wa pamoja wa Ajenda 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu na **KUIOMBA** Kamisheni kuasisi zaidi mifumo ya kusaidia utekelezaji thabiti wa Ajenda 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

13. **LINABAINISHA** kasi ndogo ya utekelezaji wa Miradi Kinara ya Ajenda 2063 ambayo inahusisha mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na; uidhinishaji unaosuasua, ufadhili mdogo wa miradi inayotumia mtaji mkubwa na ujuzi na uwezo mdogo na **KUZITAKA** Nchi Wanachama kuharakisha uidhinishaji na kutoa ufadhili wa kutosha kwa Miradi hiyo.

14. **LINAKUMBUSHA** uamuzi wake EX.CL/Dec.1315 (XLVII) wa Julai 2025 ambao ulielekeza kwamba mapendekezo mapya ya miradi kinara ya Ajenda 2063 yafuate utaratibu unaofaa. Katika suala hili, **LINAIELEKEZA** miundo yote ya AU, Makamishna wa AU na idara/kurugenzi zingine, zikifanya kazi kwa karibu na OSPD kama Sekretarieti ya Ufuatiliaji ya Mawaziri wa Ajenda 2063, ili kuhakikisha uzingatiaji wa masharti ya Uamuzi huu.

15. **LINAWAELEKEZA** Makamishna na Vyombo vyote vya Umoja wa Afrika kushiriki kikamilifu katika kutoa uongozi wa kimkakati katika nafasi zao husika kwa ajili ya

utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP) wa Ajenda 2063, na kuimarisha upatanifu na ushirikiano na Kikoso Kazi cha Kiufundi cha Ajenda 2063 (TWG) chini ya uongozi wa Ofisi ya Mipango na Uwasilishaji wa Mikakati (OSPD).

**16.** **LINAPITISHA** miradi kinara iliyopendekezwa; fidia kwa ajili ya biashara ya utumwa kuvuka bahari ya Atlantiki, ukoloni na ubaguzi wa rangi na Programu Kamili ya Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP) kama miradi ya Kitaifa ya Ajenda 2063 na **KUIELEKEZA** Kamisheni kuhakikisha ulinganifu wa miradi hii miwili kinara na ratiba ya STYIP na **KUTOA WITO** kwa Kamisheni kuwasilisha orodha ya mwisho na kutoa taarifa mpya kuhusu miradi yote ya Kitaifa kwenye kikao kijacho cha Uratibu wa Nusu-Mwaka mnamo Julai 2026.

**17.** **LINATAMBUA** jukumu kubwa la RECs kama wahusika wakuu katika uratibu, usaidizi wa kiufundi, na ulinganifu wa kikanda katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi ya Ajenda 2063, na **KUITAKA** Kamisheni na washirika, kwa kushirikiana na RECs, kuimarisha mifumo ya kikanda ya ufuatiliaji, ujifunzaji wa rika, na usaidizi wa umiliki wa kitaifa, sambamba na vipaumbele vya bara.

**18.** **LINASISITIZA** kwamba utekelezaji mzuri wa Ajenda 2063 na Mpango wake wa Pili wa Miaka Kumi unahitaji rasilimali fedha na watu wa kutosha, unaotabirika, na endelevu, na **KUIOMBA** Kamisheni, kwa kushauriana na Nchi Wanachama na RECs, kutambua mifumo bunifu ya ufadhili, ikiwa ni pamoja na vyombo vya kikanda na ushirikiano wa kimkakati, ili kusaidia zana za uendeshaji, majukwaa, na misheni za uwandani.